**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# HALI YA UCHUMI NA MAENDELEO YA JAMII
# MKOA WA DODOMA

**Kimetayarishwa kwa Ushirikiano Kati ya:**

**TUME YA MIPANGO**
**DAR ES SALAAM**
**na**
**OFISI YA MKUU WA MKOA**
**DODOMA**

## YALIYOMO

**Ukurasa**

1.1 **DIBAJI** ..................... v

## SURA YA KWANZA

## 1.0 ARDHI, WATU, HALI YA MAZINGIRA NA KANDA ZA KIUCHUMI ZA KILIMO

1.1 UTANGULIZI: ..................... 1
1.2 ENEO NA UMBILE LA MKOA ..................... 3
1.3 MAENEO YA UTAWALA ..................... 5
1.4 MUUNDO WA IDADI YA WAKAZI ..................... 7
1.5 HALI YA HEWA MIMEA NA KANDA ZA KILIMO NA UCHUMI ..................... 20
1.5.1 Hali ya Hewa: ..................... 20
1.5.2 Hali ya Hewa: ..................... 21
1.5.3 Maumbile ya Mkoa: ..................... 20
1.5.4 Mfuko wa Mtiririko wa Maji: ..................... 23
1.5.5 Hali ya Mimea: ..................... 24
1.5.6 Kanda za Kilimo na Uchumi: ..................... 24

## SURA YA PILI

## 2.0 UCHUMI WA MKOA

2.1 UTANGULIZI: ..................... 31
2.2 PATO LA MKOA NA WASTANI WA PATO KWA MTU: ..................... 29
2.3 VIGEZO VYA MAENDELEO YA KIJAMII NA KIUCHUMI ..................... 43
2.3.1 Ukaribu wa huduma za msingi za kijamii: ..................... 43
2.3.2 Hali ya Kijamii na Kiuchumi ..................... 45
2.3.3 Nafasi za Kazi: ..................... 48

## SURA YA TATU


**3.0 MIUNDO MBINU YA SEKTA YA KIUCHUMI**

3.1 MTANDNAO WA BARABARA: ..... 50

3.2 HUDUMA ZA RELI: ..... 54

3.3 HUDUMA ZA ANGA: ..... 54

3.4 VIFAA VYA MAWASILIANO ..... 55

3.5 NISHATI: ..... 49


## SURA YA NNE


**4.0 HUDUMA ZA JAMII ..... 59**

4.1 SEKTA YA ELIMU ..... 59

4.1.1 Elimu ya Msingi ..... 59

4.1.2 Elimu ya Shule za Sekondari ..... 70

4.1.3 Taasisi za Mafunzo ..... 77

4.1.4 Elimu ya Watu Wazima ..... 78

4.2 SEKTA YA AFYA ..... 89

4.2.1 Hali ya Afya Mkoani ..... 89

4.2.2 Msambao na Mahitaji ya Huduma za Afya ..... 99

4.2.3 Utaratibu wa Huduma za Afya ..... 101

4.2.4 Huduma za Kinga ..... 104

4.2.5 Matatizo yanayoikabili Sekta ya Afya ..... 107

**4.3 SEKTA YA MAJI NA USAFI NA TAKA ..... 108**

4.3.1 Hali Halisi Ilivyo ..... 98

4.3.2 Huduma ya Maji Vijijini ..... 113

4.3.3 Huduma Za Maji Mijini ..... 116


## SURA YA TANO


**5.0: SEKTA ZA UZALISHAJI**

5.1: MAENDELEO YA KILIMO: ..... 119

5.1.1 Hali Ilivyo ..... 119

5.1.2 Ardhi inayofaa kwa kilimo: ..... 120

5.1.3 Uzalishaji wa Mazao: ..... 120

5.1.4 Mazao ya Chakula: ..... 110

5.1.5 Mbegu za Mafuta: ..... 117
5.1.6 Mazao mengine ..... 120
5.1.7 Mboga na Matunda: ..... 134
5.1.8 Zana za Kilimo: ..... 135
5.1.9 Mbegu Bora, Mbolea na Madawa: ..... 136
5.1.10 Matatizo na Uwezekano wa Kpanua Sughuli za Kilimo: ..... 137
5.1.11 Baadhi ya hatua zitakazoongeza Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo: ..... 140
5.2 MAENDELEO YA SEKTA YA MIFUGO: ..... 142
5.2.1 Utangulizi: ..... 142
5.2.2 Idadi ya Mifugo na mgawanyo wake: ..... 143
5.4.3 Vikwazo vya Maendeleo ya Mifugo Mkoani: ..... 147
5.3 MAENDELEO YA SEKTA YA MALIASILI: ..... 154
5.3.1 Utangulizi: ..... 154
5.3.2 Misitu: ..... 155
5.3.3 Upanuzi Misitu na Hifadhi ya Udongo: ..... 157
5.3.4 Kilimo na Hifadhi Misitu ..... 144
5.4 UFUGAJI NYUKI: ..... 160
5.5 U V U V I : ..... 164
5.6 RASLIMALI YA MADINI: ..... 149
5.7 WANYAMA PORI: ..... 165
5.8 MAENDELEO YA SEKTA YA VIWANDA: ..... 166

## SURA YA SITA

**6.0 MASUALA MENGINE YA MAENDELEO**
6.1: MPANGO WA UHAMIAJI MAKAO MAKUU YA SERIKALI: ..... 167
6.2 VIKUNDI VYA KIUCHUMI: ..... 169
6.3 VYAMA VYA USHIRIKA: ..... 170
6.4 WAHISANI/MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI YALIPO DODOMA ..... 171

## SURA YA SABA

**7.0 MAENEO YANAYOFAA KWA UWEKEZAJI MKOA WA DODOMA**
7.2 UZALISHAJI MIFUGO: ..... 175
7.3 UFUGAJI WA NYUKI: ..... 177
7.4 ELIMU: ..... 177
7.5 VIWANDA: ..... 178

## VIAMBATISHO

**KIAMBATISHO "A"** ..... **179**
Mkoa wa Dodoma - Kwa Ufupi ..... 179

**KIAMBATISHO "B"** ..... **183**
Wilaya ya Dodoma Mjini ..... 183

**KIAMBATISHO "C"** ..... **169**
Wilaya ya Kondoa ..... 187

**KIAMBATISHO "D"** ..... **171**
Wilaya ya Dodoma Vijijini ..... 190

**KIAMBATISHO "E"** ..... **194**
Wilaya ya Mpwapwa: ..... 194

**KIAMBATISHO "F"** ..... **198**
**1.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU TANZANIA** ..... **198**
1.1 Mahali Ilipo: ..... 198
1.2 Mipaka ya Nchi: ..... 198
1.3 Ukubwa/Eneo: ..... 198
1.4 Ukubwa wa Eneo la Kila Mkoa Tanzania Bara ..... 198
1.5 Idadi ya Watu: ..... 200
1.6 Matumizi ya Ardhi ..... 201
1.7 Ardhi Kilimo na Mifugo: ..... 201
1.8 Maziwa ..... 201
1.9 Milima ..... 201
1.10 Hali ya Hewa: ..... 202
**2.0 HUDUMA ZA JAMII** ..... **203**
2.1 Afya: ..... 203
2.2 Elimu: ..... 203
2.3 Maji: ..... 205
**3.0 HIFADHI ZA TAIFA:** ..... **205**

## *DIBAJI*

1. *Kadri tunavyoikaribia Karne ya 21, matatizo ya maendeleo vijijini katika nchi zinazoendelea kama Tanzania, ndivyo yanavyozidi kuwa mengi na makubwa. Huduma za kijamii na kiuchumi zinadidimia na hivyo kusababisha nchi hizi kukabiliwa na tatizo la kushindwa kutoa huduma hizi kwa msingi wa uendelevu. Kwa mfano, kwetu Tanzania viwango vya uandikishaji wa wanafunzi mashuleni vinazidi kushuka, hali ya upatikanaji wa chakula ni mbaya, vifo vya watoto wachanga na akina mama wajawazito vinaendelea kuongezeka, ukosefu wa ajira unaongezeka na kusababisha vijana wengi vijijini kuhamia mijini ambako tayari kuna msongamano mkubwa wa watu, n.k. Katika mkoa wa Dodoma, msongamano kwenye ardhi unazidi kuongezeka, sambamba na kutoweka kwa misitu kwa kiwango cha kutisha.*

2. *Hali hii imejitokeza kutokana na sababu mbali mbali, kama vile kukosekana kwa mipango madhubuti ya maendeleo Vijijini, pamoja na ufuatiliaji na usimamizi hafifu wa utekelezaji wa programu za maendeleo na mikakati ya kisekta. Upungufu huu katika sera na utayarishaji na utekelezaji wa programu na mipango ya maendeleo vijijini katika nchi zinazoendelea, ni matokeo ya uhaba wa takwimu na habari za kutosha na za kuaminika kuhusu masuala ya maendeleo vijijini.*

3. *Uchapishaji wa vitabu hivi vinavyoonesha hali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya kila Mkoa, ambao unafanywa na Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa, ni hatua muhimu ya kuelekea kwenye ufumbuzi wa tatizo la ukosefu na uhaba wa takwimu na taarifa muhimu.*

4. *Vitabu hivi vinatoa takwimu na taarifa za aina mbali mbali, zikiwemo za kijiografia, idadi ya watu, maendeleo ya kijamii na kiuchumi, huduma za jamii, miundombinu ya kiuchumi pamoja na sekta za uzalishaji. Machapisho haya yametokea kuhitajika sana kama chanzo muhimu cha taarifa kwa viongozi na watu wote wenye dhamana ya kutunga sera, maafisa mipango, watafiti, wahisani na viongozi wa sekta mbalimbali za maendeleo nchini. Tume ya Mipango imeona umuhimu wa kuihusisha mikoa yote katika zoezi hili muhimu. Hivyo basi wasomaji wa machapisho haya wanakaribishwa kutoa maoni yao na kukosoa kwa lengo la kuboresha maudhui ya machapisho yatakayofuata, na hivyo kuyafanya kuwa yenye msaada zaidi kwa watumiaji.*

5. *Ningependa kutumia fursa hii, kwa mara nyingine, kutambua na kutaja kwa shukrani kubwa, msaada wa kifedha kutoka ubalozi wa Norway nchini, ambao umeiwezesha Tume ya Mipango na Mkoa wa Dodoma, kutoa kitabu hiki kuelezea hali ya maendeleo ya mkoa huo. Mwisho napenda kuwashukuru sana watumishi wa Idara ya Mipango Mkoani Dodoma, kwa juhudi zao kubwa walizofanya katika kufanikisha jukumu hili.*



***Nassoro W. Malocho (MB)***
***WAZIRI WA NCHI,***
***MIPANGO NA UREKEBISHAJI WA SEKTA YA MASHIRIKA YA UMMA.***

*Septemba, 1998*

# SURA YA I

## 1.0 ARDHI, WATU, HALI YA MAZINGIRA NA KANDA ZA KIUCHUMI ZA KILIMO:

### 1.1 Utangulizi:

Wakazi asilia wa Dodoma wanazo hadithi mbalimbali zinazoelezea jinsi Dodoma ilivyopewa jina hilo. Kitabu kinachoitwa "The Hand Book of Tanganyika (1958)" kinaelezea kinagaubaga kwamba jina sahihi la Dodoma linapaswa kuwa "IDODOMA". Tafsiri ya jina hili katika lugha ya Kigogo ni "mahali ambapo kitu kilinaswa. "Hata hivyo wengine wanadai kwamba jina hilo linatokana na imani ya Kigogo kwamba Tembo alifika eneo la KIKUYU kwa ajili ya kunywa maji, lakini hatimaye akanaswa katika tope zito na kuzama. Baadhi ya wazee wa Kigogo wanadai na wakawa wanasema kuwa ilikuwa "yadodomela" ikimaanisha kwa lugha ya Kigogo kuwa "Tembo amezama".

Historia ya mkoa wa Dodoma inayokumbukwa kwa urahisi inaanzia zama za biashara ya utumwa, ambapo Dodoma ilijikuta iko kati ya mojawapo ya njia kuu za misafara ya watumwa waliokuwa wakisafirishwa kutoka Bara kwenda Mwambao wa Afrika mashariki. Mmojawapo kati ya wazungu wa kwanza kuutembelea mkoa wa Dodoma zamani hizo, alikuwa Bwana Richard Burton mwaka 1859. Kati ya mwaka 1882 na 1883 Master Mariner Hore akiwa safarini kuelekea Ziwa Tanganyika, alipitia eneo hili la Wagogo. Pia, mwaka 1889 Bwana H.M. Stanley alipopitia eneo hili la Dodoma alifurahishwa sana na mazingira yake na baadaye alinukuliwa akisema, "Hakuna nchi

yeyote katika bara la Afrika yenye mazingira yaliyonivutia mimi binafsi kama hili."

Lakini, ni kweli usiofichika kwamba mazingira ya mkoa wa Dodoma yana mvuto wa kipekee katika Tanzania, kwani wakati wa majira ya kiangazi eneo lote linakuwa na mazingira kama yale ya jangwa, na wakati wa majira ya masika, mazingira hubadilika na kuwa kijani kibichi na ya kuvutia hasa vichaka vyake vilivyo changanyikana na miti mifupi mifupi.

Hata hivyo mnamo mwezi Juni mwaka 1890 wanajeshi wa Kijerumani wakiongozwa na mwenezaji dola ya Kijerumani, Carl Peters imeandikwa kwamba "baada ya kumwaga damu nyingi wakati wa mapambano katika ardhi ya Umasaini kaskazini, askari hao hatari wa Kijerumani waliongezeka idadi yao, na wakiwa na silaha nzito nzito, walilivamia eneo la kusini na kuushinda utawala wa chifu wa Kigogo bila kipingamizi kikubwa". Kutokana na uvamizi huo wa Wajerumani, utawala wa Kigogo haukuwa na njia nyingine zaidi ya kuomba amani na wavamizi hao. Hata hivyo, Wanajeshi wa Kijerumani hawakukubali na naombi hilo la suluhu/amani badala yake waliendelea na mapambano. Inakumbukwa kwamba "waliendeleza kasi ya kuvishambulia vijiji, kupora mali na kuzichoma moto nyumba, na kuharibu vitu vyote vilivyo shindikana kuungua moto:

Baada ya kufanikisha uvamizi huo na hatimaye kuitwa ardhi yote ya Wagogo, utawala wa Kijerumani iliweka makao makuu yao ya kwanza. Mpwapwa upande wa Mashariki, na hapo baadaye waliyaweka Kilimatinde upande wa Magharibi wa eneo walilolitwaa. Katika mwaka 1902, utawala huo ulijenga kambi

kubwa ya kijeshi Kondoa upande wa kaskazini wa himaya waliyoitwaa. Ni kwa sababu hizo mwaka 1912 Dodoma ikafanywa makao makuu ya wilaya ya Jimbo la Kati la Tanganyika. Hata hivyo ilikuwa ni wakati wa utawala wa Kiingereza, mwaka 1958 ndipo makao makuu ya wilaya ya Dodoma yalipopandishwa hadhi kufikia Mamlaka ya Miji. Mara baada ya Tanganyika kupata Uhuru, mojawapo ya mikoa iliyoundwa ni Dodoma, ukiwa na wilaya tatu za vijijini, yaani wilaya ya Dodoma, Kondoa na Mpwapwa, na wilaya moja ya Mji, yaani Halmashauri ya Mji wa Dodoma.

## 1.2 Eneo na Umbile la Mkoa

Mkoa wa Dodoma upo kati ya latitudo $4^o$-$7^o$ kusini mwa Ikweta na longitudo $35^o$-$37^o$ mashariki mwa Meridiani Kuu. Mkoa wa Dodoma uko katikati ya Tanzania, ukiwa umezungukwa na mikoa minne yaani Arusha, kwa upande wa Kaskazini, Morogoro kwa upande wa Mashariki. Kwa upande wa Kusini ni mkoa wa Iringa na mkoa wa Singida kwa upande wa magharibi. Sehemu kubwa ya mkoa wa Dodoma ni uwanda wa juu ambapo mwinuko unaongezeka pole pole kutoka mita 830, katika maeneo ya Bahi, hadi kufikia mita 2,000 katika maeneo ya milima ya Kondoa kaskazini.

Mvua ni za wastani, kiasi cha milimita 500-800 kwa mwaka. Hata hivyo, mvua hizo hunyesha mara moja kwa mwaka kuanzia mwezi wa Desemba hadi Machi/Aprili.


**RAMANI YA TANZANIA IKIONYESHA UMBALI KWA KILOMITA KUTOKA DODOMA**

## 1.3 Maeneo ya Utawala

Mkoa wa Dodoma ulianzishwa rasmi mwaka 1963, wakati huo ukiwa na wilaya tatu za vijijini na mamlaka moja ya mji. Hivi sasa, mkoa wa Dodoma unazo wilaya nne na Manispaa moja, ambazo ni, wilaya za Dodoma, Kondoa, Mpwapwa, Kongwa na Manispaa ya Dodoma. Wilaya mpya ya Kongwa ilianzishwa rasmi mwaka 1995.

Aidha, mkoa wa Dodoma ni wa 12 kwa ukubwa wa eneo ambapo una eneo la kilomita 41,310 za mraba, sawa na asilimia 5 ya eneo la Tanzania bara. Eneo la mkoa limegawanyika kiwilaya kama inavyoonyeshwa katika kielelezo na. I.

**Kielelezo 1: Eneo la kila wilaya Mkoa wa Dodoma**



**JEDWALI 1: UKUBWA WA ENEO KI-WILAYA MKOA WA DODOMA**

| Wilaya | Eneo Kilomita za mraba | Asilimia ya eneo la Mkoa |
|---|---|---|
| Dodoma Vijijini | 14,004 | 33.9 |
| Dodoma Mjini | 2,572 | 6.3 |
| Kondoa | 13,209 | 31.9 |
| Mpwapwa/Kongwa | 11,526 | 27.9 |
| Jumla | 41,311 | 100 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Dodoma

Wilaya nne na Manispaa moja zilizopo zimegawanyika katika Tarafa 26, Kata 136 na Vijiji 453 vilivyoandikishwa. Jedwali II linaonyesha mgawanyo wa maeneo hayo ya utawala kiwilaya.

**JEDWALI II: MGAWANYO WA MAENEO YA UTAWALA KIWILAYA 1996**

| Wilaya | Eneo Kilomita za mraba | Tarafa | Kata | Vijiji |
|---|---|---|---|---|
| Dodoma Vijijini | 14,004 | 8 | 48 | 124 |
| Dodoma Mjini | 2,572 | 4 | 30 | 38 |
| Kondoa | 13,209 | 8 | 32 | 158 |
| Mpwapwa/Kongwa | 11,526 | 3 | 15 | 73 |
| | | 3 | 11 | 60 |
| **Jumla** | **41,311** | **26** | **136** | **453** |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa

## 1.4 Hali ya Idadi ya Watu

### 1.4.1 Makabila:

Wastani wa asilimia 75 ya watu wa mkoa Dodoma ni makabila yenye asili ya kibantu. Makabila hayo ni Wagogo, Warangi, Wanguu, Wazigua, Wakaguru, na Wasagara.

Mbali ya makabila yenye asili ya kibantu, lipo pia kundi jingine lenye asili ya Kinilotiki ama Kinihamite. Kundi hili la pili lina makabila ya Wamasai, Wafyomi, Wamang'ati, Wambulu na Watatoga. Pia lipo kundi la Khoisan yaani Wasandawe. Kabila hili huishi kusini magharibi mwa wilaya ya Kondoa. Kabila la Watonga ambalo huishi kaskazini - magharibi ya wilaya ya Kondoa, hujishughulisha zaidi na uwindaji na urinaji wa asali. Hata hivyo, kabila la Wamasai ambalo hujulikana kwa uchungaji wa makundi makubwa ya mifugo wapo katika wilaya zote mkoani Dodoma.

Mbali na makundi hayo yaliyotajwa yapo pia makundi mengine kama vile Wahindi, Waarabu, Wasomali, ambao hupatikana zaidi katika maeneo na vituo vya biashara vijijini, ambako hujishhughulisha na uuzaji bidhaa na shughuli zingine za kibiashara.

### 1.4.2 Mfumuko wa Idadi ya Watu

Takwimu za mkoa wa Dodoma za Sensa za miaka ya 1948, 1957, 1967, 1978 na 1988, kama zinavyo onyeshwa katika jedwali III zinadhihirisha kwamba licha ya kushuku kwa kasi ya ongezeko la idadi ya watu, katika kipindi cha sensa ya mwaka 1978 na 1988, idadi halisi ya watu wa mkoa wa Dodoma iliongezeka karibu mara tatu katika kipindi cha miaka 1948 - 1988. Kwa kipindi hicho, idadi ya watu duniani iliongezeka mara mbili tu. Kwa kutumia kasi ya ongezeko la idadi ya watu ya asilimia 24 ya sensa ya mwaka 1988 maoteo ya idadi ya watu kwa mwaka 1996 ni 1,498,000 na matarajio ya idadi ya watu kwa mwaka 2000 ni 1,640,000 mkoani Dodoma.

Inafaa ikumbukwe kwamba kasi hii kubwa ya ongezeko la watu ambayo haiwiani na ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula, wala ongezeko la huduma za kijamii ni mojawapo ya matatizo ya kimsingi yanayopelekea ongezeko lisiloisha la umaskini mkoani. Jedwali III linaonyesha ongezeko la idadi ya watu kati ya kipindi cha sensa cha mwaka 1948 na 1988.

**JEDWALI III: ONGEZEKO LA IDADI YA WATU KITAIFA NA KIMKOA (1948-1996)**

| Mwaka | Kitaifa (000) | Mkoa wa Dodoma (000) | % | Viwango vya Ongezeko | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Kitaifa | Mkoa |
| 1948 | 7,478 | **450** | 6 | 1.8 | 1.1 |
| 1957 | 8,786 | **493** | 5.6 | 1.8 | 1.1 |
| 1967 | 12,313 | **709** | 5.8 | 3.1 | 3.3 |
| 1978 | 17,036 | **972** | 5.7 | 3.2 | 2.9 |
| 1988 | 23,058 | **1,235** | 5.3 | 2.8 | 2.4 |
| 1996(Makisio) | 28,600 | **1,498** | 5.2 | 2.8 | 2.4 |

Chanzo: Tume ya Mipango - Takwimu za Sensa ya 1948 1957, 1967, 1978 na 1988

### 1.4.3 Kasi ya Ukuaji wa Idadi ya Watu

Jedwali na. III linaonyesha kwamba, ukiacha takwimu za mwaka 1967, tokea mwaka 1948, kasi ya ukuaji wa idadi ya watu mkoa wa Dodoma ni ndogo ikilinganishwa na ile ya kitaifa. Kwa mfano, katika sensa ya mwaka 1978 na 1988 kasi ya ukuaji wa idadi ya watu mkoa wa Dodoma ilikuwa asilimia 2.9 na 2.4 ikilinganishwa na viwango vikubwa vya kitaifa vya asilimia 3.2 na 2.8 katika kipindi hicho.

Kiwilaya takwimu hizi zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 1967 - 1978 na 1978 - 1988 kasi ya ukuaji wa idadi ya watu katika wilaya ya Mpwapwa ilikuwa kubwa kuliko ilivyokuwa katika wilaya nyingine mkoani Dodoma. Wilaya ya Dodoma mjini inaonyesha kasi kubwa zaidi ya ukuaji wa idadi ya watu kati ya mwaka 1978 - 1988. Hali hii inatokana na idadi kubwa ya watu kutoka sehemu mbali mbali nchini kuhamia Dodoma kutafuta kazi kufuatia maamuzi ya serikali ya kufanya Dodoma kuwa makao makuu ya serikali mwaka 1973.


**JEDWALI IV: KASI YA UKUAJI WA IDADI YA WATU KIWILAYA**

| Wilaya | 1948-57 | 1957-67 | 1967-78 | 1978-88 |
|---|---|---|---|---|
| Dodoma Vijijini | 1.1 | 3.0 | 2.1 | 2.4 |
| Dodoma Mjini | 4.5 | 5.8 | | |
| Kondoa | 1.0 | 2.9 | 2.4 | 2.1 |
| Mpwapwa/Kongwa | 1.5 | 4.3 | 3.6 | 2.6 |
| Mkoa | 1.1 | 3.3 | 2.9 | 2.4 |

Chanzo: Kiziduo cha takwimu za 1970 na takwimu za sensa za 1978 na 1988 - Idara Kuu ya Takwimu

Kutokana na kasi ya ukuaji wa idadi ya watu kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali na. IV, maoteo ya idadi ya watu katika wilaya za Dododma (V), Dodoma (M), Kondoa na Mpwapwa/Kongwa kwa mwaka 1996 na 2000 ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali na. V.

**Kielelezo 2: Idadi ya watu (Maelfu) kiwilaya, Mkoa wa Dodoma:**




**JEDWALI V: MAENEZI YA IDADI YA WATU KIWILAYA**

| Wilaya | 1978 | 1988 | Makisio 1996 | Makisio 2000 |
|---|---|---|---|---|
| Dodoma Mjini | 156,862 | 202,399 | 245,006 | 269,388 |
| Dodoma Vijijini | 274,516 | 352,130 | 426,649 | 469,077 |
| Kondoa | 275,082 | 340,232 | 411,383 | 452,292 |
| Mpwapwa/Kong wa | 261,251 | 339,516 | 410,453 | 451,270 |
| Jumla ya Mkoa | 967,711 | 1,235,277 | 149,391 | 1,642,027 |

Chanzo: Idara Kuu ya Takwimu, Dar es Salaam"Taarifa za Sensa za Wakazi"

## 1.4.4 IDADI YA WATU KWA KILOMITA ZA MRABA

Jedwali na. VI linaonyesha kwamba, mkoa wa Dodoma una idadi kubwa ya watu katika kilomita ya mraba ikilinganishwa na mikoa mingine hapa nchini licha ya kuwa na misingi dhaifu ya kiuchumi. Jedwali na. VI pia linaonyesha kwamba Dodoma ina idadi kubwa zaidi ya watu kwa kilomita ya mraba ikilinganishwa na mikoa kama Mbeya, Iringa, Morogoro, Arusha, Ruvuma na Rukwa, mikoa inayoeleweka kuwa na misingi imara ya kiuchumi. Kwa mujibu wa Sensa ya watu ya mwaka 1988 mkoa wa Dodoma ulikuwa na jumla ya watu 1,235,277. Idadi hii inapelekea kuwa na idadi ya watu 30 kwa kila kilomita moja ya mraba, ikilinganishwa na kiwango kidogo cha wastani cha watu 26 kwa kilomita moja ya mraba kitaifa mwaka 1988.

**JEDWALI VI: MAENEZI YA IDADI YA WATU NA IDADI YA WATU KWA KILOMITA YA MRABA KIMKOA, SENSA YA 1988**

| Mkoa | Eneola Ardhi ($km^2$) | Idadi ya Watu | Wastani wa idadi ya watu kwa $km^2$ |
|---|---|---|---|
| Dar es salaam | 1,393 | 1,360,850 | 979.9 |
| Mwanza | 19,683 | 1,876,776 | 95.8 |
| Kilimanjaro | 13,309 | 1,108,699 | 83.7 |
| Mtwara | 16,710 | 887,583 | 53.2 |
| Tanga | 26,677 | 1,280,262 | 48.1 |
| Kagera | 28,456 | 1,313,639 | 46.6 |
| Mara | 21,760 | 952,616 | 43.7 |
| Shinyanga | 50,760 | 1,763,960 | 34.9 |
| **Dodoma** | **41,311** | **1,235,277** | **30.0** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mbeya | 60,350 | 1,476,261 | 24.0 |
| Kigoma | 37,040 | 853,263 | 23.1 |
| Iringa | 56,850 | 1,193,074 | 21.3 |
| Arusha | 82,098 | 1,352,225 | 16.5 |
| Rukwa | 68,635 | 704,050 | 10.1 |
| Lindi | 66,040 | 642,364 | 9.8 |
| Tabora | 76,151 | 1.036,293 | 14.0 |
| Pwani | 32,407 | 638,015 | 20.0 |
| Singida | 49,341 | 791,814 | 16.0 |
| Morogoro | 70,799 | 1,222,737 | 17.0 |
| Ruvuma | 66,477 | 783,327 | 12.0 |
| Jumla Tanzania Bara | 885,987 | 23,174,443 | 26.1 |

Chanzo: Taarifa ya Sensa 1988

Idadi ya watu kwa kilomita ya mraba mkoani Dodoma hutofautiana kati ya eneo na eneo. Yapo maeneo ambayo yana idadi ya watu chini ya kumi katika kilomita moja ya mraba, kama vile Itiso wilaya ya Dodoma vijijini, na maeneo yenye zaidi ya watu 50 kwa kilomita moja ya mraba kama maeneo yenye rutuba nzuri. Aidha maeneo yanayosemekana kuwa na idadi kubwa ya watu ni pamoja na; katikati na kusini mwa wilaya ya Kondoa, nyanda za juu za Bereko Kondoa, na sehemu kubwa ya wilaya ya Kongwa, Bahi wilayani Dodoma Vijijini, Rudi, Kibakwe na maeneo machache wilaya ya Mpwapwa. Kwa ujumla, wilaya ya Mpwapwa ndiyo yenye idadi kubwa ya watu kwa kilomita ya mraba kuliko wilaya zingine mkoani ambapo ina idadi ya watu 29.5 katika kilomita moja ya mraba, ikifuatiwa na Kondoa ambayo ina idadi ya watu 25.8 katika kilomita moja ya mraba.

**JEDWALI VII: IDADI YA WATU KWA KILOMITA YA MRABA KIWILAYA MWAKA 1967, 1978 NA 1988 MOA WA DODOMA**


| Wilaya | 1967 | 1978 | 1988 |
|---|---|---|---|
| Dodoma | 19.4 | 26.3 | 33.5 |
| Kondoa | 16.1 | 20.8 | 25.8 |
| Mpwapwa | 15.3 | 22.6 | 29.5 |
| Wastani wa Mkoa | 17.2 | 23.5 | 30.0 |

Chanzo: Makao Makuu, Takwimu, Wizara ya Uchumi na Mipango - (1972)

### 1.4.5 Maenezi ya Idadi ya Watu

Kwa mujibu wa matokeo ya sensa ya mwaka 1988, sehemu kubwa ya idadi ya watu wa mkoa wa Dodoma, takriban asilimia 89.4 wanaishi vijijini. Wanaosalia yaani asilimia 10.6 wanaishi ama Manispaa ya Dodoma au katika miji ya Kondoa, Kongwa, Mpwapwa na katika miji mingine midogo. Jedwali na. VIII linaonyesha maenezi ya idadi ya watu kiwilaya na kati ya mijini na vijijini.

**Kielelezo 3: Maenezi ya idadi ya watu (Maelfu) kati ya Mijini na Vijijini, Mkoa wa Dodoma**





**JEDWALI VIII: MAENEZI YA IDADI YA WATU KATI YA MIJINI NA VIJIJINI - 1988**

| Wilaya | Vijijini | % | Mijini | % | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Kondoa | 325,262 | 95.6 | 14,970 | 4.4 | 340,232 |
| Mpwapwa/Kongwa | 306,243 | 90.2 | 33,273 | 9.8 | 339,516 |
| Dodoma Vijijini | 327,705 | 92.8 | 25,425 | 7.2 | 353,130 |
| Dodoma Mjini | 119,213 | 58.9 | 83186 | 41.1 | 202,399 |
| Jumla | 1,104,338 | 89.4 | 130939 | 10.6 | 1,235,277 |

Chanzo: Sensa ya 1988: Sura ya Mkoa.

**Kielelezo 4: Mgawanyiko wa wakazi (Maelfu) kijinsia 1988 Mkoa wa Dodoma**




1.4.6 **Maenezi ya Idadi ya Watu kwa Jinsia:**

Uchambuzi wa takwimu za matokeo ya sensa ya mwaka 1988, umedhihirisha kwamba katika wilaya zote za mkoa wa Dodoma idadi ya wanawake ni kubwa ikilinganishwa na ile ya wanaume. Aidha, uwiano wa wanawake kwa wanaume ni 100:92

**JEDWALI IX: MAENEZI YA IDADI YA WATU KIJINSIA**

| Wilaya | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|
| Dodoma Mjini | 97,381 | 105,018 | 202,399 |
| Kondoa | 166,349 | 173,883 | 340,232 |
| Dodoma Vijijini | 164,975 | 188,155 | 352,130 |
| Mpwapwa/Kongwa | 163,114 | 176,402 | 339,516 |
| Jumla | 591,819 | 643,458 | 1,235,277 |

Chanzo: Sensa ya Watu 1988 - Sura ya Mkoa

### 1.4.7 Ukubwa wa Kaya:

Jedwali na. X linaonyesha kwamba mkoa wa Dodoma unao wastani wa watu 5.0 kwa kaya, kiwango ambacho ni kidogo kikilinganishwa na wastani wa kitaifa wa watu 5.2. Kiwango cha juu mkoani cha idadi ya watu kwa kaya ni watu 5.8 wilaya ya Mpwapwa, na kiwango cha chini kabisa ni watu 4.7 wilaya ya Dodoma Vijijini. Kimsingi, ukubwa wa kaya unategemea sana kiwango cha uzaliano nchini.

Aidha mlinganisho wa takwimu za sensa ya watu ya mwaka 1978 na 1988 unadhihirisha kwamba kiwango cha uzaliano nchini kwa ujumla kinaendelea kupungua. Kupungua kwa kiwango cha uzaliano kimechangiwa na hali ya maisha kuwa duni na kupanda kwa umri wa wanawake kuolewa kutoka umri wa miaka 19 mwaka 1978 hadi miaka 23 mwaka 1988. Hata hivyo, jedwali X linaonyesha kuwa kati ya mwaka 1978 na 1988 ukubwa wa kaya haujabadilika sana, mkoani Dodoma.

**JEDWALI X: WASTANI WA IDADI YA WATU KWA KAYA KIWILAYA**

| Wilaya | 1978 | 1988 |
|---|---|---|
| Dodoma | 4.9 | 4.7 |
| Kondoa | 4.6 | 5.0 |
| Mpwapwa/Kongwa | 5.4 | 5.8 |
| Mkoa | 4.9 | 5.0 |


Chanzo: Sensa ya Watu 1978 na 1988 - Sura za Mikoa

### 1.4.8 Makundi Tegemezi:

Jedwali na.XI linabaini kuwa watoto wenye umri kati ya miaka 0 - 14 ni asilimia 46, wakati vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 44 ni asilimia 39. Kundi la nguvu kazi ambalo hujumuisha watu wenye umri kati ya miaka 15 hadi 64 walifikia asilimia 49 ya idadi ya watu wote. Hata hivyo lile kundi tegemezi lenye umri kati ya miaka 0 hadi 14, na wale walio na umri zaidi ya miaka 65 ni sawa na asilimia 51 ya idadi ya watu wote.

Kwa tarakimu halisi maana yake ni kwamba katika mwaka 1988, mkoa wa Dodoma ulikuwa na idadi ya watu tegemezi wapatao 627,055, ambao kinadharia walikuwa wanawategemea watu wenye uwezo wa kufanyakazi karibu na idadi inayolingana ya watu 608,222.

**Kielelezo 5: Idadi ya Watu kwa rika (Maelfu) mwaka 1988, Mkoa wa Dodoma**



**JEDWALI XI: IDADI YA WATU KWA RIKA KIWILAYA, 1998**

| Wilaya | Rika | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 0-4 | 5-14 | 15-44 | 45-64 | 65+ | |
| Kondoa | 59,703 | 102,499 | 127,697 | 34,650 | 15,783 | 340,232 |
| Mpwapwa/ Kongwa | 58,993 | 101,198 | 133,939 | 30,722 | 14,664 | 339,516 |
| Dodoma Vijijini | 60,752 | 97,875 | 136,191 | 38,289 | 20,023 | 353.130 |
| Dodoma Mjini | 32,725 | 54,798 | 88,639 | 18,095 | 8,142 | 202,399 |
| Mkoa | 212,173 | 356,370 | 486,466 | 121,756 | 58,204 | 1,235,277 |

Chanzo: Takwimu za Sensa 1988 - Sura ya Mkoa

## 1.5 Hali ya Hewa Mimea na Kanda za Kilimo na Uchumi

### 1.5.1 Hali ya Hewa:

Hali ya hewa katika mkoa wa Dodoma ni savana kavu ambayo huwa na kipindi kirefu cha ukame kuanzia mwezi Aprili hadi mwezi Desemba, na kipindi kifupi cha mvua katika miezi inayosalia. Mkoa wa Dodoma, uko nyuma ya milima ya Morogoro, eneo ambalo kijiografia halipata mvua za kutosha. Katika kipindi kirefu cha ukame panakuwepo na upepo mkavu na unyevu mdogo ambao unachangia mmomonyoko wa ardhi. Nyakati za masika mvua nyingi hunyesha na kusababisha mafuriko. Kwa sababu hiyo asilimia 60 ya maji ya mafuriko hayo

hutiririka badala ya kuzama ardhini ili yasaidie mimea au kuwa chanzo cha chemchem.

Aidha wastani wa mvua katika Manispaa ya Dodoma ni milimita 570 na asilimia 85 ya wastani huu hunyesha kwa miezi minne yaani kati ya mwezi Desemba na mwezi Machi kila mwaka. Hata hivyo, katika maeneo yajulikanayo kwa kilimo kama vile Mpwapwa na Kondoa, hupata mvua nyingi zaidi.

Mvua inyeshayo mkoani Dodoma ni ndogo na pia haiaminiki, ikilinganishwa na maeneo mengine nchini hasa katika mwezi Januari, ambapo mvua ya kutosha ni muhimu sana kwa kupandia mbegu. Ni kwa sababu hiyo ya kutokuwa na mvua za kuaminika kulikopelekea kilimo kutoaminika na hivyo kuuwia vigumu mkoa kuendeleza na kuboresha uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

### 1.5.2 Hali ya Hewa:

Hali ya hewa mkoani Dodoma hutofautiana kutokana na mwinuko ambapo kwa ujumla wastani wa juu wa joto ni nyuzi joto 31 sentigredi (mwezi Oktoba) na wastani wa chini ni nyuzi joto 18 sentigredi (mwezi Desemba). Katika kipindi cha jua kali wastani wa juu wa joto ni kati ya nyuzi joto $27^{o}$ hadi 28 sentigredi na wastani wa chini wa joto ni kati ya nyuzi joto 10 hadi 11 sentigredi. Kati ya mwezi Juni na Agosti hali ya joto mchana huweza kufikia nyuzi joto 35 sentigredi na usiku hubadilika hadi kufikia nyuzij oto 10 sentigredi, hasa katika maeneo yenye vilima.

### 1.5.3 Maumbile ya mkoa:

Eneo lote la mkoa wa Dodoma liko ndani ya mwinuko tambarare uliyopo katikati ya Afrika Mashariki, ambapo mwinuko huo umeanzia nchini Ethiopia kwa upande wa kaskazini hadi Transevaal nchini Afrika ya Kusini kwa upande wa kusini. Kwa hali halisi ilivyo, mkoa umeenea katika safu nyingi za milima iliyoko kaskazini magharibi ya mkoa, kama vile safu za milima ya Mbulu zenye urefu upatao mita 1800 juu ya usawa wa bahari. Mbuga zilizoinuka za Masai zinaendelea hadi kaskazini na kaskazini mashariki ya mkoa wa Dodoma. Miinuko ya Mbulu kuelekea kusini imegawanyika katika safu mbili za milima; safu inayoambaa kaskazini mashariki ya mkoa, na safu nyingine ni ile inayokatiza katikati ya mkoa, na kugawa mkoa kutoka kaskazini hadi kusini.

### 1.5.4 Mfuko wa mtiririko wa maji:

Maumbile ya mkoa wa Dodoma yameruhusu kuwepo kwa mtiririko wa maji unaoanzia kaskazini na kuelekea kusini. Mtiririko huu wa maji hatimaye hupinda kuelekea mashariki ya mkoa hadi bahari ya Hindi.

Mto Kisogo-Ruaha, ambao upo kwenye mpaka wa mikoa ya Iringa na Dodoma, ni mto pekee usiokauka. Mito mingine ni mto Kinyasungwe ambao unaungana na mto Wami wa Dodoma, na mto Bubu ambao chanzo chake ni safu za milima iliyopo kaskazini mwa mkoa ambao humwaga maji yake katika mbuga za Bahi. Kwa mujibu wa utafiti uliyofanywa na wataalam, na hususan katika maeneo ya Farkwa, mto Bubu una uwezo wa kuzalisha umeme pamoja na kumwagilia eneo kubwa la mashamba.

Maeneo mengine ya mkoa yaliyosalia hayana maumbile yanayowezesha shughuli za umwagiliaji, isipokuwa eneo dogo lililopo kaskazini linalokusanya maji ya mvua na kuyamwaga katika ziwa Manyara kupitia maeneo ya Tarangire.

### 1.5.5 Hali ya Mimea:

Mimea iliyopo karibu maeneo yote ya mkoa wa Dodoma ni vichaka vya aina mbali mbali. Hali hiyo ipo kila mahali ambapo shughuli za uharibifu wa uwoto wa asilia umefanyika. Katika maeneo ya mabondeni na maeneo ambayo hupata mvua za kutosha nyasi pamoja na vichaka na miti hushamiri ipasavyo. Hata hivyo, katika maeneo ambayo uwoto wa asilia umeathirika zaidi na shughuli za kilimo cha kuhama hama na ukataji hovyo wa misitu, wakati wa masika nyasi na vichaka hujirudia. Katika safu za vilima, miteremko pamoja na maeneo yaliyotengwa kuwa ni hifadhi ya misitu ya umma miti mingi iliyoshonana imewezesha kuwepo vyanzo vya maji madhubuti na imara.

### 1.5.6 Kanda za Kilimo na Uchumi:

Sehemu kubwa ya mkoa wa Dodoma ni kame na tambarare kiasi kwamba ni vigumu kutambua kwa haraka mipaka ya kanda zake za kilimo. Hata hivyo, ikizingatiwa kuwa mazingira ya mkoa yanazo tofauti za hali ya hewa na kiasi cha mvua, mkoa unaweza kugawanywa katika kanda kuu tatu za kilimo na uchumi. Muhtasari wa kanda hizo tatu ni kama ilivyoonyeshwa katika jedwali na. XII.

**JEDWALI XII: KANDA ZA KILIMO NA UCHUMI MKOA WA DODOMA**

| Kanda | Kiasi cha Mvua | Mazingira na hali ya Udongo |
|---|---|---|
| I | Milimita 30-50 | - Eneo hili ni pamoja na eneo la uwanda wa kaskazini mashariki mwa Kondoa, kusini mwa wilaya ya Dodoma vijijini, kusini - magharibi mwa wilaya ya Mpwapwa. Maeneo yote haya yametawaliwa na uwanda wa chini ambao muda mwingi ni mkame, na pia yana idadi ndogo ya watu.<br><br>- Hali ya amvua katika maeneo haya ni ndogo na haaitabiriki. Udongo wake ni mwekundu na wa mfinyanzi na mchanga. Katika sehemu nyingi za ukanda huu, mbung'o hupatikana. |
| II | Milimita 500-700 | - Kanda hii hujumuisha eneo la katikati ya kusini mwa wilaya ya Kondoa, kaskazini mwa wilaya ya Dodoma, na eneo la Bahi. Pia ni pamoja na eneo la katikati ya wilaya ya Dodoma, eneo lote la wilaya ya Kongwa na baadhi ya eneo la Mpwapwa.<br><br>- Maeneo yote yaliyotajwa yanayo udongo mweusi, mwekundu uliochanganyika na mchanga na mfinyanzi. |
| III | Milimita 700-1000 | - Kanda hii hujumuisha eneo lote la katikati ya wilaya ya Mpwapwa hasa nyanda za juu za wilaya, kuelekea magharibi, pia nyanda za juu za eneo la Bereko wilayani Kondoa.<br><br>- Maeneo yote haya yana udongo mweusi uliochanganyika na mwekundu na mchanga, pamoja na mfinyanzi. Mabonde yaliyopo katika ukanda huu yana udongo mweusi na mfinyanzi. |

Chanzo: Takwimu zilizokusanywa na Tume ya Mipango kutokana na taarifa ya BRALUP.

Katika mwaka wa 1971, taasisi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inayoshughulikia na tathimini ya mpango wa matumizi bora ya ardhi (BRALUP) ilifanikiwa kuainisha na kutenga kanda za mikoa ya Singida na Dodoma katika wilaya zote.

Ufuatao ni muhtasari wa taarifa ya BRALUP kuhusiana na utengaji wa kanda za kilimo na kiuchumi za wilaya zilizomo mkoani Dodoma.

**Jedwali XIII: KANDA ZA KILIMO NA UCHUMI MKOA WA DODOMA KIWILAYA**

| Kanda | Mazingira ya Kanda | Kiasi cha Mvua | Hali ya Udongo | Mazao yanayolimwa |
|---|---|---|---|---|
| (a) Wilaya ya Kondoa | | | | |
| 1 | - Uwanda wa Wamasai, mkame na wenye miinuko na miteremko midogo. Umejaa mbung'o | Chini ya milimita 500 | - | - Mazo machache ya chakula<br>- Hakuna zao la biashara |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2. | - Mazingira makavu, ipo miteremko na miinuko midogo, vipo vilima hapa na pale, mabwawa na wapo mbung'o. Ardhi ina rutuba kidogo | 500-600 | Mweusi na mwekundu kwa upande wa kaskazini, na mwekundu na kichanga kwa upande wa kusini na mfinyanzi katika maeneo yaliyo mabondeni | - Wakulima wadogo hulima mahindi, ulezi, mtama, alizeti, mbegu za mafuta na muhogo. Ziada ya mazao haya huuzwa kama mazao ya biashara |
| 3. | - Ukanda wa juu wa Bereko, una mvua nyingi kuliko eneo lolote wilayani Kondoa. Eneo lenye vilima na milima, zaidi ya mita 1,800 juu ya usawa wa bahari. | 650-800 | - Mweusi mzito umechanganyika na udongo mwekundu na wa kichanga, udongo mweusi na la mfinyanzi maeneo yaliyopo mabondeni | - Mahindi, uwele, mtama, ulezi, maharage, alizeti, mbegu za mafuta. Kwa upande wa kaskazini ndizi na matunda hulimwa. |
| 4. | - Nyanda za juu za katikati, milima mingi na imejigawa tokea kaskazini mashariki kwa mito mingi. Maeneo ya kilimo yameathirika na mmomonyoko wa udongo | 650 | Udongo mwekundu, kichanga | - Mahindi, Ulenzi, mtama, uwele, maharage, viazi vitamu, vitunguu, nyanya, viazi mviringo, ndizi hasa katika maeneo yaliyoinuka. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5. | - Uwanda wa chini wa magharibi; miteremko na miinuko, vilima vya hapa na pale hasa katikati na mashariki mwa wilaya. Mbung'o hasa karibu na hifadhi ya misitu ya Songa shughuli kubwa ni ufugaji kuliko uzalishaji mazao | 500 magharibi hadi 700 mashariki | Hutofautiana | - Eneo kubwa halitumiki kwa kilimo. Uzalishaji mdogo wa mahindi, mtama, muhogo kwa ajili ya chakula tu. |
| (b) Wilaya ya Dodoma | | | | |
| 6. | - Miinuko na miteremko, baadhi ya vilima, mvua nyingi na ya kuaminika shughuli za kilimo zinafanyika vizuri | 550-650 | - Rangi ya kijivu na wekundu na sehemu nyingine udongo mweusi na mwekundu, na kichanga changa | - Mahindi muhogo, mtama, uwele. Karanga na Zabibu hulimwa pia. |
| 7. | Eneo la Bahi, ukanda wa chini unaomwagwa maji katika mbunga za Bahi | 550-650 | Udongo mwekundu wenye kichanga changa | - Zao muhimu ni mpunga. Upanuzi wa kilimo hiki unawezekana. Pia, mahindi mtama, uwele, karanga, vitunguu, nyanya na nyonyo pia hulimwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8. | Ukanda wa chini wenye miinuko na miteremko, milima upande wa kusini. Ukanda wenye wakazi wengi kwa sababu ya mji wa Dodoma, mvua ndogo na haziaminiki | 500-650 | Udongo mwekundu na mweusi wenye mfinyanzi | - Zao kuu ni mtama, uwele, mahindi hasa kaskazini ambako ipo mvua nyingi. Nyonyo, karanga. nyanya, vitunguu, zabibu, zao ambalo lina sana |
| 9. | - Eneo kame sana, miinuko na miteremko, idadi ndogo ya wakazi. Mvua haiaminiki, eneo hutumika kwa kuchungia mifugo isipokuwa sehemu ya magharibi yenye mbung'o. | 400-500 | Udongo mwekundu na wenye kichanga changa na udongo wa mfinyanzi katika mabonde | - Eneo dogo tu hutumika kwa kilimo |
| 10 | - eneo kavu, ukanda wa chini, lenye vilima kaskazini, sehemu kubwa ya eneo linamilikiwa na shamba la mifugo la Kongwa. | 500-650 | Udongo mweusi na kijivu pamoja na kichanga changa | - Mahindi, karanga, nyonyo, na alizeti |
| (c) Wilaya ya Mpwapwa | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11 | - Nyanda za juu zenye vilima na kanda tatu zilizoinuka. Idadi ya watu ni kidogo, shughuli za kilimo ni ndogo kutokana na mazingira yake. | 700-900 | - Kina cha udongo ni kifupi, mawe yapo, udongo mweusi na kijivu, mabondeni kuna udongo jekundu sana mwekundu sana. | - Mahindi, maharage, viazi mviringo. Baadhi ya mazao hulimwa kwa kutumia njia za jadi za umwagiliaji |
| 12 | - Eneo lenye milima milima lenye miteremko kuelekea magharibi. Idadi ndogo ya watu kasoro eneo la mji wa Mpwapwa | 650-800 | - Udongo mweusi na mwekundu wenye kichanga changa. Kina kidogo cha udongo kwenye miteremko | - Mahindi hulimwa kwa ajili ya chakula na ziada huuzwa, karanga, uwele, mpunga na ndizi hulimwa katika maeneo yenye mvua za kutosha |
| 13 | - Eneo lenye vilima limegawanyika kutokana na mito. Eneo kavu kuliko yote wilayani, malisho ya mifugo ni kidogo, lenye idadi ndogo ya watu | 450-630 | - Udongo mwekundu wenye mchanganyiko wa kichanga changa. Kina kidogo cha udongo kwenye miteremko na kina kirefu kwenye mabonde | - Mahindi, uwele na mtama hulimwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 14 | - Uwanda wa juu unaozunguka bonde la Ruaha Mwega. Eneo hili ni kame, shughuli ndogo za kilimo, ufugaji mdogo. Idadi ndogo ya watu | 550-650 | - | - Mahindi, maharage, vitunguu, mboga za majani hulimwa |

Chanzo: BRALUP - Chuo Kukuu cha Dar es Salaam

# SURA YA PILI

## 2.0 Uchumi wa Mkoa

## 2.1 Utangulizi:

Mkoa wa Dodoma ni miongoni mwa mikoa yenye uchumi duni nchini. Kwa mfano mwaka 1996 wastani wa pato la mtu katika mkoa wa Dodoma lilikuwa Tshs.278.00, kiwango ambacho ni kikubwa kidogo tofauti na mikoa ya Singida (Tshs 227.00), Ruvuma (Tshs.262.00) na Kigoma (Tshs.260.00). Ukiondoa mkoa wa Ruvuma, mikoa mitatu iliyosalia yaani Dodoma, Singida na Kigoma ni miongoni mwa mikoa mitano ya mwisho yenye uchumi duni kuliko yote Tanzania Bara kwa kuangalia wastani wa

pato la mtu kwa mwaka na mchango wa mkoa katika pato la taifa.

Uchumi wa mkoa wa Dodoma unategemea zaidi shughuli za kilimo na ufugaji, ambazo hufanywa na wakulima na wafugaji wadogo sehemu kubwa kwa ajili ya mahitaji yao tu. Uzalishaji wa mazao kwa eneo ni mdogo sana kutokana na mvua ndogo na isiyoaminika, upotevu wa maji mengi kwa njia ya mvuke na uwezo mdogo wa ardhi kuhifadhi maji ya mvua.

Hali hii imechangia kwa kiasi kikubwa pamoja na matumizi mabaya ya ardhi hususan ufugaji wa mifugo mingi ambayo inasababisha mmomonyoko wa ardhi, uzalishaji mdogo wa shughuli za kiuchumi

.

Mazao makuu ya chakula yanayolimwa Dodoma ni pamoja na mtama, uwele na mahindi. Mazao ya biashara ni pamoja na mahindi, karanga, alizeti, nyonyo, ufuta na aina za mikunde. Katika miaka ya 1970 na mwanzoni mwa mwaka 1980 zao la zabibu na zao la mpunga yalitokea kuwa ni mazao muhimu ya biashara, japokuwa mchango wake katika pato la taifa ulikuwa wa muda mfupi tu. Hata hivyo, uongozi wa mkoa kwa hivi sasa umekwisha andaa mpango wa kufufua tena kilimo cha zao la zabibu ikiwa ni pamoja na kulitafutia masoko yenye uhakika.

Mifugo ni njia kuu ya pili ya kiuchumi inayochangia pato la mkoa. Aidha Dodoma ni mkoa wa nne wenye idadi kubwa ya mifugo mingi Tanzania Bara. Mifugo hiyo ni pamoja na ng'ombe, mbuzi

na kondoo. Ufugaji wa nguruwe na kuku wa kisasa unafanyika kwa kiwango kidogo katika maeneo ya mijini na vituo vikubwa vya kibiashara.

Sekta ya maliasili, ambayo inajumuisha misitu, wanyapori, nyuki, uvuvi na madini, ni shughuli zingine za kiuchumi ambazo hutoa ajira kwa baadhi ya watu wa mkoa wa Dodoma. Mazao kama, mbao, magogo, nguzo, wanyamapori, asali, nta, samaki, chumvi na dhahabu yanavunwa kwa njia ya asili. Kutokana na zana na vifaa duni sekta ya maliasili inachangia kiasi kidogo sana katika pato la mkoa.

Hali kadhalika, sekta ya viwanda ni duni sana mkoani Dodoma. Kwa hivi sasa vipo viwanda vidogo vidogo hususan katika maeneo ya mijini.

## 2.2 Pato la Mkoa na Wastani wa Pato kwa Mtu

Katika mwaka 1994 wastani wa pato la mtu kwa mwaka lilikuwa Tshs.39,604. Ikiliganishwa na mikoa mingine mkoa wa Dodoma umeendelea kuwa mojawapo ya mikoa yenye uchumi duni. Kwa mujibu wa takwimu za kitaifa zilizopo, wastani wa mchango wa mkoa wa Dodoma kwa mwaka katika pato la taifa kwa bei za sasa na kwa miaka 15 iliyopita umeendelea kuwa asilimia 3.07. Jedwali na.XIV linaonyesha kiwango ambacho kila mkoa umechangia katika pato la taifa na nafasi ya kila mkoa kwa kipindi kilichoonyeshwa.


**JEDWALI XIV: MCHANGO WA KILA MKOA KWENYE PATO LA TAIFA 1980 - 1994**

| Mkoa | Wastani wa mchango kwa mwaka | Nafasi ya Mkoa katika michango |
|---|---|---|
| Arusha | 7.8 | 2 |
| Pwani | 1.33 | 20 |
| Dar es Salaam | 20.33 | 1 |
| **Dodoma** | **3.07** | **16** |
| Iringa | 5.53 | 6 |
| Kagera | 4.6 | 9 |
| Kigoma | 2.53 | 18 |
| Kilimanjaro | 3.67 | 10 |
| Lindi | 2.0 | 19 |
| Mara | 3.47 | 11 |
| Mbeya | 6.0 | 4 |
| Morogoro | 4.67 | 8 |
| Mtwara | 3.27 | 14 |
| Mwanza | 7.67 | 3 |
| Rukwa | 3.13 | 15 |
| Ruvuma | 3.33 | 13 |
| Shinyanga | 5.8 | 5 |
| Singida | 2.87 | 17 |
| Tabora | 3.4 | 12 |
| Tanga | 5.53 | 7 |
| Jumla | 100.0 | |

Chanzo: Tume ya Mipango kuzingatia ripoti ya Hesabu za Taifa za Mapato mwaka 1976 - 1994 toleo la II Agosti 1995

Wastani wa pato la mtu kwa mwaka mkoani Dodoma kwa bei za sasa, katika kipindi cha 1980-1994 ilikuwa Tshs.11,525/=, kiwango ambacho ni sawa na nusu ya wastani wa taifa. Jedwali na. XIV linabaini kuwa kati ya mwaka 1980 hadi 1994, wastani wa pato la mtu kwa mwaka kwa bei za sasa, kwa mkoa wa Dodoma, ilikuwa ndogo ikilinganishwa na mikoa ya jirani kama vile Iringa, Arusha, Singida na Dodoma. Katika mwaka 1994 pekee Dodoma ilikuwa na wastani wa pato la mtu la Tshs.39,604/=, Arusha TShs.91,024/=, Iringa Tshs.64,502/=, Singida Tshs.55,644/= na Morogoro Tshs.59,370/=.

**Kielelezo.8: Mapato yatokanayo na mazao ya chakula mkoani Dodoma kwa mwaka 1994/95**




**JEDWALI XV: MTIRIRIKO WA WASTANI WA PATO LA MTU KWA MWAKA - MKOA WA DODOMA NA MIKOA YA JIRANI**

| Mwaka | Mkoa wa Dodoma | Mkoa wa Arusha | Mkoa wa Iringa | Mkoa wa Singida | Mkoa wa Morogoro |
|---|---|---|---|---|---|
| 1980 | 1048 | 2709 | 1801 | 1362 | 1977 |
| 1981 | 1310 | 3216 | 2325 | 1700 | 2485 |
| 1982 | 1561 | 3820 | 2868 | 2138 | 3016 |
| 1983 | 1509 | 3986 | 3131 | 2261 | 2937 |
| 1984 | 1911 | 4497 | 3975 | 2842 | 3065 |
| 1985 | 2511 | 5736 | 5204 | 3619 | 3946 |
| 1986 | 3307 | 7265 | 6789 | 5195 | 4493 |
| 1987 | 4110 | 10182 | 9390 | 7038 | 5737 |
| 1988 | 7380 | 17497 | 17010 | 12809 | 9550 |
| 1989 | 11556 | 27053 | 26339 | 19871 | 14476 |
| 1990 | 17779 | 41131 | 28144 | 24750 | 27054 |
| 1991 | 21914 | 50997 | 34812 | 30703 | 32974 |
| 1992 | 26007 | 59928 | 42028 | 36484 | 39189 |
| 1993 | 31380 | 72009 | 51659 | 44332 | 47034 |
| 1994 | 39604 | 91024 | 64502 | 55644 | 59370 |

Chanzo: Hesabu za Taifa za Tanzania miaka 1976 - 1994 Taasisi ya Takwimu, Toleo la Kumi na Moja Agosti 1995


Kielelezo 9: Mpato yatokanayo na mazao ya chakula Mkoani Dodoma mwaka 1990/91:




Kama ilivyoelezwa hapo awali katika kitabu hiki, kukosekana kwa mazao makuu ya kibiashara kama vile chai, kahawa, na pamba kumesababisha mapato ya mkoa kutegemea zaidi ziada ya mazao ya chakula. Wastani wa kati ya asilimia 60 hadi 70 ya mapato ya mwaka ya mkoa hutokana na ziada ya mazao ya chakula, kama vile mahindi, mtama, karanga, maharage na uwele. Hata hivyo, hivi karibuni zao la mpunga limeonyesha matumaini mazuri hasa kipindi chenye mvua ya kutosha.

Uchumi wa mkoa kwa ujumla umeendelea kukuwa (kwa tarakimu halisi) tokea mwaka 1984 ingawaje thamani ya wastani wa pato la mtu kwa mwaka imeendelea kushuka kama jedwali na. XV linavyoonyesha. Pato la mkoa liliongezeka kutoka Tshs.1,048 milioni mwaka 1980 hadi kufikia Tshs.57,656 mwaka 1994.

**Kielelezo10: Mapato yatokanayo na mazao ya chakula mwaka 1985/86:**




**JEDWALI XVI: PATO LA MKOA WA DODOMA KWA BEI ZA SASA NA ASILIMIA YA MCHANGO WAKE KWA PATO LA TAIFA (1980 - 1994)**

| Mwaka | Pato la Mkoa kwa bei za sasa (Mil.) | Badiliko kiasilimia | Asilimia ya mchango wa mkoa kitaifa | Kiwango cha thamani ya sarafu yetu kwa Dola | Dola ya Kimarekani | Wastani wa Pato la mtu kwa mwaka | Asilimia ya badiliko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1980 | 1068 | - | 3 | 8.22 | 127 | 1048 | - |
| 1981 | 1367 | 28 | 3 | 8.35 | 157 | 1310 | 25 |
| 1992 | 1669 | 22.9 | 3 | 9.52 | 164 | 1561 | 19.16 |
| 1983 | 1652 | -1.01 | 3 | 12.44 | 121 | 1509 | -3.33 |
| 1984 | 2142 | 29.66 | 3 | 18.16 | 105 | 1911 | 26.64 |
| 1985 | 2881 | 34.50 | 3 | 16.50 | 152 | 2511 | 31.39 |
| 1986 | 3886 | 34.88 | 3 | 51.70 | 64 | 3307 | 31.70 |
| 1987 | 4935 | 26.99 | 3 | 83.70 | 49 | 4101 | 24.00 |
| 1988 | 9113 | 84.66 | 3 | 125.00 | 59 | 7380 | 79.95 |
| 1989 | 14677 | 61.05 | 3 | 192.00 | 60 | 11556 | 56.58 |
| 1990 | 23220 | 58.20 | 3 | 197.00 | 90 | 17779 | 53.85 |
| 1991 | 29434 | 26.76 | 4 | 234.00 | 94 | 21914 | 23.25 |
| 1992 | 35923 | 22.04 | 3 | 335.00 | 78 | 26007 | 18.67 |
| 1993 | 44575 | 24.08 | 3 | 480.00 | 65 | 31380 | 20.65 |
| 1994 | 57856 | 29.79 | 3.07 | 553.00 | 72 | 39604 | 26.20 |
| Wastani | 15626.53 | | | | 97.13 | | |

Chanzo: Taasisi ya Takwimu

Jedwali na. XVII linaonyesha mapato yaliyopatikana katika misimu ya kilimo ya mwaka 1995/96, 1990/91 na 1994/95 kutokana na mauzo ya mazao ya chakula. Maeneo yanayozalisha mazao ya chakula na kupata ziada ni tarafa za Beseko wilayani Kondoa na Zoisa wilayani Kongwa. Maeneo ya Kibakwe na Rudi wilayani Mpwapwa pia huzalisha ziada ya mazao ya chakula.

**JEDWALI XVII: MTIRIRIKO WA MAPATO YATOKANAYO NA MAUZO YA MAZAO YA CHAKULA MKOANI DODOMA (TSHS.`000)**

| ZAO | 1985/86 | | | 1990/91 | | | 1994/95 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uzito (Tani) | Wastani Tani/Ha | Thamani (000) | Uzito (Tani) | Wastani Tani/Ha | Thamani (000) | Uzito (Tani) | Wastani Tani/Ha | Thamani (000) |
| Mahindi | 72983 | 1,21 | 383160 | 4900 | 0.72 | 637104 | 163091 | 1.89 | 4892730 |
| Mtama | 75529 | 0.52 | 302166 | 61525 | 0.95 | 492200 | 267881 | 1.50 | 8036430 |
| Uwele | 41446 | 0.34 | 165784 | 66255 | 0.90 | 530040 | 138145 | 1.03 | 4144350 |
| Mpunga | | | | 1306 | 2.0 | 33956 | 2808 | 2.0 | 88171 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dodoma

Ufugaji mkoani Dodoma inachukuwa nafasi ya pili katika shughuli za kiuchumi. Mazao ya mifugo yanakisiwa kuchangia kati ya asilimia 30 hadi 40 ya pato la mkoa kwa mwaka

Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti uliofanywa mwaka 1975 na mtafiti Dr. Trevor Chandler kutoka Canada, mkoa wa Dodoma unayo raslimali kubwa ya kuendeleza shughuli za ufugaji wa nyuki kwani

mbalimbali za mimea inayofaa kwa ajili ya kuendeleza ufugaji wa nyuki imetapakaa mkoani pote. Katika ushauri wake Dr. Chandler anasisitiza kuwa ili kuendeleza shughuli za ufugaji nyuki mkoani Dodoma, upo umuhimu wa kuwahamasisha wawekezaji na wananchi kuhusu matumizi ya mizinga ya nyuki ya kisasa na pia kuainisha na kuyatambua masoko ya ndani na nje ya nchi, ya mazao mbali mbali ya nyuki.

Katika kipindi cha ukame, mzinga mmoja wa kisasa unaweza kutoa wastani wa kilo 20 za asali na kilo moja ya nta mkoani Dodoma. Hata hivyo, katika mazingira mazuri zaidi uzalishaji wa asali na nta unaweza ukaongezeka maradufu. Hata hivyo,mkoa bado unazalisha asali na nta kwa kiwango kinachoridhisha kwa kutumia vifaa vya jadi na teknologia duni. Kwa mfano kati ya mwaka 1992 na 1994 mauzo ya mazao ya nyuki yaliupatia mkoa jumla ya Tshs. 399,400,000.00 kama jedwali na. XVIII linavyoonyesha.

**JEDWALI XVIII: MAPATO YALIYOTOKANA NA MAUZO YA MAZAO YA NYUKI MKOANI DODOMA 1992-1994**

| Zao | 1992 | | 1993 | | 1994 | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uzito (Tani) | Thamani (000) | Uzito (Tani) | Thamani (000) | Uzito (Tani) | Thamani (000) | Uzito (Tani) | Thamani (000) |
| Asali | 814 | 92880 | 158.53 | 149589 | 350.16 | 84173 | 1323.5 | 326651 |
| Nta | 55.7 | 38118 | 1982 | 17711 | 147.12 | 16919 | 90.23 | 72748 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa - Dodoma

Katika shughuli za uvuvi, kati ya mwaka 1992 hadi 1994 mkoa uliweza kujipatia jumla ya Tshs. 1,412.744/= kama jedwali XIX linavyoonyesha.

**JEDWALI XIX: MAPATO YALIYOTOKANA NA MAUZO YA SAMAKI KATI YA 1992-1994 MKOANI DODOMA**

| Mwaka | Uzito (Tani) | Thamani Tshs. "000" |
|---|---|---|
| 1992 | 5306.3 | 558.760.6 |
| 1993 | 4023.6 | 383.699.55 |
| 1994 | 4664.9 | 470,914.05 |
| Jumla | 13994.8 | 1,412,744.2 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dodoma

Pamoja na shughuli za kiuchumi zilizotajwa hapo juu, wananchi hujishughulisha pia na uuzaji wa mazao ya misitu kama vile mkaa, kuni na mbao. Tokea mwaka 1973 wakati mji wa Dodoma ulipotangazwa kuwa makao makuu ya serikali biashara za mazao yatokanayo na misitu zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku.

## 2.3 Vigezo vya Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi

### 2.3.1 Upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii:

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Taasisi ya Chakula na Lishe ya Tanznia mwaka 1973 ilidhihirika kwamba kwa wastani wanalazimika kutembea umbali kati ya kilomita 2 hadi 10 ili kufikia huduma za kimsingi za kijamii mkoani Dodoma kama jedwali na. XX linavyoonyesha.

**Jedwali XX:** **UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA MSINGI ZA KIJAMII**

| Huduma za Kimsingi | UMBALI KATIKA KILOMITA | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| Maji | 158 | 75.2 | 41 | 15.5 | 6 | 2.0 | 5 | 2.4 | - | - |
| Nishati | 37 | 17.6 | 100 | 41.6 | 62 | 29.6 | 5 | 2.4 | 1 | 0.5 |
| Soko | 60 | 28.6 | 3 | 1.4 | - | - | - | - | 1 | 0.5 |
| Duka | 205 | 96.7 | 4 | 2.0 | 1 | 0.5 | - | - | - | - |
| *Zahanati | 168 | 80.0 | 8 | 3.9 | 6 | 2.9 | - | - | 3 | 1.5 |
| Hospitali | 6 | 2.9 | 11 | 5.2 | 18 | 8.6 | - | - | 174 | 82. |
| Shule | 117 | 84.3 | 31 | 5.3 | 2 | 1.0 | - | - | - | 8 |
| Shamba | 79 | 37.8 | 93 | 44.5 | 28 | 13.4 | 4 | - | - | -.- |
| Wakunga wa Jadi | 3 | | | | | | | | | |
| Mashine za kusaga | 198 | 94.3 | 5 | 2.4 | 1 | 0.5 | - | - | - | |
| Ushirika | 167 | 79.5 | 8 | 3.9 | 1 | 0.5 | - | - | - | - |
| Mji | 103 | 49.0 | 1 | 0.5 | - | - | - | - | - | - |
| | 20 | 9.5 | - | - | 2 | 1.0 | | - | 188 | - |
| | | | | | | | | | | 89.4 |
| | | 54.6 | | 10.85 | 5.075 | | | - | 0.4 | 2.9 |

Chanzo: Ripoti ya uchambuzi wa hali ya Lishe Mkoani Dodoma - 1993

Taarifa hiyo imeendelea kubaini kwamba kutokana na ukweli kwamba kazi nyingi vijijini hufanywa na akina mama, wanawake vijijini hulazimika kutembea umbali mrefu kwa mfano kwenda kutafuta maji, kuni, kuwapeleka watoto katika huduma za afya kama vile vituo vya afya na zahanati, kwenda mashambani, kwenda kusaga nafaka, madukani, sokoni, vyama vya ushirika, kwenda mijini na sehemu zingine zenye huduma za lazima.

Hata hivyo hali huwa ngumu na mbaya zaidi kwa wanawake wajawazito na wale wanaonyonyesha watoto wadogo wanapolazimika kutembea umbali mrefu kuzifuata huduma hizo.

### 2.3.2 Hali ya Kijamii na Kiuchumi

Kama ilivyoelezwa awali, Dodoma ni mojawapo ya mikoa yenye uchumi duni nchini. Kwa kutumia kigezo cha wastani wa pato la mtu kwa mwaka ya mwaka 1994 Dodoma ni moja kati ya mikoa mitano yenye uchumi duni kuliko yote nchini. Umaskini umekithiri na upo ushahidi wazi kuwa huduma za kimsingi zimeendelea kushuka kadri miaka inavyozidi kwenda, kutokana na viwango vidogo vya bajeti ya serikali kwa huduma hizo. Viwango vya vifo vya watoto wachanga na watoto walio chini ya miaka mitano, vifo vya akina mama wajawazito, na viwango vya ujumla vya vifo vya watu ni vikubwa zaidi vikilinganishwa na wastani wa viwango vya kitaifa.

Ni dhahiri kwamba huduma za kiafya zimeathiriwa sana na viwango vidogo vya bajeti ya serikali vitolewavyo na kwa sababu hiyo vifaa muhimu pamoja na madawa katika hospitali, vituo vya afya na katika zahanati havitosholezi kulingana na mahitaji halisi. Kutokana na hali hiyo, wastani wa umbali kutoka kwenye kaya hadi kituo cha afya cha karibu ni kati ya kilomita 5 hadi 10.

Kwa upande mwingine kiwango cha uandikishaji watoto wa shule za msingi ni sawa na asilimia 55.5 na pia kiwango cha wanafunzi wa darasa la saba wanaochaguliwa kwenda kidatu cha kwanza katika shule za sekondari za umma ni sawa na asilimia 3.8 na wastani wa miaka ya kuishi kwa mkoa wa Dodoma ni miaka 46,

ambapo ni vidogo vikilinganishwa na viwango vya kitaifa. Viwango vya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika vimeongezeka kutoka asilimia 21 mwaka 1980 hadi kufikia asilimia 37 mwaka 1994. Hata hivyo upo uwezekano kuwa idadi ya wasiojua kusoma ni kubwa kuliko asilimia 37 ilivyo.

Katika mwaka 1994 mlinganisho wa idadi ya watu waliokuwa karibu na huduma ya maji ilifikia asilimia 55.5 ya watu wote. Kiwango hiki ni kikubwa kikilinganishwa na wastani wa kitaifa ingawaje ipo miradi mingi ya maji ambayo haifanyi kazi. Kwa sababu hizo, upungufu wa vyanzo vya maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo ni kikwazo kikubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi mkoani Dodoma.

Sehemu kubwa ya watu waishio vijijini huishi katika nyumba ambazo ni duni sana. Hata hivyo inakadiriwa kuwa wastani wa asilimia 27 tu ya watu wa mkoa wa Dodoma huishi katika nyumba bora na za kisasa. Sehemu kubwa ya nyumba hizi zijulikanazo kama “matembe” zimetengenezwa kwa vifaa duni ambapo juhudi kubwa inahitajika ili kuziboresha kufikia hali ya kuridhisha kiafya na kimakazi.

**JEDWALI XXI: BAADHI YA VIGEZO VYA KIJAMII NA KIUCHUMI VINAVYOWEZA KULINGANISHWA NA MIKOA MINGINE**

| Kigezo | Dodoma | Mbeya | Iringa | Arusha | Mwanza | Wastani Kitaifa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wastani wa pato kwa mwaka Tshs.(1994) | 39,604 | 48,737 | 64,502 | 91.024 | 48,508 | 62,138 |
| Wastani wa mtu kuishi | 46 | 55 | 48 | 57 | 52 | 50 |
| Idadi ya watu kwa kilomita moja ya mraba (1988) | 30 | 25 | 21 | 16 | 98 | 26 |
| Asilimia ya wanaojua kusoma na kuandika | 63 | 76 | 56 | 72 | 71.5 | 76 |
| Asilimia ya wanafunzi walioandikishwa shuleni (1993) | 59.8 | 79.6 | 80.6 | 75.6 | 67.3 | 74.2 |
| Asilimia ya watu wapatao maji safi (1994) | 55.5 | 48.7 | 48.2 | 37.4 | 56.4 | 50.5 |
| Idadi ya shule za sekondari (1994) | 22 | 27 | 44 | 54 | 39 | 23 |
| Asilimia ya watu walio kilomita 5 hadi 10 karibu na huduma ya afya | 46.4 | 38 | 36.5 | 41.2 | 38 | 42.5 |
| Viwango vya vifo vya watoto wachanga (1995) | 131 | 116 | 111 | 82 | 90 | 92 |
| Wastani wa watu wanaoishi katika nyumba bora (%) | 27 | 44 | 36 | 32 | 31.5 | n.a. |
| Uwiano wa watu/idadi ya hospitali (1995) | 278,480 | 134,182 | 93,201 | 96,571 | 170,727 | 100,000 |
| Uwiano wa watu/vituo vya afya (1995) | 85,782 | 86,824 | 75,563 | 122,909 | 72,231 | 50,000 |
| Uwiano wa watu/zahanati | 7675 | 7,936 | 8,574 | 7,511 | 7,891 | 10,000 |
| Uwiano wa watu/madaktari | 32,738 | 28,142 | 56,416 | 30,044 | 75,120 | 24,930 |

Chanzo: Tume ya Mipango: Ripoti mbali mbali

### 2.3.3 Nafasi za Kazi:

Mkoani Dodoma idadi kubwa ya watu hawana ajira. Uchambuzi wa takwimu za sensa ya mwaka 1967 unaonyesha kuwa wastani wa asilimia 1.2 ya watu 433,704 wenye uwezo wa kufanya kazi walikuwa wameajiriwa katika ajira rasmi. Pia, uchambuzi wa takwimu za sensa ya mwaka 1988 unaonyesha kuwa ni asilimia 5.9 ya watu 830,201 wenye uwezo wa kufanya kazi walikuwa wana ajira rasmi. Hata hivyo nyingi kati ya ajira hizo zilikuwa katika miji mikuu ya wilaya. Kwa upande wa maeneo ya vijijini, wastani wa asilimia 62 ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi walijihusisha na shughuli za kilimo. Taarifa ya matokeo ya sensa ya mwaka 1988 inaonyesha kwamba asilimia 26.9 ya nguvu kazi iliyokuwepo haikuwa na kazi. Hata hivyo yapo maoni kwamba asilimia 26.9 ni ndogo ikilinganishwa na hali halisi ilivyo huko vijijini, kwani nguvu-kazi hiyo inatumika kikamilifu wakati wa msimu mmoja tu wa kilimo takriban miezi 4 hadi 5. Baada ya msimu wa kilimo nguvu-kazi hiyo huwa hawana shughuli ya muhimu ya uzalishaji.

Pamoja na hali hiyo, wakati wa msimu wa kilimo nguvu-kazi iliyopo haitumiki kwa ukamilifu. Ipo mifano hai ambapo kaya moja yenye watu wazima 10 hulima hekta moja au mbili tu. Sekta ya viwanda bado ni changa sana mkoani, na kwa hali hiyo inaajiri wafanyakazi wachache sana. Jedwali XXII linaonyesha mchanganuo wa ajira ya watu wenye umri zaidi ya miaka 10 na kwa jinsia.

**JEDWALI XXII: IDADI YA WAAJIRIWA WENYE UMRI ZAIDI YA MIAKA 10 KIKAZI, KIJINSIA NA KIWILAYA - MKOANI DODOMA MWAKA 1988**

| Wilaya/Jinsia | | Shughuli za Kiuchumi | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Waajiriwa | Wakulima | Wakulima mchanganyiko | Wasio na ajira | Hawajulikani | Jumla | Asilimia ya wasio na ajira |
| WANAUME: | | | | | | | |
| Kondoa | 4,744 | 64,900 | 6,702 | 31,732 | 759 | 108,837 | 29.2 |
| Mpwapwa | 5,300 | 67,570 | 6,356 | 26,397 | 939 | 106,562 | 24.8 |
| Dodoma V | 4,371 | 69,038 | 9,225 | 25,482 | 435 | 108,551 | 23.5 |
| Dodoma M | 20,319 | 27,476 | 1,528 | 17,616 | 297 | 67,236 | 26.2 |
| WANAWAKE: | | | | | | | |
| Kondoa | 2,122 | 72,471 | 5,826 | 36,745 | 541 | 117,705 | 31.2 |
| Mpwapwa | 2,190 | 82,308 | 5,059 | 28,118 | 881 | 118,556 | 23.7 |
| Dodoma V | 1,616 | 93,087 | 4,749 | 29,894 | 524 | 129,870 | 23.0 |
| Dodoma M | 8,731 | 34,939 | 1,540 | 27,439 | 335 | 72,984 | 37.6 |
| JUMLA: | | | | | | | |
| Kondoa | 6,866 | 137,371 | 12,528 | 68,477 | 1,300 | 226,542 | 30.2 |
| Mpwapwa | 7,490 | 149,878 | 11,415 | 54,515 | 1,820 | 225,118 | 24.2 |
| Dodoma V | 5,987 | 162,125 | 13,974 | 55,376 | 959 | 238,421 | 23.2 |
| Dodoma M | 29,050 | 62,415 | 3,068 | 45,055 | 632 | 140,220 | 32.1 |
| Juumla Kuu | 49,393 | 511,789 | 40,985 | 223,423 | 4,711 | 830,301 | 26.9 |

Chanzo: Mchanganuo wa taarifa ya Sensa ya 1988, Tume ya Mipango

## SURA YA TATU

## 3.0 MIUNDOMBINU YA SEKTA YA KIUCHUMI:

### 3.1 Mtandao wa Barabara:

Mkoa wa Dodoma una mawasiliano mazuri ya barabara kati yake na mikoa inayoizunguka. Dodoma imeunganishwa na barabara zifuatazo; Barabara kuu kutoka mashariki - magharibi kuelekea Dar es Salaam kupitia Morogoro; kaskazini kuelekea Arusha, magharibi kuelekea Mwanza kupitia Singida na barabara kutoka kusini kuelekea mikoa ya kusini kupitia Iringa.

Barabara za vijijini hazijapita sehemu zote muhimu za uzalishaji. Hadi kufikia mwaka 1996 mkoa ulikuwa na kilomita 4,236 za aina tofauti za barabara kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali na. XXIII.

**JEDWALI XXIII: MTANDAO WA BARABARA UREFU NA AINA - 1995**

| Aina ya Barabara | Lami (Km) | Kifusi (Km) | Udongo (Km) | Jumla (Km) |
|---|---|---|---|---|
| Kuu | 137 | 419 | - | 556 |
| Za Mkoa | 5 | 188 | 486 | 679 |
| Za Wilaya | 33 | 70 | 1247 | 1350 |
| Za Vijijini | - | - | 1651 | 1651 |
| Jumla | 175 | 677 | 3384 | 4236 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa - Dodoma (Ujenzi)

Mtandao wa barabara kuu mkoani, isipokuwa ile ya Dodoma - Morogoro ambayo ni ya lami, zimeharibika kwa kiasi kikubwa katika miaka ya karibuni, hasa kutokana na idadi kubwa ya magari mazito yanayopita tofauti na uwezo wa barabara, na ukosefu wa matengenezo ya mara kwa mara.

Barabara za mkoa, wilaya na zile za vijijini ziko katika hali mbaya kutokana na utunzaji usio makini. Hali ya barabara za Kondoa zimeathirika zaidi kuliko barabara za wilaya zingine.

Katika miaka ya hivi karibuni Serikali ya Tanzania ikishirikiana na serikali na Uholanzi kwa kupitia shirika lake lisilo la kiserikali (SNV) liliendesha utafiti wa kina wa namna ya kuboresha barabara za wilaya ya Kondoa, hususan zile za vijijini. Mtandao wa barabara kiwilaya kwa mkoa wa Dodoma ni kama ifuatavyo:

**JEDWALI XXIV: MTANDAO WA AINA ZA BARABARA KIWILAYA - 1995**

| Wilaya | Barabara Kuu (Km) | Kimkoa (Km) | Kiwilaya (Km) | Kijiji (Km) | Jumla (Km) |
|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma (M) | 127 | 44 | 353 | - | 524 |
| Dodoma (V) | 191 | 158 | 216 | 558 | 1123 |
| Mpwapwa | 123 | 233 | 110 | 847 | 1313 |
| Kondoa | 115 | 244 | 568 | 349 | 1276 |
| Jumla | 556 | 679 | 1247 | 1754 | 4236 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa - (Ujenzi - Dodoma

Kama ilivyoelezwa awali, mkoa wa Dodoma uko katikati ya nchi na hivyo upo muhimu wa kuwa na barabara nzuri ambazo zinaunganisha mkoa na maeneo mengine yote ya Tanzania Bara. Mpango wa kuimarisha barabara kuu, mkoa, wilaya na zile vijiji utaongeza kasi ya maendeleo ya mkoa pamoja na ukuaji wa makao makuu ya serikali.

Iwapo barabara zinazounganisha makao makuu zitaimarishwa, hii itasaidia kupunguza tatizo la mkoa kuendelea kutegemea njia ya reli na pia kufupisha sana mawasiliano ya barabara inayounganisha Afrika ya Kaskazini na Kusini kupitia Arusha - Dodoma - Iringa.

Aidha kwa mkoa wa Dodoma zifuatazo ni barabara muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya jamii na uchumi wa mkoa na nchi kwa ujumla:

(i) **Barabara Kuu ya Arusha - Dodoma - Iringa (Kilomita 365)**

Barabara hii ni barabara fupi kati ya Kaskazini na Kusini mwa nchi. Barabara hii ya changarawe ina urefu wa kilomita 365 na hupiti katika maeneo ya kilimo, katika wilaya za Babati, Kondoa na Iringa. Kama ilivyoelezwa awali uimarishaji wa barabara hii kuu utaimarisha na kukuza mahusiano makubwa ya kiuchumi kati ya Afrika ya kaskazini na kusini kupitia Tanzania.

(ii) **Barabara Kuu ya Dodoma - Singida - Mwanza (Kilomita 66)**

Barabara hii ni muhimu kwani ni barabara mbadala kati ya mashariki na magharibi ya nchi. Uimarishaji wa barabara hii utapunguza tatizo la kutegemea reli ya kati kama njia kuu ya kusafirishaji mazao ya biashara yanayozalishwa mikoa ya Kagera, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Singida na Dodooma. Pia, itarahisisha usafirishaji wa shehena kwenda na kutoka nchi za jirani za Uganda, Rwanda, Burundi na Zaire. Hata hivyo, ujenzi wa barabara hii hadi kiwango cha lami umeanza kati ya mkoa wa Mwanza na Shinyanga.

(iii) **Barabara ya mkoa kati ya Dodoma - Mpwapwa - Mlali - Pandambili; (Kilomita 99).**

Barabara hii ni muhimu sana katika maendeleo ya mkoa wa Dodoma kwani inapita katika maeneo muhimu sana kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo kama mahindi, maharage, mtama na karanga katika wilayani za Mpwapwa na Kongwa.

### 3.1.2 Matatizo yanayokabili barabara Mkoani:

(i) Mvua za mawe pamoja na kilimo cha kwenye miteremko huacha ardhi wazi na kusababisha mmomonyoko mkubwa wa ardhi.

(ii) Uhaba wa fedha za kutengeneza/kukarabati na kuimarisha barabara kutokana na bajeti finyu ya serikali.

(iii) Ukosefu wa zana na vifaa vya kukarabati na kutengeneza barabara

(iv) Uhaba wa Wahandisi wa barabara

## 3.2 Huduma za Reli:

Njia za mawasiliano ya barabara ndani ya mkoa wa Dodoma ni za kuridhisha na vile vile kuwepo kwa reli ya kati kutoka mashariki kwenda magharibi kunapunguza tatizo la usafiri na usafirishaji. Hata hivyo umaarufu wa reli ya kati kwa uchumi na shughuli za kijamii za Dodoma ulianza kuporomoka mara baada ya barabara ya Dodoma - Dar es Salaam kuwekwa lami. Uwezo wa shirika la reli wa kusafirisha shehena na mizigo umepungua kwa kiwango kikubwa kutokana na usafirishaji kwa njia ya barabara kuwa nzuri.

## 3.3 Huduma za Anga:

Mkoa wa Dodoma unazo huduma chache na duni za anga. Hata hivyo, katika miaka ya 1990 Manispaa ya Dodoma ilikuwa inapata huduma za ndege kila siku. Baadaye, Shirika la Ndege la Tanzania lilibaini kuwa linaingia hasara na ndipo likaamua kusitisha ndege zake kupitia Dodoma. Kwa hivi sasa uwanja wa ndege wa Dodoma ambao uko katikati ya mji unatumika kwa ndege ndogo za watu/makampuni binafsi hususan kampuni ya MAF pamoja na ndege za serikali. Pia, katika mji wa Mpwapwa na hospitali ya

Mvumi vipo viwanja vidogo vya ndege, ambavyo mara nyingi hutumika kwa ajili ya ndege zinazowasafirisha madaktari.

## 3.4 Vifaa vya Mawasiliano

Baadhi ya vifaa vya mawasiliano vilivyopo mkoani Dodoma ni pamoja na njia 2,981 za simu, njia 50 za teleksi, njia 50 za Faksi na vituo 3 vya posta kubwa. Aidha mkoa una vituo vidogo vya posta.

Jedwali XXV linaonyesha hali halisi ya maendeleo ya huduma za mawasiliano zilizopo mijini na katika vitongoji vikubwa vya kibiashara:

**JEDWALI XXV: MGAWANYO WA HUDUMA ZA MAWASILIANO MWAKA 1995**

| | Dodoma | Kondoa | Kongwa | Mpwapwa | Mtera | Mvumi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1993 | | | | | | | |
| Simu | 3465 | 186 | 43 | 139 | 28 | - | 3861 |
| Teleksi | 58 | - | - | - | - | - | 58 |
| 1994 | | | | | | | |
| Simu | 2917 | 185 | 35 | 128 | 18 | - | 3283 |
| Teleksi | 50 | - | - | - | - | - | 51 |
| 1995 | | | | | | | |
| Simu | 2826 | 178 | 36 | 130 | 16 | - | 3186 |
| Teleksi | 50 | - | - | - | - | - | 50 |
| Faksi | 43 | - | - | 1 | - | - | 44 |
| 1996 | | | | | | | |
| Simu | 2605 | 171 | 36 | 132 | 16 | 21 | 2981 |
| Teleksi | 50 | - | - | - | - | - | 50 |
| Faksi | 49 | - | - | 1 | - | - | 50 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa

## 3.4 NISHATI:

### Utangulizi:


Nishati zitumikazo viwandani pamoja na majumbani mkoani ni pamoja na umeme utokanao na nguvu za maji (kutoka Mtera) umeme unaozalishwa na mitambo, diseli, petroli na mafuta ya taa. Hata hivyo, idadi kubwa ya wakazi waishio vijijini wanategemea kuni na mkaa kama vyanzo vya nishati.

### 3.5.1 **Umeme**:

Chanzo kikuu cha nishati mkoani Dodoma ni umeme, hususan umeme unaozalishwa na nguvu za maji. Nishati hii inatumika majumbani, pamoja na viwandani. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni mahitaji halisi ya nishati mkoani Dodoma yameongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na uamuzi wa kuhamisha makao makuu ya serikali kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma na pia kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu katika miji na vitongoji vikubwa vya kibiashara.

Katika mwaka wa 1973 mkoa ulikuwa na uwezo wa kutumia asilimia 30 ya kilowati 3,010 zilizokuwa zinazalishwa, na asilimia 28 ya kilowati 4,326 zilizokuwa zinazalishwa mwaka 1979. Kwa hivi sasa inakisiwa kuwa mahitaji halisi ya umeme ni kilowati 21,200, ikilinganishwa na uzalishwaji wa kilowati 5,250. Jedwali XXVI linaonyesha hali halisi ya umeme uliopelekwa Dodoma na mahitaji.

**Kielelezo 11: Hali halisi ya Umeme uliopelekwa (maelfu ya Kw) Mkoani Dodoma mwaka 1996**




**JEDWALI XXVI: HALI YA UMEME ULIOPELEKWA NA KUTUMIWA MKOANI DODOMA, MWAKA 1996 (Kilowati)**

| | **Wilaya** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Dodoma | Kondoa | Mpwapwa/Kongwa | Jumla |
| Uwezo wa Uzalishaji wote | 7,444 | 952 | 1,035 | 9,431 |
| Uwezo wa Sasa | 4,000 | 900 | 920 | 5,820 |
| Mahitaji halisi | 8,200 | 5,000 | 8,000 | 21,200 |
| Uzalishaji halisi | 4,000 | 450 | 800 | 5,250 |

Chanzo: Shirika la Taifa la Umeme (TANESCO)

### 3.5.2 **Mkaa/Kuni:**

Mkoani Dodoma matumizi ya mkaa na kuni ni njia kuu ya nishati, na inaelekea hali hiyo itaendelea kwa muda mrefu ujao. Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa matumizi ya aina hii ya nishati iliongezeka kutoka mita za ujazo 475,638 za kuni mwaka 1988 hadi kufikia mita za ujazo 2,992,998 mwaka 1995. Ni dhahiri kuwa hali hiyo inapelekea uharibifu mkubwa wa mazingira na misitu iliyopo.

Ili kuepusha uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa jangwa mkoani, wataalam wamependekeza vyanzo mbadala vya nishati viendelezwe matumizi hususan ya umeme na gesi inayozalishwa kutokana na samadi ya wanyama.

### 3.5.3 **Gesi ya samadi ya wanyama:**

Hii ni aina nyingine ya nishati ambayo imeanza kutumika mkoani Dodoma hususan kwa matumizi ya nyumbani. Hadi Desemba, 1996, jumla ya mitambo 103 ya gesi ya samadi ilikuwa imejengwa katika maeneo ya Dodoma Vijijini na mijini. Jitihada kubwa zinaendelea kati ya mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na uongozi wa mkoa katika kuhamasisha wananchi wenye mifugo kutumia teknologia hii.

## SURA YA NNE

## 4.0 HUDUMA ZA JAMII

## 4.1 SEKTA YA ELIMU

### 4.1.1 Elimu ya Msingi

**Shabaha Kuu:**

Shabaha kuu ya ujumla katika mfumo wa elimu ya msingi ni kufanikisha sera ya kuwapatia elimu ya msingi watoto wote wanaostahili kwenda shule, kuanzia umri wa miaka 7 hadi 13. Aidha mfumo huo wa elimu ya msingi unalenga zaidi katika utoaji wa elimu ya vitendo na nadharia ambayo itawafanya watoto wamalizapo elimu ya msingi waweze kujitegemea. Aidha mafanikio ya utekelezaji wa mpango huu wa elimu ya msingi katika mkoa wowote, unapimwa kwa kutumia kigezo hicho.

### 4.1.1.2 Upanuzi wa elimu ya Msingi:

Kipindi cha kati ya mwaka 1973 na 1982 palikuwepo na ongezeko kubwa la upanuzi wa elimu ya msingi mkoani Dodoma. Mafanikio ya upanuzi wa elimu ya msingi mkoani yalitokana na maamuzi ya aina tatu yaliyofanyika kitaifa kama ifuatavyo:- Sera ya kurekebisha vijiji ambayo ilitekelezwa kati ya mwaka 1972 hadi 1974, (b) Maamuzi ya serikali ya kuhamisha makao makuu kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma , na (c) Sera ya kuwapatia elimu ya msingi watoto wote wanaostahili kwenda shule (UPE).

Wakati wa kipindi cha kupata uhuru yaani Desemba 1961, mkoa wa Dodoma ulikuwa na jumla ya shule 186 za msingi zenye darasa la kwanza hadi la nne. Shule chache zilikuwa na darasa la kwanza hadi saba. Pia zilikuwepo shule chache za kati yaani zenye darasa la nne hadi la nane. Hata hivyo mkoa wa Dodoma ulifanikiwa katika muda mfupi kuongeza idadi ya shule za msingi kutoka 312 mwaka 1973/74 hadi kufikia 484 mwaka 1985.

Hadi kufikia mwaka 1996, mkoa ulikuwa na shule 526 za msingi, kati ya hizo shule 20 zilikuwa za watoto wenye matatizo mbalimbali kama vile wasioona, viziwi n.k. Jedwali XXVII linaonyesha maendeleo ya upanuzi wa sekta ya elimu ya msingi katika kipindi cha miaka 19..

**JEDWALI XXVII: UPANUZI WA ELIMU YA MSINGI - SHULE, MIKONDO, IDADI YA WATOTO NA VIWANGO VYA WANAFUNZI**

| Idadi ya | 1973/74 | 1978 | 1982 | 1986 | 1990 | 1994 | 1996 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vijiji | 359 | 384 | 411 | 416 | 422 | 422 | 422 |
| Shule | 312 | 443 | 477 | 484 | 495 | 505 | 526 |
| Mikondo | 1,691 | 3,778 | 4,0365 | 4295 | 4659 | 4874 | 5,128 |
| Wasichana | 28,295 | 84,041 | 94,566 | 84,553 | 85,682 | 91,380 | 96,315 |
| Wavulana | 43,328 | 91,778 | 98,503 | 83,736 | 84,012 | 93,291 | 100,693 |
| Jumla wanafunzi | 71,624 | 175,819 | 193,069 | 168,589 | 169,694 | 184,490 | 197,108 |
| Asilimia ya Wanafunzi waliopo | 49.8 | 82.4 | 85.7 | 78.6 | 75.8 | 70.6 | 61.8 |
| Waalimu | 1416 | 3,261 | 4,824 | 5,166 | 5,217 | 5,614 | 5,583 |
| Uwiano wa Waalimu kwa wanafunzi | 1:50 | 1:54 | 1:40 | 1:33 | 1:32 | 1:33 | 1:35 |

Chanzo: Tume ya Mipango, kwa kuzingatia:

(a) Takwimu kuhusu elimu na mafunzo
(b) Takwimu kuhusu elimu ya kimsingi: (BEST) 1994
(c) RIDEP ya Dodoma - 199
(d) Taarifa za mwaka za Mkoa wa Dodoma.
(iv) Taarifa za mkoa za mwaka


### 4.1.13 Uandikishaji kwa Ujumla:

Mkoa wa Dodoma ni miongoni mwa mikoa iliyofanikiwa sana katika utekelezaji wa agizo la kuwaandikisha shule watoto wote wanaostahili (UPE). Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 1969 hadi 1974 palikuwepo na ongezeko la kadri la uandikishwaji shule kutoka watoto 42,384 hadi kufikia watoto 54,752. Pia, kutoka mwaka 1975 hadi 1982 andikishaji uliongezeka sana kuliko miaka ya nyuma na kufikia watoto 193,069 mwaka 1982. Hata hivyo, uandikishaji ulipungua kati ya mwaka 1983 hadi 1988 kutoka watoto 193,069 mwaka 1983 hadi watoto 160,644 mwaka 1988. Baada ya mwaka 1988 uandikishaji uliendelea kuongezeka kwa kiwango cha wastani hadi mwaka 1996.

Aidha mwaka 1996 mkoa ulikuwa na jumla ya shule 526 za msingi zenye jumla ya wanafunzi 197,108. Kwa hali hii, sera ya uandikishaji watoto wote wanaostahili kwenda shule iliongeza kwa kiwango kikubwa nafasi za shule tokea mwaka 1982.

Jedwali XXVIII linaonyesha viwango vya uandikishaji watoto wa shule za msingi kati ya mwaka 1973 hadi 1996. Katika mwaka 1996 kiwango cha ujumla cha uandikishaji shule watoto kilikuwa asilimia 61.8 kiwango ambacho ni chini kidogo ya wastani wa kitaifa, ambao ulikuwa asilimia 63.5. Hata hivyo uandikishaji wa jumla wa watoto uliendelea kupungua tokea mwaka 1982.

**Kielelezo 12: Uandikishaji wa jmla wa watoyto shle za msingi (maelfu) mkoa wa Dodoma**




**JEDWALI XXVIII: UANDIKISHAJI WA WATOTO KATIKA SHULE ZA MSINGI MKOA WA DODOMA, 1990 - 1996**

| Mwaka | Idadi ya Shule | Madarasa | | | | Jumla Wanafunzi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Darasa I -IV | Darasa V | Darasa VI | Darasa VII | |
| 1990 | 496 | 111502 | 18341 | 25673 | 14219 | 167570 |
| 1991 | 499 | 111860 | 21720 | 15288 | 24749 | 173617 |
| 1992 | 505 | 116704 | 21777 | 21811 | 15720 | 176012 |
| 1993 | 505 | 113614 | 24689 | 20551 | 20689 | 179183 |
| 1994 | 505 | 114857 | 23793 | 25566 | 20388 | 184604 |
| 1996 | 526 | 131088 | 23081 | 21924 | 21015 | 197108 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa - Dodoma

**JEDWALI XXXI: UANDIKISHAJI WA JUMLA WA WANAFUNZI SHULE ZA MSINGI KIJINSIA MKOA WA DODOMA, 1980 - 1996**

| Mwaka | Wavulana | Wasichana | Jumla |
|---|---|---|---|
| 1980 | 101,336 | 90,947 | 192,283 |
| 1981 | 105,887 | 96,960 | 202,847 |
| 1982 | 98,503 | 94,566 | 193,069 |
| 1983 | 94,298 | 92,932 | 187,230 |
| 1984 | 91,539 | 92,252 | 183,791 |
| 1985 | 82,798 | 83,777 | 166,575 |
| 1986 | 82,819 | 85,770 | 168,589 |
| 1987 | 80,404 | 83,872 | 164,276 |
| 1988 | 79,016 | 81,628 | 160,644 |
| 1989 | 80,095 | 82,275 | 162,370 |
| 1990 | 82,486 | 85,084 | 167,570 |
| 1991 | 83,610 | 90,007 | 173,617 |
| 1992 | 87,690 | 88,322 | 176,012 |
| 1993 | 89,875 | 89,308 | 179,183 |
| 1994 | 92,073 | 92,598 | 184,671 |
| 1995 | 92,583 | 91,812 | 184,395 |
| 1996 | 100,693 | 96,315 | 197,108 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) - Dodoma

## 4.1.1.4 Uandikishaji Darasa la Kwanza

Katika mwaka 1995, kati ya watoto 76,410 waliofikia umri wa kuanza shule ni asilimia 41.2 tu ndiyo walioandikishwa. Kati ya walioandikishwa wilaya ya Mpwapwa iliandikisha wanafunzi wengi zaidi kuliko zingine yaani asilimia 87, Dodoma Vijijini ilikuwa na kiwango kidogo kuliko wilaya zingine, yaani asilimia 23. Viwango vya chini vya uandikishaji vilijitokeza zaidi katika wilaya ya Dodoma vijijini kutokana na mila na desturi ya kabila la Wagogo, ambapo wavulana na wasichana hulazimishwa na wazazi kwenda kuchunga mifugo badala ya kwenda shule.

Sababu ya pili ni tabia ya wasichana kuolewa wangali bado shuleni. Kwa sababu hiyo uandikishaji shule wa watoto wa kike umekuwa wa chini ikilinganishwa na watoto wa kiume. Kwa mfano katika mwaka 1995 asilimia 51.3 ya watoto walioandikishwa walikuwa wavulana na asilimia 46.9 walikuwa wasichana.

**JEDWALI XXX: UANDIKISHAJI WATOTO DARASA LA KWANZA KIWILAYA MWISHO WA MWAKA 1995**

| Wilaya | Idadi ya shule za msingi | Idadi ya watoto miaka 7-13 | Idadi ya watoto walioandikishwa | Asilimia ya walioandikishwa |
|---|---|---|---|---|
| Kondoa | 172 | 25,340 | 10,643 | 42 |
| Dodoma (V) | 135 | 30,044 | 7,071 | 23 |
| Mpwapwa | 141 | 8,579 | 7,522 | 87 |
| Dodoma (M) | 59 | 12,447 | 5,458 | 43 |
| Jumla | 505 | 76,410 | 30,694 | 41.2 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa - Dodoma

Kama jedwali XXX hapo juu linavyoonyesha, uandikishaji wa wavulana na wasichana katika darasa la kwanza ulipungua mwaka hadi mwaka. Hali hiyo ni mbaya sana katika wilaya ya Dodoma vijijini. Katika mwaka 1996 idadi ya wanafunzi waliomaliza darasa la saba na wanafunzi walioanza darasa la kwanzna hali ni kama ifuatavyo:

| Darasa | Wavulana | Wasichana | Jumla |
|---|---|---|---|
| I | 4,723 | 4,488 | 9,211 |
| II | 2,650 | 2,489 | 5,139 |
| Hawakumaliza Shule | 2,073 | 1,999 | 4,072 |

Aidha tatizo ambalo linahitaji ufumbuzi mapema ni upungufu wa madarasa katika shule za msingi za mijini. Shule nyingi zina wanafunzi hadi 110 kwa darasa moja badala ya wanafunzi 45. Kwa upande mwingine tofauti na shule za mjini, baadhi ya shule za vijijini zina wanafunzi pungufu kwa darasa. Kwa mfano, darasa moja lina wanafunzi pungufu zaidi ya 25. Kwa sababu hii kuna haja ya kujenga madarasa mapya katika shule zilizopo mjini.

#### 4.1.1.5 Matatizo yanayokabili Elimu ya Msingi

Kama ilivyo katika baadhi ya mikoa hapa nchini mkoa wa Dodoma una matatizo mengi yanayokwamisha maendeleo ya elimu ya msingi. Matatizo hayo ni kama vile upungufu wa majengo, samani za shule, waalimu, utoro wa wanafunzi na vifaa muhimu.

**JEDWALI XXXI: VIFAA VILIVYOPO VYA SEKTA YA ELIMU MKOANI DODOMA IKILINGANISHWA NA BAADHI YA MIKOA - 1994**


| Vigezo | **Dodoma** | Arusha | Iringa | Morogoro | Singida |
|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya shule za msingi | **505** | 579 | 710 | 625 | 349 |
| Idadi ya Majengo | | | | | |
| Vyumba vya madarasa | **2,353** | 3,382 | 4,496 | 3,146 | 2,056 |
| Nyumba za Waalimu | **1,117** | 1,583 | 2,729 | 1,427 | 1,442 |
| Vyoo | **1,841** | 2,166 | 5,515 | 2,104 | 2,036 |
| Idadi ya mikondo | **4,874** | 6,039 | 6,987 | 5,543 | 3,575 |
| Idadi ya Waalimu | **5,586** | 5,557 | 5,992 | 5,614 | 3,556 |
| Shule za Sekondari | **17** | 36 | 45 | 23 | 10 |
| - za umma | **10** | 13 | 13 | 13 | 5 |
| - za binafsi | **7** | 23 | 32 | 10 | 5 |
| Idadi ya Mikondo | | | | | |
| - za umma | **113** | 119 | 187 | 150 | 53 |
| - za binafsi | **48** | 235 | 247 | 111 | 30 |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Utamaduni, 1996

## (i) Majengo ya Shule za Msingi

1. Mkoa wa Dodoma una upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia pamoja na majengo ya shule, kama madarasa, nyumba za waalimu, ofisi za waalimu pamoja na vyoo. Hali ni mbaya sana katika shule za vijijini, kwani karibu majengo yote yamejengwa kwa matofali ya tope, na kuezekwa kwa nyasi. Waalimu wanafundisha vijijini wanaishi katika nyumba mbovu zijulikanazo kama "Matembe". Vile vile asilimia 90 ya shule za vijijini hazina vyoo. Jedwali na. XXXII linaonyesha hali ya majengo ya shule ilivyo mkoani mwaka 1995.

**Kielelezo 13: Hali ya majengo ya shule Mkoani Dodoma, 1995**



**JEDWALI XXXII: MGAWANYO WA VYUMBA VYA MADARASA KIWILAYA MKOANI DODOMA - 1995**

| Majengo | Mahitaji | Idadi halisi | Upungufu | Asilimia upungufu |
|---|---|---|---|---|
| Madarasa | 4021 | 2,561 | 1,460 | 36.31 |
| Walimu | 5,324 | 1,234 | 4,090 | 76.82 |
| Vyoo | 5,697 | 1,419 | 5,464 | 95.9 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) Dodoma


Kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali na. XXXII, upungufu wa vyoo unaonyesha kwamba ni tatizo kubwa kwani upo upungufu wa asilimia 95 ikifuatiwa na waalimu. Vile vile upungufu wa madarasa ni asilimia 36.31. Hata hivyo, takwimu hizi hazielezei hali halisi ilivyo vijijini kwani karibu madarasa yote yalipo huko sio ya kudumu. Hali hii inaonyesha kwamba, upungufu wa madarasa mkoani Dodoma ni zaidi ya asilimia 36.31 iliyotajwa hapo juu

**JEDWALI XXXIII: MGAWANYO WA MADAWATI KIWILAYA**

| Wilaya | Mahitaji | Idadi halisi | Upungufu |
|---|---|---|---|
| Kondoa | 1240 | 874 | 366 |
| Dodoma (V) | 912 | 346 | 566 |
| Mpwapwa | 1222 | 845 | 377 |
| Dodoma (M) | 647 | 496 | 151 |
| Jumla | 4021 | 2561 | 1460 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) Dodoma

**Kielelezo 14: Mgawanyo wa vyumba vya madarasa kiwilaya, Mkoa wa Dodoma, 1995**





Uwiano wa darasa / wanafunzi mkoani Dodoma ni darasa moja kwa wanafunzi 72 yaani, 1:72. Hata hivyo, madarasa ya mjini yana wanafunzi wengi zaidi. Uwiano wa darasa / wanafunzi wa mkoa ni mkubwa kuliko wa kitaifa wa wanafunzi 45 kwa darasa moja.

**(ii) Vifaa Muhimu vya Shule na Samani.**

Upungufu wa samani kama madawati, viti meza, ,mbao na vifaa vya kufundishia vimechangia utoaji wa elimu duni. Jedwali XXXIV linaonyesha kwamba mwaka 1996 mkoa ulikuwa na upungufu wa madawati wa asilimia 43.1.

Kielelezo 15: Mgawanyo wa Madawati Kiwilaya Mkoa wa Dodoma, 1995




**JEDWALI XXXIV: IDADI YA MADAWATI KIWILAYA MKOANI DODOMA, 1995**

| Wilaya | Mahitaji | Yaliopo | Upungufu | Asilimia ya upungufu |
|---|---|---|---|---|
| Kondoa | 19,562 | 9,521 | 10,041 | 48.6 |
| Dodoma (V) | 16,266 | 6,443 | 9,823 | 39.6 |
| Mpwapwa | 27,354 | 20,650 | 6,704 | 75.4 |
| Dodoma (M) | 11,902 | 6,111 | 5,791 | 51.3 |
| Mkoa | 75,084 | 42,725 | 32,359 | 43.1 |

Chanzo: Ofisi ya Elimu Mkoa - Dodoma

### (iii) Waalimu wa Shule za Msingi:

Upungufu mkubwa wa waalimu wa shule za msingi pamoja na mgawanyo wake usioridhisha ni matatizo yanayoikabili sekta hii ya elimu ya msingi.
Takwimu za mwaka 1996 zinaonyesha kuwa wilaya ya Kondoa iliathirika zaidi kwa kuwa na upungufu wa waalimu 445, ikifuatiwa na wilaya ya Dodoma vijijini na Manispaa ya Dodoma. Kwa upande mwingine, wilaya ya Mpwapwa/Kongwa wapo waalimu wa kutosha. Katika mwaka 1996 kwa mfano, wilaya ya Mpwapwa/Kongwa ilikuwa na upungufu wa waalimu 18 tu, sawa na asilimia 1.2.

**JEDWALI XXXV: MGAWANYO WA WAALIMU KIWILAYA, MKOA WA DODOMA, 1996**

| Wilaya | Mahitaji | Idadi kamili | Upungufu | Asilimia ya upungufu |
|---|---|---|---|---|
| Kondoa | 1,834 | 1,389 | 445 | 23.5 |
| Dodoma (V) | 1,433 | 1,353 | 80 | 5.6 |
| Mpwapwa | 1,492 | 1,474 | 18 | 1.2 |
| Dodoma (M) | 824 | 754 | 65 | 8.5 |
| Jumla | 5,583 | 4,975 | 608 | 10.9 |


Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) Dodoma

### (iv) Wanafunzi wanaoacha shule katika shule za msingi:

Ukatizaji wa masomo katika shule za msingi ni tatizo sugu mkoani Dodoma. Kwa mfano, katika mwaka 1996,

jumla ya wanafunzi 1,897 wa shule za msingi walikatiza masomo yao mkoani Dodoma. Kati ya idadi hiyo, wanafunzi 1,008 walikuwa wavulana na 889 wasichana.

**Kielelezo 16: Mgawanyo wa Waalimu Kiwilaya - Mkoa wa Dodoma mwaka 1996**





**JEDWALI XXXVI: SABABU ZA KUKATIZA MASOMO KIJINSIA, MKOANI DODOMA, 1996**

| Sababu | Jinsia | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Wavulana | Wasichana | |
| Utoro | 877 | 589 | 1,466 |
| Mimba | - | 215 | 215 |
| Vifo | 99 | 68 | 167 |
| Sababu zingine | 32 | 17 | 49 |
| Jumla | 1,008 | 889 | 1,897 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) Dodoma

Takwimu za jedwali XXXVI zinaonyesha kwamba utoro ndiyo sababu kubwa inaongoza kwa ukatizaji wa masomo kwa wanafunzi wa shule za msingi mkoani Dodoma. Sababu zingine ni pamoja na kushika mimba, kuolewa wasichana wangali shuleni, na vifo. Katika mwaka 1993 kwa mfano, wanafunzi 897 sawa na asilimia 67.4 walikatiza masomo kutokana na utoro.

**Kielelezo 17: Sababu za kukatiza masomo kijinisia Mkoani Dodoma, 1996**




**JEDWALI XXXVII: SABABU ZA KUKATIZA MASOMO KIJINSIA, MKOA WA DODOMA (1993-1996)**

| **Mwaka/Jinsia** | **Sababu za ukatizaji Masomo** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Utoro** | **Mimba** | **Vifo** | **Sababu zingine** |
| 1993 | | | | |
| Wavulana | 544 | 4 | 116 | 28 |
| Wasichana | 353 | 148 | 105 | 34 |
| **Jumla** | 897 | 152 | 221 | 62 |
| 1994 | | | | |
| Wavulana | 734 | 1 | 133 | 31 |
| Wasichana | 482 | 181 | 87 | 37 |
| **Jumla** | 1,216 | 182 | 220 | 68 |
| 1995 | | | | |
| Wavulana | 809 | - | 87 | 25 |
| Wasichana | 524 | 163 | 83 | 14 |
| **Jumla** | 1,333 | 163 | 170 | 39 |
| 1996 | | | | |
| Wavulana | 877 | - | 99 | 32 |
| Wasichana | 589 | 215 | 68 | 17 |
| **Jumla** | 1,466 | 215 | 167 | 49 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) - Dodoma

**Kielelezo 18: Sababu za kukatiza masomo kijinsia Mkoa wa Dodoma**




(a) **Utoro Shuleni:**

Takwimu za ujumla za wanafunzi wanaokatiza masomo ya shule za msingi ni kubwa mkoani Dodoma. Kwa mfano, katika mwaka 1996 sababu kubwa iliyoainishwa hapo juu ni utoro. Katika mwaka huo, takwimu zinaonyesha kuwa kulikuwepo na wanafunzi 1,466 watoro, ambapo 877 walikuwa wavulana na 589 wasichana. Mara nyingi utoro wa wanafunzi wavulana unasababishwa na wavulana kupenda kufanya biashara ndogo ndogo katika vituo vya reli vya kati, maeneo ya vitongoji vya kibiashara pamoja na miji mikubwa. Katika maeneo mengine husㅤusan Dodoma vijijini, wazazi wengi wanayo tabia ya kuwakatiza shule wanafunzi wavulana kwa ajili ya kuchunga mifugo. Kwa upande mwingine, wanafunzi

wasichana hulazimishwa kuolewa wakiwa bado shuleni na wenye umri mdogo.

(b) **Mimba:**

Tatizo la watoto wa kike kushika mimba limeanza kujitokeza kwa kasi zaidi hivi sasa kuliko zamani. Katika mwaka wa masomo wa 1993, kwa mfano, jumla ya wanafunzi 148 wa kike na 4 wa kiume walihusishwa na kitendo hiki na hatimaye kufukuzwa shule. Kati ya mwaka 1994 yalikuwepo matukio 182 ya mimba na mwaka 1995 yalikuwepo matukio 168. Matukio 215 ya mimba yalijitokeza mwaka 1996, na wanafunzi wote waliohusika walifukuzwa shule. Hali hii inatisha na kwa sababu hiyo wazazi, waalimu na viongozi wa halmashauri za wilaya na mkoa hawana budi kutafuta ufumbuzi wa hudumu wa tatizo hili.

(c) **Vifo :**

Idadi ya vifo vya wanafunzi imepungua. Hata hivyo viwango vya vifo vya jumla vinaongezeka. Kwa ajili hiyo, upo umuhimu kwa uongozi wa mkoa na wilaya wa kufanya utafiti na kuainisha sababu za kimsingi zinazopelekea vifo hivyo kwa shabaha ya kuchukua hatua thabiti dhidi ya tatizo hili.

(d) **Kukosa Masomo**

Tatizo la wanafunzi kukosa masomo ni kubwa mkoani Dodoma. Takwimu za mwaka 1992 za kitaifa zinaonyesha kuwa Dodoma ulikuwa mkoa wa pili baada ya mkoa wa Shinyanga (asilimia 63) ambao ulikuwa unaongoza. Hata hivyo kukosa masomo ni kielelezo cha mfumo wa maisha wa jamii fulani katika mikoa. Kwa mfano idadi kubwa ya watu wa mikoa ya Shinyanga na Dodoma ni wafugaji ambao huthamini mifugo zaidi kuliko elimu kwa watoto wao.

## 4.1.2 Elimu ya Sekondari

### 4.1.2.1 Utangulizi

Dodoma ni mojawapo ya mikoa ambayo haijapiga hatua kubwa katika elimu ya sekondari. Katika miaka ya 1960 kwa mfano, mkoa ulikuwa na sekondari mbili tu za umma yaani "Dodoma Alliance Secondary School", iliyojengwa na umoja wa madhehebu ya ki-Anglikani, na sekondari ya serikali ya Bihawana. Hata hivyo, idadi ya shule za sekondari za umma ziliongezeka hadi kufikia 13 mwaka 1996. Mwaka 1998 mkoa una shule 22 za sekondari, ambapo tisa kati ya hizo ni za watu/mashirika binafsi. Kati ya idadi hiyo ya shule, 10 ziko ndani ya Manispaa ya Dodoma. Baadhi ya shule za sekondari za watu binafsi na mashirika zilizoko vijijini, inasemekana hazina vifaa wala waalimu wa kutosha.

**JEDWALI XXXVIII: MGAWANYO WA SHULE ZA SEKONDARI KIWILAYA, 1995**

| Wilaya | Idadi ya Shule za Sekondari | | |
|---|---|---|---|
| Wilaya | za Umma | za Watu/Mashirika | Jumla |
| Kondoa | 4 | 1 | 5 |
| Dodoma (V) | 1 | 1 | 2 |
| Mpwapwa | 4 | 1 | 5 |
| Dodoma (M) | 4 | 6 | 10 |
| Jumla | 13 | 9 | 22 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) Dodoma

Jedwali XXXIX linalinganisha idadi ya shule za sekondari mkoani Dodoma na baadhi ya mikoa ya jirani.

**JEDWALI XXXIX: IDADI YA SHULE ZA SEKONDARI MKOANI DODOMA IKILINGANISHWA NA MIKOA YA JIRANI**

| | Idadi ya shule za sekondari | | |
|---|---|---|---|
| Mkoa | Za Umma | Za Binafsi | Jumla |
| Arusha | 13 | 23 | 36 |
| **Dodoma** | **13** | **9** | **22** |
| Iringa | 10 | 32 | 42 |
| Kilimanjaro | 15 | 62 | 77 |
| Singida | 5 | 9 | 14 |
| Tabora | 10 | 9 | 19 |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Utamaduni (BEST), 1994

Uongozi wa mkoa wa Dodoma umeazimia kujenga shule moja ya sekondari angalau kwa kila tarafa ili kukidhi mahitaji ya elimu ya sekondari na elimu ya ufundi yaliyopo mkoani. Aidha watu binafsi na mashirika ya umma wanakaribishwa kufungua na kuendesha shule za msingi na za sekondari.

#### 4.1.2.2 Uandikishaji katika Elimu ya Sekondari

Kutokana na uhaba wa shule za sekondari mkoani ni wanafunzi wachache wanaofanikiwa kupata nafasi katika shule zilizopo. Idadi ya wanafunzi wanaofanikiwa kupata nafasi za kidato cha kwanza kutoka mkoa wa Dodoma ni ndogo sana ikilinganishwa na mikoa ilivyoendelea kielimu kama mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro, Kagera na Tanga. Takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba mwaka 1990 ni asilimia 4.3 tu ya wanafunzi waliofanya mtihani wa darasa la VII ndiyo waliopata nafasi ya kidato cha I katika shule za sekondari za umma. Kiwango hicho kiliongezeka mwaka 1995 hadi kufikia asilimia 5.8, wakati wastani wa kitaifa ulikuwa asilimia 6.3. Hata hivyo, idadi ya wanafunzi wanaosoma katika shule za sekondari katika mkoa wa Dodoma iliongezeka kutoka wanafunzi 5,605 mwaka 1991 hadi kufikia wanafunzi 28,485 mwaka 1995.

**JEDWALI XL: UANDIKISHAJI WANAFUNZI SHULE ZA SEKONDARI, KWA KIDATO, MKOA WA DODOMA, 1991-1995**

| Mwaka | Kidato/Darasa | | | | | | Jumla ya Wanafunzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kidato I | Kidato II | Kidato III | Kidato IV | Kidato V | Kidato VI | |
| 1991 | 1445 | 1201 | 1129 | 917 | 276 | 434 | 5607 |
| 1992 | 1352 | 1406 | 1120 | 1036 | 263 | 292 | 5517 |
| 1993 | 1440 | 1396 | 1276 | 1173 | 193 | 191 | 5720 |
| 1994 | 1170 | 1447 | 1057 | 960 | 287 | 264 | 4855 |
| 1995 | 1722 | 1756 | 1390 | 1322 | 31 | 282 | 6783 |
| Jumla | 7129 | 7127 | 6025 | 5408 | 1322 | 1463 | 28482 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) Dodoma


**JEDWALI XLI: WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KUINGIA SHULE ZA SEKONDARI, MKOANI DODOMA**

| Mwaka | Waliomaliza Darasa la VII | Waliochaguliwa Kidato cha I | | | Asilimia yake |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Wavulana | Wasichana | Jumla | |
| 1990 | 18,721 | 467 | 338 | 805 | 4.3 |
| 1991 | 24,892 | 514 | 385 | 899 | 3.7 |
| 1992 | 19,288 | 533 | 435 | 868 | 4.5 |
| 1993 | 19,912 | 547 | 450 | 997 | 5.1 |
| 1994 | 20,388 | 634 | 574 | 1,208 | 6.0 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1995 | 22,275 | 637 | 684 | 1,321 | 5.8 |
| 1996 | 22,778 | 700 | 678 | 1,378 | 6.0 |

Chanzo: Ofisi kya Mkuu wa Mkoa - Dodoma

**Kielelezo 19: Wanafunzi waliochaguliwa kuingia shule za Sekondari - Kijinsia, Mkoa wa Dodoma**




Jedwali XLI linaonyesha kwamba kiwango cha wanafunzi walioingia kidato cha I kilikuwa kinapanda na kushuka mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, ni dhahiri pia kuwa kundi kubwa la wanafunzi, wanaomaliza darasa la saba zaidi ya asilimia 90 wanaongezea idadi ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi.

### 4.1.2.3 Uandikishaji wa Wasichana:

Pamekuwepo na maendeleo mazuri ya kuwapatia elimu wasichana kwa kutazama idadi ya walioingia na kidato cha kwanza. Kati ya mwaka 1990 na 1995 kwa mfano, kati ya wanafunzi 100 walioingia kidato cha kwanza, 44 walikuwa wasichana. Hata hivyo, hali ya uandikishaji wa wasichana katika shule za sekondari

za mkoa wa Dodoma inaonekana sio nzuri kama ilivyo katika elimu ya msingi ambako wanafunzi wasichana ni karibu asilimia 50. Katika madarasa ya juu, hali inazidi, kuwa mbaya zaidi, kwa mfano, kati ya wanafunzi 100 waliojiunga na kidato cha V na VI mkoani Dodoma, mwaka 1994, walikuwa wasichana 25 tu kama jedwali XLII linavyoonyesha.

### 4.1.24 Matokeo ya Mitihani:

Matokeo ya mitihani wa kitaifa wa mwaka 1996 unaonyesha kuwa mkoa wa Mara ndiyo uliyotoa mafanikio mazuri kuliko mikoa mingine yote kwa vigezo vya ubora na uwingi wa wanafunzi, ukifuatiwa na mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Kilimanjaro n.k. Mkoa wa Dodoma ulikuwa wa 20 na wa mwisho, kati ya mikoa yote 20. Hata wilaya za mkoa wa Dodoma matokeo yalikuwa ya chini sana ikilinganishwa na mafanikio ya wilaya zingine zote 109 za nchi hii. Matokeo yake yalikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Manispaa ya Dodoma ilikuwa ya 46 kati ya wilaya 109 zilizopo nchini

(ii) Wilaya ya Mpwapwa/Kongwa ilikuwa ya 89 kati ya wilaya 109 zilizopo nchini

(iii) Wilaya ya Kondoa ilikuwa ya 100 kati ya wilaya 109

(iv) Wilaya ya Dodoma vijijini ilikuwa ya 103 kati ya wilaya zote

Kwa upande mwingine kiwango cha wanafunzi waliochaguliwa kuingia shule za sekondari kimekuwa kinabadilika badilika, kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali XLII.

**JEDWALI XLII: UANDIKISHAJIKATIKA SHULE ZA SEKONDARI KWA JINSIA MKOA WA DODOMA - 1992 HADI 1994**

| Darasa | 1992 | | 1994 | | Asilimia ya Wanawake 1994) |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| Kidato I | 814 | 780 | 1011 | 823 | 5.2 |
| Kidato II | 803 | 814 | 911 | 892 | 8.7 |
| Kidato III | 665 | 631 | 784 | 684 | 7.7 |
| Kidato IV | 614 | 582 | 766 | 695 | 16.3 |
| Kidato V | 237 | 56 | 253 | 54 | -0.3 |
| Kidato VI | 225 | 66 | 224 | 66 | 0.0 |
| Jumla | 3388 | 2929 | 3949 | 3111 | |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) Dodoma

**JEDWALI XLIII: MGAWANYO WA WANAFUNZI KIJINSIA WALIOFANYA MTIHANI WA DARASA VII NA WALIOFAULU MWAKA 1997 MKOA WA DODOMA**

| Wilaya | Idadi ya ya Shule | Idadi ya Waliofanya Mtihani - 1997 | | | Waliofaulu Mtihani | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Asilimia ya Ongezeka |
| Nanispaa | 58 | 1,772 | 1,963 | 3,735 | 366 | 233 | 599(16%) |
| Dodoma (V) | 134 | 2,153 | 2,401 | 4,554 | 191 | 38 | 229(5%) |
| Kondoa | 167 | 2,682 | 3,113 | 5,795 | 280 | 88 | 368(6%) |
| Mpwapwa | 79 | 1,426 | 1,414 | 2,840 | 74 | 27 | 101(4%) |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kongwa | 58 | 1,151 | 1,172 | 2,323 | 1,078 | 517 | 159(68%) |
| Jumla | 496 | 9,184 | 10,063 | 19,247 | 1,989 | 903 | 2,892(15%) |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) Dodoma

Kama jedwali XLIII linavyoonyesha, wilaya ya Kongwa imepata mafanikio makubwa kwani asilimia 68 ya watahiniwa wa darasa la saba walifaulu mtihani, ikifuatiwa na Manispaa ya Dodoma kwa asilimia 16. Wilaya za Mpwapwa - 4%, Dodoma(V) - 5% na Kondoa - 6% matokeo hayo hayaridhishi.

Kitaifa, mwaka 1996 mkoa wa Dodoma ulishika nafasi ya mwisho yaani mkoa wa 20, na mwaka 1997 ulikuwa mkoa wa 16.

### 4.1.3 TAASISI ZA MAFUNZO

Mkoa wa Dodoma ni mojawapo ya mikoa michache yenye taasisi nyingi na nzuri kwa ajili ya elimu ya wasiojiweza. Hadi sasa mkoa unazo taasisi 10, ambapo kati ya hizo Manispaa ya Dodoma ina shule mbili za wasioona na wenye akili tahira. Wilaya ya Dodoma inayo shule moja ya wanafunzi wasioona, wakati wilaya ya Mpwapwa inazo shule mbili za wanafunzi tahira, wakati wilaya ya Kondoa inazo shule nne za wanafunzi tahira.

Pamoja na mkoa kuwa na shule hizi maalumu, mkoa pia una taasisi za kiufundi kama zinavyonyeshwa katika jedwali XLIV hapa chini.

**JEDWALI XLIV: MSAMBAO WA TAASISI ZA MAFUNZO MKOANI DODOMA, 1995**

| VYUO | IDADI |
|---|---|
| • Vyuo vya mafunzo ya Ualimu | 2 |
| • Vyuo vya mafunzo ya wananchi | 2 |
| • Vyuo cya mafunzo ya Mifugo | 1 |
| • Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini | 1 |
| • Chuo cha Biashara | 1 |
| • Chuo cha Mafunzo ya Serikali za Mitaa | 1 |
| • Vyuo vya Ufundi | 2 |
| • Vyuo vya Mafunzo ya Afya | 2 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) Dodoma

## 4.1.4 ELIMU YA WATU WAZIMA

Kiwango cha wananchi wasiojua kusoma na kuandika inazidi kuongezeka mkoani Dodoma hususan katika maeneo ya vijijini, ambako inakisiwa kufikia asilimia 38 kwa wanaume na asilimia 47 kwa wanawake.

Matokeo ya Sensa ya mwaka 1967, 1978 na 1988 yanaonyesha kuwa kiwango cha wananchi waliokuwa wanajua kusoma na kuandika kilifikia asilimia 24(1967) 37.8(1978) na 48.2 (1988). Hata hivyo, kampeni ya elimu kwa watu wasiojua kusoma na

kuandika iliyofanyika miaka ya 1970 na 1980 iliongeza kwa kiwango kikubwa watu wanaojua kusoma na kuandika kutoka asilimia 24 mwaka 1978 hadi asilimia 65.5 mwaka 1990. Hata hivyo pamoja na mafanikio hayo, mwaka 1996 kiwango cha watu wenye uwezo wa kusoma na kuandika kilishuka hadi kufikia asilimia 58. Utelekezaji wa mpango huu wa elimu ya watu wazima umeshindwa kujiendesha mwenyewe kwani tangu ulipoanza miaka ya 1970 utekelezaji wake ulitegemea fedha kutoka serikali kuu na michango mdogo kutoka kwa walengwa. Jedwali XLV linaonyesha mafanikio ya elimu ya watu wazima mkoani Dodoma kama taarifa za sensa ya mwaka 1978 na 1988 zinavyoonyesha.

**JEDWALI XLV: VIWANGO VYA WATU WANAOJUA KUSOMA NA KUANDIKA KIJINSIA MKOANI DODOMA, MWAKA 1978 NA 1988**

| MWAKA | WANAUME - % | | | WANAWAKE - % | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Vijijini | Mijini | Jumla | Vijijini | Mijini | Jumla |
| 1978 | 59.7 | 83.5 | 62.2 | 35.4 | 64.1 | 37.8 |
| 1988 | 61.5 | 85.4 | 64.3 | 45.1 | 73.1 | 48.2 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) Dodoma

**JEDWALI XLVI: IDADI YA WATU WENYE UMRI WA MIAKA 5 NA ZAIDI, WANAOJUA KUSOMA - (KISWAHILI) NA KUANDIKA KIJINSIA, MKOA WA DODOMA 1988**

| MAKUNDI YA UMRI | JUMLA WOTE | | | WANAOJUA KUSOMA/KUANDIKA (SWAHILI) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| 5 - 9 | 96522 | 97142 | 193664 | 6792 | 9236 | 16028 |
| 10 - 14 | 81286 | 81419 | 162705 | 50933 | 55594 | 106527 |
| 15 - 19 | 66927 | 70139 | 137066 | 55154 | 55430 | 110584 |
| 20 - 24 | 41793 | 54434 | 96227 | 34910 | 39299 | 74209 |
| 25 - 29 | 41844 | 50429 | 92273 | 32057 | 25695 | 57752 |
| 30 - 34 | 29099 | 32755 | 61854 | 20333 | 12493 | 32826 |
| 35 - 39 | 24290 | 29313 | 53603 | 16158 | 9540 | 25698 |
| 40 - 44 | 19474 | 25432 | 44906 | 11665 | 4965 | 16630 |
| 45 - 49 | 19156 | 21609 | 40765 | 9967 | 3096 | 13063 |
| 50 - 54 | 13795 | 17840 | 31635 | 5728 | 1544 | 7272 |
| 55 - 59 | 12671 | 13083 | 25754 | 4948 | 1089 | 6037 |
| 60 - 64 | 10860 | 12743 | 23603 | 2843 | 703 | 3546 |
| 65 - 69 | 10583 | 9996 | 20579 | 2491 | 554 | 3046 |
| 70 - 74 | 7664 | 7707 | 15371 | 1283 | 281 | 1564 |
| 75 - 79 | 4202 | 3682 | 7884 | 680 | 87 | 767 |
| 80+ | 6935 | 7436 | 14371 | 654 | 135 | 789 |
| N.S. | 574 | 1015 | 1589 | 63 | 75 | 138 |
| Total | 487675 | 536174 | 1023849 | 256659 | 219816 | 476476 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Elimu) Dodoma

## 4.2 Sekta ya Afya

### 4.2.1 Hali ya Afya Mkoani

Hali ya maendeleo ya sekta ya afya mkoani Dodoma haitofautiani sana na mikoa mingine yenye kiwango cha chini cha maendeleo kama Dodoma. Magonjwa yafuatayo ndiyo yanayosumbua sana

watu wa Dodoma; malaria, magonjwa ya ngozi, magonjwa ya macho, magonjwa ya kuambukiza, kuharisha, yanayoambukiza kwa pumzi, minyoo na magonjwa mengine kama yanavyoonyeshwa katika jedwali XLVII.

**JEDWALI XLVII: MATUKIO YA MAGONJWA YANAYOONGOZA KIWILAYA IKILINGANISHWA NA WASTANI WA MKOA 1995**

| MAGONJWA | MATUKIO % | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Dodoma Manispaa | Dodoma Vijijini | **Mpwapwa /Kongwa** | **Kondoa** | **Jumla ya Mkoa** |
| 1. Malaria | 37.15 | 46.63 | 43.28 | 46.50 | 44.85 |
| 2. Dondakoo | 16.87 | 15.26 | 17.07 | 17.55 | 17.02 |
| 3. Magonjwa ya macho | 13.58 | 12.96 | 9.22 | 11.40 | 12.20 |
| 4. Kuharisha | 13.85 | 8.90 | 10.59 | 8.78 | 10.58 |
| 5. Magonjwa ya ngozi | 3.70 | 4.45 | 6.09 | 4.56 | 4.79 |
| 6. Minyoo | 2.66 | 3.51 | 4.44 | 3.0 | 3.48 |
| 7. Vichomi | 2.61 | 2.11 | 1.86 | 1.62 | 2.09 |
| 8. Magonjwa ya Zinaa | 4.72 | 2.97 | 4.94 | 3.0 | 3.13 |
| 9. Upungufu-Damu | 2.85 | 1.44 | 1.48 | 1.60 | 1.08 |
| 10 Magonjwa- ya Masikio | 2.01 | 1.77 | 1.03 | 1.99 | 0.78 |

Chanzo: Taarifa ya Mwaka ya Afya - Mkoa, 1995

Mbali na kuwepo kwa magonjwa ya kawaida katika jamii ya mkoa wa Dodoma, viwango vya vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka moja na watoto wadogo chini ya miaka mitano, vifo vya akina mama wajawazito na viwango vya vifo vya kawaida, ni vikubwa ikiliganishwa na wastani wa kitaifa.

Takwimu za mwaka 1995 za hali ya LISHE mkoani Dodoma zinaonyesha kuwa wastani wa asilimia 51.6 ya watoto wote chini ya miaka mitano walikuwa na utapiamlo mkali. Kiwango hicho ni kikubwa kikilinganishwa na wastani wa kitaifa, asilimia 47. Hata hivyo kuwepo kwa utapiamlo mkali na ule wa wastani miongoni mwa watoto chini ya miaka mitano unatokana na sababu nyingi za kimsingi. Kwa mkoa wa Dodoma, wataalam wa LISHE wameainisha vyanzo vitatu vinavyosababisha utapiamlo kuwa ni:

- Upungufu wa chakula chenye protini

- Kukosekana kwa elimu ya afya ya msingi miongoni mwa jamii kuhusu lishe, ambapo wazazi hawatilii maanani maelekezo wanayopewa wanapohudhuria kliniki.

- Matunzo duni ya watoto kutoka kwa baadhi ya wazazi. Aidha upungufu wa elimu pamoja na kufuata mila na desturi potofu zimechangia sana hali hii.

**JEDWALI XLVIII: ISHARA ZA MSINGI ZA AFYA MKOA WA DODOMA ZIKILINGANISHWA NA LENGO LA KITAIFA MWAKA 200**

| Vigezo vya Afya | Wastani Kitaifa | Wastani wa Dodoma | Lengo la Taifa Ifikapo 2000 |
|---|---|---|---|
| Muda wa kuishi (1988) | 50 | 45 | 60 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • Umri wa kuishi (miaka) | 98 | 130 | 50 per 1,000 |
| • Vifo vya watoto wachanga mwaka 1995 | 155 | 220 | 70 per 1,000 |
| | 200-400 | 214 | 100-200per 100,000 |
| • Vifo vya watoto chini ya miaka 5 | 63% | 46.3% | 100% |
| • Vifo vya akina mama wajawazito | 273,580 | 278,580 | 100,000 |
| • Wanaojua kusoma/kuandika (1995) | 50,000 | 85,782 | n.a |
| • Uwiano watu/hospitali | 5,000-10,000 | 7,675 | n.a |
| • Uwiano watu/kituo cha afya | 883 | 764 | n.a |
| • Uwiano watu/zahanati | 24,930 | 32,738 | 5,000-10,000 |
| • Uwiano watu/kitanda | 47% | 51.6% | 3% |
| • watu/mtaalamu Lishe | 6% | 9% | 3% |
| • Asilimia ya utapiamlo kawaida | | | |

Chanzo: Tume ya Mipango

Karibu majengo mengi ya huduma za afya yalijengwa miaka ya 1960 na 1970, na kutokana na ufinyu wa bajeti za mwaka hadi mwaka, majengo hayo hayajapata fedha za kufanya ukurabati. Pia, ukosefu wa vifaa muhimu pamoja na zana za kitaaluma kumeathiri sana maendeleo ya sekta ya afya mkoani. Taarifa ya afya mkoani Dodoma inadhihirisha kwamba mitambo, zana na vifaa vingi vilivyoko katika hospitali ya mkoa, na hospitali za wilaya, ama vimeharibika, au teknolojia yake imepitwa na wakati.

Mbali ya ufinyu wa bajeti na ukosefu wa zana na vifaa muhimu vya afya, lipo pia tatizo la upungufu wa wataalam wa afya, pamoja na ukosefu wa motisha. Kwa mfano, mwaka 1995, mkoa ulikuwa na madaktari bingwa watatu tu ikilinganishwa na ikama ya madaktari 12. Taarifa ya mkoa ya sekta ya afya inaonyesha kuwa mwaka 1995 mkoa ulikuwa na upungufu wa manesi waliofuzu 252 pamoja na wataalam wengine muhimu. Jedwali XLIX inaonyesha msambao wa watumishi wa afya kiwilaya, mwaka 1995.

**JEDWALI XLIX: MSAMBAO WA WATUMISHI WA AFYA KIWILAYA, 1995**

| | Hospitali ya Mkoa | Kondoa | Mpwapwa | Dodoma (Vijijini | Dodoma Mjini |
|---|---|---|---|---|---|
| Madaktari Wafawidhi | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Madaktari | 8 | 1 | 1 | 5 | 0 |
| Madaktari Wasaidizi | 10 | 3 | 3 | 6 | 1 |
| Bwana Afya | 9 | 5 | 4 | 6 | 9 |
| Maofisa Wauguzi | 49 | 12 | 15 | 12 | 6 |
| Watibabu Wasaidizi | 14 | 28 | 27 | 17 | 22 |
| Ofisa Muuguzi Darafa A | 7 | 1 | 2 | 4 | 3 |
| Ofisa Muuguzi darafa B | 0 | 1 | 3 | 4 | 5 |
| Wakunga | 68 | 48 | 41 | 96 | 74 |
| Matabibu Wasaidizi | - | 22 | 36 | 56 | 21 |
| Vijijini | 2 | 16 | 21 | 24 | 19 |
| Wahudumu wa Afya | 192 | 104 | 147 | - | 137 |
| Wauguzi Wasaidizi | 19 | 16 | 47 | 167 | 26 |
| Bwana Afya Wasaidizi | | | | | |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (RMO) Dodoma

(i) **Viwango vya Vifo:**

Kama ilivyoelezwa hapo juu, takwimu za afya za mwaka 1975, 1985 na 1995 zinaonyesha kuwepo kwa viwango vikubwa vya vifo vya watoto wachanga na watoto chini ya umri wa miaka mitano, mkoani Dodoma, ikilinganishwa na mikoa kama vile Arusha, Singida, Tabora, Kigoma na Mwanza. Kwa mfano, mwaka 1975, Dodoma ilikuwa moja ya mikoa michache yenye viwango vikubwa sana vya vifo vya watoto wachanga (133 kwa kila 1,000 wazaliwao hai) na vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano (225 kwa kila watoto 1,000). Hadi mwaka 1995 mkoa wa Dodoma bado ulikuwa na viwango vya juu vya vifo vya watoto wachanga na wale walio chini ya umri wa

miaka mitano. Hata hivyo pamoja na viwango kuendelea kuwa vikubwa kwa jumla, takwimu kwenye jedwali L zinaonyesha kwamba viwango hivyo vimekuwa vinapungua taratibu katika kipindi hicho.

**JEDWALI L: VIWANGO VYA VIFO VYA WATOTO WACHANGA NA WALE CHINI YA MIAKA MITANO, KIWILAYA, MKOA WA DODOMA, 1975, 1985 NA 1995**

| Miaka | Viwango vya vifo vya Watoto wachanga | | Vifo vya Watoto chini ya miaka mitano | |
|---|---|---|---|---|
| | Mkoa wa Dodoma | Wastani Kitaifa | Mkoa wa Dodoma | Wastani Kitaifa |
| 1975 | 133 | 137 | 225 | 223 |
| 1985 | 132 | 115 | 222 | 192 |
| 1995 | 130 | 98 | 220 | 158 |

Chanzo: Takwimu za Afya, 1975

**JEDWALI LI: VIWANGO VYA VIFO VYA WATOTO WACHANGA NA WALE CHINI YA MIAKA MITANO, KIWILAYA, MKOA WA DODOMA, 1995**

| Wilaya | Jumla ya Wakazi | Idadi ya watoto miaka (0-5) | Viwango vya vifo watoto wachanga | Viwango vya vifo watoto chini ya miaka 5 |
|---|---|---|---|---|
| Dodoma V. | 398,000 | 79,600 | 257 | 152 |
| Dodoma M. | 229,500 | 45,900 | 190 | 114 |
| Kondoa | 383,400 | 76,680 | 194 | 116 |
| Mpwapwa/Kongwa | 382,000 | 76,400 | 233 | 138 |
| Wastani Kimkoa | 1,392,900 | 278,580 | 220 | 130 |
| Wastani Kitaifa | 27,100,000 | 5,600,000 | 98 | 155 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Mipango) Dodoma

Mbali ya viwango vya vifo matatizo ya uzalio mkubwa, umaskini na ujio wa watu wengi, bado yanayoukabili mkoa wa Dodoma,

na kusababisha utoaji wa huduma za afya kuwa duni. Kwa hali ilivyo, Dodoma ni mojawapo ya mikoa michache yenye, viwango vikubwa vya vifo vya kawaida, na vifo vya wanawake wajawazito. Pia, mkoa unao watoto wengi wenye utapiamlo mkali (51.6% kwa mwaka 1995) na umri mdogo wa kuishi wa miaka 45 ambao ni umri mfupi zaidi kuliko wastani wa kitaifa wa miaka 52.

**JEDWALI LII: HALI YA VIWANGO VYA VIFO VYA AKINA MAMA WAJAWAZITO KIMKOA 1992-1993**

| Mkoa | Viwango vya Vifo vya Akina Mama Wajawazito | |
|---|---|---|
| | 1992 | 1993 |
| Arusha | 102 | 158 |
| Pwani | 209 | 111 |
| Dar es salaam | 220 | 398 |
| **Dodoma** | **197** | **214** |
| Iringa | 311 | 321 |
| Kagera | 304 | 343 |
| Kigoma | 144 | 155 |
| Kilimanjaro | 126 | 46 |
| Lindi | 262 | 289 |
| Mara | 67 | 59 |
| Mbeya | 67 | 361 |
| Morogoro | 289 | 172 |
| Mtwara | 264 | 212 |
| Mwanza | 221 | 186 |
| Rukwa | 172 | 294 |
| Ruvuma | 225 | 189 |
| Shinyanga | 143 | 188 |
| Singida | 242 | 171 |
| Tabora | 151 | 185 |
| Tanga | 255 | 172 |
| Jumla | 199.0 | 211.0 |

Chanzo: MCH/FP Wizara ya Afya

## (ii) Hali ya Lishe:

Suala la lishe ni suala linalohusu utaratibu wa matumizi ya chakula kwa ajili ya kukua, kuuendeleza na kuimarisha mwili wa binadamu. Matokeo ya utafiti wa mwaka 1992 uliyofanywa na mkoa kwa kushirikiana na Shirika la Lishe (TFNC) ulionyesha kuwa asilimia 44.4 ya watoto wote mkoani Dodoma wamedumaa wakati asilimia 11.5 na 42.6 walikuwa na uzito pungufu. Jedwali lifuatalo

linajaribu kulinganisha viwango vya lishe kati ya mkoa na wastani wa kitaifa.

**JEDWALI LIII: HALI YA LISHE YA MKOA WA DODOMA IKILINGANISHWA NA WASTANI WA KITAIFA(WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5)1992**

| | Uzito mdogo | Utapiamlo mkali | Utapiamlo kawaida |
|---|---|---|---|
| Mkoa wa Dodoma | 16% | 51.6% | 9% |
| Wastani Kitaifa | - | 47% | 5% |

Chanzo: Utafiti wa Lishe (1992)

Ili tuweze kufanikisha malengo yaliyomo katika mpango wa "The National Programme of Action - NPA" kuhusiana na Uhai wa Mtoto na Maendeleo yake, kabla ya mwaka 2000, mkoa umebuni mikakati mbalimbali itakayotumika ikiwa ni pamoja na kutayarisha mfumo mzuri wa kuratibu utekelezaji, pamoja na kuandaa shughuli zitakazopelekea kufikia malengo hayo.

Kutokana na hali hiyo, majukumu ya jumla yatakayotekelezwa na viongozi wa mkoa ni kama ifuatavyo:

- Kuboresha elimu, mtazamo na ujuzi katika ngazi zote za jamii dhidi ya tatizo la utapiamlo, ili jamii wao wenyewe waanze kuchukua hatua thabiti kwa kutumia raslimali zao kuanzia vijijini.

- Kuanzisha mfumo usio tegemezi katika ngazi zote ambao utaiwezesha jamii kutambua matatizo pamoja na kuainisha

na kuchambua njia mbali mbali za kukabiliana na tatizo la utapiamlo.

- Kuwapa uwezo wananchi ili waweze kumudu kujiendeleza kielimu kwa faida yao wenyewe.

- Kuwapatia elimu ya afya ya msingi, usafi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wao wenyewe ili kuboresha maisha yao

- Kupunguza kiwango cha umaskini na ufukara uliyopo hadi kufikia ngazi itakayouwezesha umma kumudu kufikia malengo yaliyowekwa katika programu ya NPA.

- Kuboresha ulinzi wa watoto hasa kipindi cha matatizo.

- Kuhakikisha kuwa upo uratibu imara wa kufuatilia programu hii.

- Kuboresha afya za akina mama na watoto hasa katika nyanja za kinga, tiba na uzazi wa majira.

Kwa ujumla, uongozi wa mkoa umejitahidi kwa uwezo wake wote katika kukabiliana na tatizo hili. Watumishi wa "Huduma za akina mama na watoto (MCH) wa mkoa wameshiriki kikamilifu katika kuuhamasisha umma hadi kuwezesha vituo 191 vya kukarabati utapiamlo kuanzishwa mwaka 1995.

**JEDWALI LIV: HALI YA WATOTO WALIO ATHIRIWA NA UTAPIAMLO MKOANI DODOMA 1995**

| Wilaya | Vituo vya ukarabati | Watoto walioathirika na Utapiamlo | Vifo | Asilimia ya Vifo |
|---|---|---|---|---|
| Dodoma Mjini | 35 | 1744(3%) | 20 | 1 |
| Dodoma Vijijini | 63 | 242(0.3%) | 8 | 3 |
| Kondoa | 47 | 197(0.2%) | 10 | 5 |
| Mpwapwa | 46 | 225(0.2%) | 3 | 1 |
| | 191 | 2488(3.7%) | 41 | 2.5 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Mipango) Dodoma

### 4.2.2 Msambao na Upatikanaji wa Huduma za Afya

Serikali pamoja na watu binafsi wamesaidia sana kutua huduma ya afya kwa wananchi wa Dodoma katika kipindi cha miaka 28 iliyopita. Mtazamo umendelea kuwa ni kuimarisha afya za wananchi hasa watoto, na wanachi ambao hawana uwezo wa kulipia gharama za huduma hizo.

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo za mwaka 1968, mkoa wa Dodoma ulikuwa na vituo saba vya afya na zahanati 22. Ilipofika mwaka 1996, mkoa ulikuwa na hospitali sita, vituo 17 vya afya, na zahanati 200. Hospitali mbili kati ya hizo sita na zahanati 53 kati ya 2000 zilianzishwa na zinaendeshwa na watu binafsi

**JEDWALI LV: MGAWANYO WA HUDUMA ZA AFYA , 1968, 1978, 1988 NA 1995 MKOA WA DODOMA**

| Mwaka | Idadi ya Hospitali | Vito vya Afya | Zahanati |
|---|---|---|---|
| 1968 | Haihusiki | 7 | 22 |
| 1978 | 2 | 14 | 152 |
| 1988 | 5 | 17 | |
| 1995 | 6 | 17 | 200 |

Chanzo: Taarifa ya Afya ya Mkoa - 1996.

**JEDWALI LVI: MGAWANYO WA HUDUMA ZA AFYA KIWILAYA MKOA WA DODOMA 1996**

| Wilay | Hospitali | | | Vituo vya Afya | | | Zahanati | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Binafsi | Jumla | Serikali | Binafsi | Jumla | Serikali | Binafsi | Jumla |
| Dodoma Mjini | 2 | 1 | 3 | 3 | - | 3 | 21 | 28 | 49 |
| Dodoma | - | 1 | 1 | 6 | - | 6 | 52 | 4 | 56 |
| Vijijini | 1 | - | 1 | 4 | - | 4 | 39 | 10 | 49 |
| Mpwapwa | 1 | - | 1 | 4 | - | 4 | 39 | 11 | 50 |
| Kondoa | | | | | | | | | |
| Jumla | 4 | 2 | 6 | 17 | - | 17 | 147 | 53 | 200 |

Chanzo: Taarifa ya Afya ya Mkoa - 1995

**JEDWALI LVII: UWIANO WA HUDUMA ZA AFYA KIWILAYA, MKOANI DODOMA, 1994**

| Wilaya | Watu/Hospitali | Watu/Kituo cha Afya | Watu/Zahanati | Watu/Kitanda | Watu/Daktari Bingwa |
|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma (M) | 114,750 | 79,734 | 4,513 | 234 | 9,299 |
| Dodoma (V) | 398,000 | 69,433 | 8,679 | 973 | 42,752 |
| Kondoa | 383,400 | 100,425 | 8,369 | 1,717 | 127,143 |
| Mpwapwa | 382,000 | 100,200 | 9,776 | 1,797 | 76,557 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Wastani Kimkoa | 278,580 | 85,782 | 7,675 | 764 | 32,738 |
| Kiwango cha Kitaifa | 150,000 | 50,000 | 10,000 | 1,123 | 24,930 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Mipango)

### 4.2.3 Utaratibu wa Huduma za Afya

(i) Huduma za Afya katika ngazi ya Jamii:

Wahisani wengi ikiwa ni pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali, wanashirikiana na uongozi wa mkoa wa Dodoma katika kuimarisha vituo vya afya vya vijiji kwa kutoa mafunzo kwa "wahudumu wa afya wa vijiji. Watumishi hawa wa afya hufanya kazi kwa kujitolea ingawaje kuna kipindi hupewa posho na serikali za vijiji husika, na wahisani na mashirika mbalimbali yanayosaidia huduma hii.

Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 1985 na 1994 jumla ya wahudumu wa afya wa vijiji 619 walikuwa wamepatiwa mafunzo na serikali kwa kushirikiana na mashirika ya watu binafsi. Aidha vilikuwepo vituo 267 ambavyo havikuwepo kwenye programu pamoja na kliniki za muda. Pia, kulikuwepo na wakunga wa jadi 1191 ambao wanafanya kazi za ukunga kwa kusaidiana na wanavijiji wenyewe. Jedwali LVIII linaonyesha mgawanyo na msambao wa huduma za afya kiwilaya.

**JEDWALI LVIII: MGAWANYO WA HUDUMA ZA AFYA NGAZI YA JAMII, KIWILAYA MKOANI DODOMA, 1995**

| Wilaya | Wahudumu wa Afya wa Vijiji | Wakunga wa Jadi | Vituo vya mbali vinavyotembelewa | Kliniki zinazozungukwa kwa magari |
|---|---|---|---|---|
| Dodoma Mjini | 59 | 283 | 42 | 8 |
| Dodoma Vijijini | 271 | 846 | 64 | 21 |
| Kondoa | 99 | 194 | 106 | 16 |
| Mpwapwa | 190 | 357 | 55 | 9 |
| Jumla | 619 | 1191 | 267 | 54 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Mipango) Dodoma

(ii) **Zahanati:**

Hadi mwaka 1996 mkoa wa Dodoma ulikuwa na jumla ya zahanati 200, ambapo kati ya hizo, zahanati 147 ni za serikali na 53 ni za mashirika na watu binafsi. Kwa wastani, kila zahanati inahudumia watu 7,675. Kiwango hiki kinaridhisha kutokana na kwamba lengo la kitaifa ni zahanati moja kuhudumia wastani wa watu 5,000 hadi 10,000.

(iii) **Vituo vya Afya:**

Kituo cha afya kinajulikana kama hatua ya pili ya utoaji wa huduma ya afya katika mfululizo mzima wa utaratibu wa afya nchini. Hadi kufikia mwaka 1995, mkoa ulikuwa na jumla ya vituo 17 vya afya, vyote vikiwa ni mali ya halmashauri za wilaya. Kwa wastani, kila kituo cha afya

kinahudumia watu 85,782, na wastani wa watu 764 kwa kitanda.

Japokuwa karibu majengo yote ya vituo vya afya yako katika hali mbaya, serikali kwa kushirikiana na wahisani, mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile "World Vision, "KRDEP" na "BSF" wanayafanyia baadhi ya majengo hayo ukarabati hususan katika wilaya za Kondoa na Dodoma vijijini.

(iv) **Hospitali ya Mkoa na za Wilaya:**

Hospitali ya wilaya ni hatua ya tatu ya utoaji wa huduma ya afya, katika mfululizo mzima wa utoaji huduma ya afya nchini. Hospitali ya mkoa, kimsingi ndiyo hatua ya juu kabisa ya rufaa mkoani. Hadi mwaka 1966, mkoa ulikuwa na jumla ya hospitali sita.

Hospitali ya mkoa pamoja na za wilaya zina jumla ya vitanda 1909. Hospitali za wilaya za Kondoa na Mpwapwa, ambazo hapo awali zilikuwa na hali mbaya sana, zimekwisha fanyiwa ukarabati mkubwa na shirika la Kiitaliano lisilo la kiserikali (NGO) liitwalo CUAMN.

### 4.2.4 Huduma za Kinga

Mpango wa chanjo kwa watoto wote ulianzishwa na serikali kwa kushirikiana na shirika la msaada la Denmark (DANIDA), shirika la Kimataifa la kuhudumia watoto (UNICEF) na shirika la Afya la Dunia (WHO), ili kukabiliana na magonjwa sita yanayo wakabili

watoto, yaani upungufu wa damu, kifua kikuu, kifaduro, polio, dondakoo, tetanasi na ugonjwa wa kikohozi kikavu. Ilipofikia mwaka 1994/95 kiwango cha chanjo kwa watoto wote ilifikia asilimia 86.

**JEDWALI LIX: HATUA ILIYOFIKIWA YA CHANJO KWA WATOTO WOTE WACHANGA (Chini ya Mwaka Mmoja) KIWILAYA, 1994 - 1995**

| | Mwaka | Dodoma(M) | Dodoma (V) | Mpwapwa | Kondoa | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Matarajio | 1991 | 10309 | 15392 | 15678 | 15706 | 57075 |
| | 1995 | 10557 | 15762 | 16054 | 16083 | 58456 |
| Kifua Kikuu | 1994 | 8342 (81%) | 14952 (99%) | 15655 (99%) | 13662 (87%) | 52959 (93%0) |
| | 1995 | 9888 (94%) | 15447 (98%) | 16051 (99%) | 12388 (77%) | 53774 (92%) |
| Kifaduro | 1994 | 8808(85%) | 14572(95%) | 14255 (93%) | 12656 (81%) | 50291 (88%) |
| | 1995 | 9368 (89%) | 14972 (95%) | 15079 (93%) | 12476 (78%) | 51895 (89%) |
| Polio | 1994 | 8806 (85%) | 14560 (99%) | 14255 (93%) | 13702 (87%) | 51323 (89%) |
| | 1995 | 9368 (89%) | 14972 (95%) | 15079 (93%) | 12476 (78%) | 51895 (89%) |
| Surua | 1994 | 8384(81%) | 14220 (92%) | 14234 (91%) | 11529 (73%) | 48367 (85%) |
| | 1995 | 8804 (83%) | 14345 (91%) | 14934 (93%) | 10096 (63%) | 48179 (82%) |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Afya) Dodoma

**JEDWALI LX: HATUA ILIYOFIKIWA YA CHANJO KWA WATOTO CHINI YA MIAKA MITANO KIWILAYA, 1994 - 1995**

| | Mwaka | Dodoma (M) | Dodoma (V) | Mpwapwa | Kondoa | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Matarajio | 1994 | 51546 | 76961 | 78388 | 78528 | 285423 |
| | 1995 | 52783 | 78809 | 80270 | 80413 | 292275 |
| Walioandikishwa | 1994 | 48909 | 76733 | 71288 | 73432 | 268363 (95%) |
| | 1995 | 51010 | 74869 | 74884 | 69038 | 269861 (92%) |
| Kifua Kikuu | 1994 | 46910 | 76733 | 71288 | 73432 | 268363 (94%) |
| | 1995 | 51010 | 74869 | 74884 | 69098 | 269861 (92%) |
| Kifaduro | 1994 | 44776 | 69116 | 69373 | 67067 | 250332 (86%) |
| | 1995 | 49810 | 68564 | 72800 | 64582 | 255756 (88%) |
| Palio | 1994 | 44776 | 68220 | 69373 | 66869 | 249238 (87%) |
| | 1995 | 49810 | 68564 | 72800 | 64171 | 255343 (87%) |
| Surua | 1994 | 42136 | 67900 | 69300 | 68484 | 247820 (87%) |
| | 1995 | 50235 | 65849 | 72760 | 64315 | 253159 (86%) |
| Walioandikishwa | 1994 | 42136 | 67900 | 69300 | 66899 | 246205 (86%) |
| | 1995 | 49810 | 65849 | 72750 | 64171 | 252590 (86%) |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Afya) 1995

**JEDWALI LXI: HATUA ILIYOFIKIWA KATIKA CHANJO YA SURUA, 1994-1995, KIWILAYA**

| | Mwaka | Dodoma(M) | Dodoma(V) | Mpwapwa | Kondoa | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Tarajiwa | 1994<br><br>1995 | 51546<br><br>52783 | 76961<br><br>78806 | 78388<br><br>80270 | 78528<br><br>80413 | 285423<br><br>292272 |
| T.T.I | 1994<br><br>1995 | 48623(94%)<br><br>50345 (95%) | 54243 (70%)<br><br>66988 (85%) | 51232 (65%)<br><br>61613 (77%) | 66026 (84%)<br><br>67871 (84%) | 220134 (77%)<br><br>46817 (84%) |
| T.T.2 | 1994<br><br>1995 | 43016 (51%)<br><br>50110 (94%) | 43016 (56%)<br><br>50110 (94%) | 41519 (53%)<br><br>50455 (63%) | 43879 (56%)<br><br>51985 (65%) | 175042 (61%)<br><br>212445 (73%) |
| T.T.3 | 1994<br><br>1995 | 23601 (43%)<br><br>46500 (88%) | 23601 (31%)<br><br>40980 (52%) | 25598 (33%)<br><br>33944 (42%) | 14876 (19%)<br><br>19712 (25%) | 86461 (30%)<br><br>141136 (48%) |
| T.T.4 | 1994<br><br>1995 | 7095 (18%)<br><br>30202 (52%) | 7095 (9%)<br><br>24430 (21%) | 12642 (16%)<br><br>17532 (22%) | 4932 (6%)<br><br>7979 (10%) | 34061 (12%)<br><br>80143 (27%) |
| T.T.5 | 1994<br><br>1995 | 5200 (10%)<br><br>19116 (36%) | 1651 (2%)<br><br>11821 (15%) | 4751 (6%)<br><br>9393 (21%) | 3091 (4%)<br><br>1109 (1%) | 12711 (4%)<br><br>43421 (15%) |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Afya) - Dodoma

### 4.2.5 Matatizo yanayoikabili Sekta ya Afya

(a) **Upungufu wa wataalam wa Afya:**

Mkoa unakabiliwa na upungufu mkubwa wa wataalam wa afya. Kwa mfano katika mwaka 1995, mkoa ulikuwa na madaktari bingwa watatu wakati mahitaji halisi yalikuwa 12. Katika kipindi hicho hicho, mkoa ulikuwa na upungufu wa manesi na wakunga 252. Aidha hospitali nyingi zimeendelea kufanya kazi zikiwa na idadi ndogo ya wataalam hawa.

**(b) Mahitaji na Vifaa:**

Vifaa na mahitaji muhimu yaliyopo katika hospitali ya mkoa ni duni na havifanyi kazi. Katika hospitali za wilaya, upungufu huu haujitokezi mara kwa mara kutokana na msaada maalum wa vifaa kutoka umoja wa nchi za Ulaya (European Community Assistance).

**(c) Upungufu wa Fedha:**

Ufinyu wa bajeti dhidi ya sekta ya afya umekuwa ni kikwazo kikubwa katika uendeshaji wa hospitali zilizopo mkoani.

## 4.3 Sekta ya Maji Safi na Taka

Sera ya serikali ya maji ni kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wote ifikapo mwaka 2002. Ili kufanikisha malengo haya, uongozi wa mkoa umeweka mikakati ifuatayo:-

- Kuimarisha ulinzi wa miradi ya maji pamoja na vyanzo vya maji

- Kusaidia mashirika pamoja na watu binafsi kuwa na miradi yao ya maji

- Matumizi ya teknolojia inayofaa na ile yenye gharama nafuu, ili kuhakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha kwa wote

- Uhusishaji wa jamii katika kuainisha matatizo, kupanga kutekeleza na kutunza miradi ya maji.

### 4.3.1 Hali Halisi ilivyo:

Hali mbaya ya ukame, pamoja na upungufu wa vyanzo vya maji vinavyoaminika kama vile mito ya kudumu, maziwa, umepelekea uongozi wa mkoa kutafuta teknolojia nyingine ya upatikanaji wa maji. Hata hivyo, baadhi ya teknolojia zinazotumika kama vile uchimbaji wa visima virefu, visima vifupi, pamoja na mabwawa, imepunguza kwa kiwango kikubwa tatizo la upatikanaji wa maji kwa ajili ya watu na mifugo. Mnamo mwaka 1970, wastani wa asilimia 18 ya watu wote mkoani Dodoma walikuwa wanapata maji safi na salama. Takwimu za mwaka 1978 zinaonyesha kuwa ni asilimia 54 tu ya watu 967,650 wa Dodoma walipata maji safi na salama. Katika mwaka 1988 asilimia 64 ya watu 1,237,819 wa mkoa wa Dodoma walipata maji safi na salama. Ilipofikia mwisho wa mwaka 1996, mkoa ulikuwa na jumla ya miradi 334 ya maji yenye uwezo wa kuhudumia watu wote wa mkoa

wa Dodoma iwapo miradi hiyo ingekuwa inafanya kazi kikamilifu.

Aidha, kutokana na matatizo mbali mbali, wastani wa asilimia 40 ya miradi 334 ya maji haifanyi kazi. Kwa sababu hiyo, idadi ya watu ambao wanatarajiwa kupata maji safi na salama inawezekana ikawa ndogo. Wastani wa asilimia 50 ya watu wanaopata maji safi na salama kama takwimu zinavyoonyesha henda usiwe sahihi kipindi cha kiangazi na inawezekana kuwa sahihi majira ya mvua, kwani miradi inayotegemea maji ya mvua hufanya kazi bila matatizo yoyote.

**JEDWALI LXII: MSAMBAO WA MAJI KIWILAYA 1996**

| Wilaya | Sensa ya 1978 | | Sensa ya 1988 | | Maoteo ya 1996 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya watu | Asilimia wanaopata maji | Idadi ya watu | Asilimia wanaopata maji | Idadi ya watu | Asilimia wanaopata maji |
| Dodoma (M). | 156,862 | 18 | 203,333 | 65 | 265,935 | 76.7 |
| Dodoma (V). | 274,514 | 88 | 353,473 | 45 | 394,065 | 53.4 |
| Kondoa | 275,082 | 83 | 340,554 | 51 | 402,370 | 78.9 |
| Mpwapwa /Kongwa | 261,251 | 27 | 339,954 | 62 | 401,346 | 68.8 |
| Jumla | 967,649 | 54 | 1,237,819 | 64 | 1,463,716 | 70.2 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Maji) Dodoma

**JEDWALI LXIII: MSAMBAO WA MAJI KIWILAYA - MKOA WA DODOMA, 1996**

| Maelezo | DODOMA (M) | DODOMA (V) | KONDOA | MPWA-PWA | KONG-WA | Jumla Kimkoa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya Watu | 265,935 | 394,065 | 402,370 | 250,946 | 150,400 | 1,463,716 |
| Idadi ya miradi ya maji inayofanya kazi | 36 | 107 | 92 | 40 | 37 | 312 |
| Miradi isiyofanya kazi | 27 | 73 | 76 | 31 | 32 | 239 |
| Idadi ya watu wapatao maji | 9 | 34 | 16 | 9 | 5 | 73 |
| Idadi ya watu kwenye miradi isiyofanya kazi | 203,915 | 210,430 | 317,440 | 172,746 | 122,898 | 1,027,429 |
| Vijiji visivyo na vyanzo vya maji kabisa | 38,990 | 101,326 | 50,011 | 25,635 | 14,432 | 230,394 |
| Asilimia ya watu wapatao maji safi | 6 | 16 | 43 | 10 | 7 | 82 |
| Asilimia ya Wastani | 76.7 | 53.4 | 78.9 | 68 | 81.7 | 70.2 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Maji - Dodoma

## Wahisani Wanaosaidia Sekta ya Maji

Katika harakati za kuboresha hali ya upatikanaji wa maji safi na salama, uongozi wa mkoa pamoja na serikali zimefanya juhudi za kutafuta misaada ya fedha na ufundi kutoka kwa wahisani mbali mbali. Shirika la Uingereza linalojihusisha na sekta ya maji lijulikanalo kama "The British Water Aid" ni shirika la lwanza kwa utoaji wa misaada ya kusaidia upatikanaji wa maji mkoani Dodoma likifuatiwa na shirika la Uholanzi liitwalo "The Royal Volunteers International Association (LVIA)" na shirika la Ubeligiji liitwalo "Belgiun Survival Fund (BSF)".

**JEDWALI LXIV: HALI HALISI YA UPATIKANAJI WA MAJI NA TEKNOLOJIA ILIYOPO KIWILAYA, MKOA WA DODOMA, 1996**

| Teknolojia | Wilaya | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | Dodoma (M) | Dodoma (V) | Kondoa | Mpwapwa | |
| **Visima vifupi:** | | | | | |
| - Vinafanya kazi | 20 | 13 | - | 12 | 45 |
| - Vimeharibika | 2 | 47 | - | 7 | 56 |
| Jumla | 22 | 60 | - | 19 | 101 |
| **Visima virefu:** | | | | | |
| - Vinafanya kazi | 29 | 60 | 18 | 12 | 119 |
| - Vimeharibika | 6 | 29 | 2 | 3 | 40 |
| Jumla | 35 | 89 | 20 | 15 | 159 |
| **Maji ya mtelemko:** | | | | | |
| - Inafanya kazi | 2 | 7 | 4 | 17 | 30 |
| - Imeharibika | - | - | - | 6 | 6 |
| Jumla | 2 | 7 | 4 | 23 | 36 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mabwawa:** | | | | | |
| - Yanafanya kazi | 2 | 23 | 30 | 1 | 56 |
| - Yameharibika | - | - | - | - | - |
| Jumla | 2 | 23 | 30 | 1 | 56 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Maji - Dodoma

### 4.3.2 Huduma ya Maji Vijijini

Vyanzo vingi vya maji mkoani Dodoma vinatokana na vyanzo vya jadi kama vile visima, mabwawa n.k. Teknolojia za kisasa kama vile uvunaji maji ya mvua na uchimbaji visima umeanza kutumika mkoani Dodoma siku za karibuni.

Kati ya miradi 334 ya maji iliyopo (1996), wastani wa asilimia 75 ya miradi hiyo ipo maeneo ya vijijini. Hata hivyo asilimia kubwa ya miradi hii vijijini haifanyi kazi. Kwa kutumia maoteo ya idadi ya watu wa mkoa wa Dodoma kwa mwaka 1996, (watu 1,360,980) ni watu 571,611 ambao wanapata maji safi na salama. Idadi hii ya watu ni wenye kupata maji safi na salama ni asilimia 42 ya watu wote. Kwa upande mwingine kati ya vijiji 422 vilivyopo mkoani, ni vijiji 226 tu ndivyo vyenye maji safi na salama.

Upungufu wa maji vijijini ni mkubwa zaidi hasa kipindi cha kiangazi. Idadi kubwa ya watu waishio vijijini bado hutegemea zaidi vyanzo vya maji vya visima vifupi ambavyo vipo wazi kwa ajili ya matumizi yao na mifugo. Kutokana na hali hiyo watu wengi hasa wanawake hulazimika kutembea kilomita 5 - 8 hasa kipindi cha kiangazi kutafuta maji. Aidha vyanzo vingi vya asili vya maji sio salama na maji yake sio ya uhakika kwa sababu:

(i) Vyanzo vingi vya maji hukauka wakati wa ukame.

(ii) Vyanzo hivi vya maji mara nyingi viko mbali na makazi ya wana vijijiji

(iii) Ubora wa maji haya hasa katika kipindi cha ukame sio mazuri kwa matumizi ya binadamu.

(iv) Vyanzo vya maji vya asili havijahifadhiwa vya kutosha na kwa sababu hiyo huchafuliwa kirahisi na mifugo na wanyama pori.

Chanzo cha maji yenye uhakika kilichopo ambacho kingeweza kutosheleza mahitaji ya vijiji vingi ni bwawa la Mtera. Vyanzo vingine ni pamoja na visima virefu, visima vya kati na mabwawa ya kuchimbwa kama vile bwawa la Hombolo. Teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua ni njia ingine ambayo itapunguza upungufu wa maji mkoani Dodoma.

**JEDWALI LXV: UPATIKANAJI WA MAJI VIJIJINI, KIWILAYA, MKOA WA DODOMA, 1996**

| Wilaya | Jumla ya Idadi ya Vijiji | Watu wa Vijijini | Watu wapatao maji Vijijini % | Asilimia ya Vijiji vipatavyo maji |
|---|---|---|---|---|
| Dodoma (M) | 31 | 224,110 | 65.3 | 64.5 |
| Dodoma (V) | 131 | 388,650 | 45.0 | 57.25 |
| Kondoa | 154 | 374,440 | 51.58 | 46.75 |
| Mpwapwa/Kongwa | 116 | 373,780 | 62.3 | 69.83 |
| Jumla | 422 | 1,360,980 | 50.08 | 59.58 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Maji) - Dodoma

Jedwali LXV linaonyesha kwamba iwapo miradi yote ya maji 237 iliyopo vijijini ingefanya kazi kwa asilimia 50, watu waishio vijijini kama asilimia 59.5 wangepata maji safi na salama katika umbali wa mita 400.

Serikali kwa kushirikiana na wahisani mbali mbali na wananchi wanatekeleza mpango mahususi wa kukarabati miradi yote iliyoharibika au kuchakaa. Baadhi ya mbinu zilizobuniwa na mkoa wa Dodoma ili kuhakikisha kuwa miradi ya maji inayojengwa vijijini inadumu na haiwi tegemezi ni pamoja na:

(i) **Kuchangia Gharama:**

Kijiji chochote ambacho wananchi wake tayari kupatiwa mradi wa maji safi na salama wanatakiwa kuunda kamati ya maji na mfuko wa maji wa kijiji. Kwa vigezo hivi, serikali 94 za vijiji zilianzisha kamati pamoja na mifuko ya maji mwaka 1993/94. Kufikia mwaka 1995, jumla ya mifuko 225 ya maji ya vijiji ilikuwa imeanzishwa, kama jedwali LXVI linavyoonyesha. Kwa takwimu hizo (1996) wilaya ya Kondoa ilikuwa ikiongoza kwa kuwa na idadi ya vijiji 90 vyenye mifuko ya maji na kiwango cha fedha Tshs.16.5m.

**JEDWALI LXVI: IDADI YA VIJIJI VYENYE MIFUKO YA MAJI NA VIWANGO VYAKE, KIWILAYA MKOA WA DODOMA, (1993-1995) TSHS. 000'**

| Wilaya | Idadi ya Vijiji Vilivyoanzisha Mifuko ya Maji | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1993 | Kiasi kilichopo | 1994 | Kiasi kilichopo | 1995 | Kiasi kilichopo |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma (V) | 30 | 1,557 | 56 | 4,763 | 66 | 14,353 |
| Dodoma (V) | 19 | 380 | 26 | 1,520 | 28 | 2,023 |
| Kondoa | 27 | 3,412 | 42 | 7,128 | 90 | 16,514 |
| Mpwapwa/Kongwa | 18 | 4,786 | 39 | 9,212 | 41 | 4,528 |
| Jumla | 94 | 10,135 | 163 | 22,623 | 225 | 37,418 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Maji) - Dodoma

(ii) **Umilikaji Mradi:**

Mbinu nyingine iliyotumika ni serikali za vijiji kumiliki miradi yote ya maji. Kwa hali hiyo, jukumu la kugharamia ukarabati, matengenezo, na ulinzi wa vyanzo vya maji dhidi ya matumizi yasiofaa, wizi au uchafuzi wa mazingira ni majukumu ya serikali ya vijiji au wananchi wenyewe.

(iii) **Miradi Mipya:**

Mikakati ya uanzishaji wa miradi mipya ya maji inalenga kuona kwanza msukumo unatoka kwa wananchi wenyewe na wananchi wanatakiwa kushiriki kikamilifu katika kukarabati, kuendesha na kufanya matengenezo punde miradi hii inapoharibika.

## 4.3.3 HUDUMA ZA MAJI MIJINI

**JEDWALI LXVII: HALI YA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MAJI YA WILAYA MKOANI DODOMA, 1995**

| Wilaya | Mahitaji ya Maji Mita za Ujazo kwa siku | Upatikanaji wa Maji-Mita za Ujazo kwa siku | Uwezo wa uzalishaji maji uliyopo kwa siku | Asilimia ya usambazaji maji |
|---|---|---|---|---|
| Dodoma Makao Makuu | 47,670 | 33,140 | 34,8 | 69.3 |
| Kondoa | 2,310 | 2,640 | 3,3 | 100 |
| Mpwapwa | 4,010 | 1,864 | 2,5 | 46.5 |
| Kongwa | 1,880 | 219 | 2,926 | 11.6 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Maji) - Dodoma

(i) **Huduma ya Maji - Mji Mkuu Dodoma**

Vyanzo vya maji kwa ajili ya Mji Mkuu - Dodoma ni pamoja na mabwawa mawili ya Makalama na Biringi, yakisaidiwa na visima virefu vilivyopo katika bonde la Makutopora. Hata hivyo maji yanayotokana na vyanzo hivi hayakidhi mahitaji halisi ya wakazi wa Mji Mkuu, wapatao 245,000 (1995). Vyanzo vyote vitatu vina uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 33,140 za maji kwa siku, kiwango ambacho ni asilimia 69.3 ya mahitaji ya maji, ambayo ni mita za ujazo 47,670 za maji kwa siku.
Ongezeko kubwa la watu wanaoingia kutoka vijijini, kwa ajili ya kutafuta kazi pamoja na mahitaji ya maji kwa ajili ya viwanda vichache vilivyopo, kunaongeza upungufu wa mahitaji halisi ya maji mjini Dodoma.

(ii) **Huduma za Maji - Mji wa Kondoa**

Chanzo cha maji kwa ajili ya mji wa Kondoa kinatokana na chemchem iliyopo yenye uwezo wa kuzalisha mita za

ujazo 2,340 za maji kwa siku, ikilinganishwa na mahitaji ya mita za ujazo 2,940 za maji kwa siku. Idadi ya watu wa mji wa Kondoa kwa mwaka 1996, ni 29,964 na kwa mwaka 2002 watakuwa 44,583. Aidha ikilinganishwa na idadi ya watu 21,181 sensa ya mwaka 1988 ni dhahiri kwamba ongezeko la watu kwa asilimia 5 kwa mwaka litaathiri sana huduma hii ya maji.

(iii) **Huduma za Maji - Mji wa Mpwapwa**

Mji wa Mpwapwa ambao ni makao makuu ya wilaya ya Mpwapwa, ni mji wa pili kwa ukubwa mkoani Dodoma, baada ya Mji Mkuu - Dodoma. Mji wa Mpwapwa unaokadiriwa kuwa na watu wapatao 40,162 (1996) na unapata maji kutoka chemchem za Mayawila na VIC, pamoja na visima virefu viwili ambapo vyanzo vyote vina uwezo wa kutoa mita za ujazo 1,864 za maji kwa siku. Visima virefu viwili vimeongezwa na vina uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo 648 kwa siku. Hata hivyo mji wa Mpwapwa bado una upungufu wa mita za ujazo 1,498 za maji kwa siku, au sawa na asilimia 53.5 ya mahitaji halisi ya maji.

(iv) **Huduma za Maji - Mji wa Kongwa:**

Wilaya ya Kongwa ambayo awali ilikuwa ni sehemu ya wilaya ya Mpwapwa ilianzishwa rasmi mwaka 1995, na mji wa Kongwa ndiyo makao makuu ya wilya hiyo. Vyanzo vikuu vya maji katika mji wa Kongwa ni visima

virefu vitatu vilivyopo mjini Kongwa pamoja na chemchem itwayo Saraga. Vianzo hivi hutoa mita za ujazo 219 za maji kwa siku kwa ajili ya watu wapatao 17,683 (1996). Hata hivyo, mji wa Kongwa una upungufu wa maji kwani ni asilimia 15 tu ya idadi ya watu wote wenye uhakika wa kupata maji.

# SURA YA TANO

## 5.0: SEKTA ZA UZALISHAJI:

## 5.1: MAENDELEO YA KILIMO:

### 5.1.1 Hali Ilivyo:.

Kilimo mkoani Dodoma ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa mkoa. Kilimo pamoja na shughuli za mifugo huchangia kiwango kikubwa sana cha uchumi wa mkoa. Sekta ndogo zingine kama vile viwanda, madini, misitu, nyuki na uvuvi huchangia kiwango kidogo sana cha uchumi wa mkoa.

Hata hivyo, hali ya hewa isiyo nzuri na udongo vimeathiri sana kilimo mkoa wa Dodoma na uzalishaji wa mazao kwa eneo. Matatizo hayo pamoja na mifugo mingi iliyopo na kilimo cha kuhamahama, vimesababisha mmomonyoko mkubwa wa ardhi, na uharibifu mkubwa wa mazingira.

### 5.1.2 Ardhi inayofaa kwa kilimo:

Kwa mujibu wa taarifa ya mkoa ya mwaka 1993 inayohusu maendeleo ya kilimo, jumla ya eneo linalolimwa ni asilimia 14.3 ya eneo lote linalofaa kwa kilimo. Aidha, asilimia 70 ya eneo lote la mkoa (yaani hekta 2,902,390) linafaa kwa kilimo, ambapo hekta 600,000 (au 20% linalofaa kwa kilimo) zinalimwa.

Taarifa ya mkoa inabaini kuwa jumla ya hekta 310,473 zinapandwa mazao ya chakula na jumla ya hekta 269,559 zinapandwa mazao ya biashara. Kwa kuwa siyo eneo lote lifaalo kwa kilimo linalimwa, mkoa unayo nafasi ya kupanua shughuli za kilimo. Kwa mfano, lipo eneo kubwa linalofaa kwa kilimo kusini magharibi ya mkoa sehemu za Mlowa, Mpwayungu, na Usuwanga ambayo yana wastani wa mvua wa milimita 650 kwa mwaka. Eneo hili lina rutuba lakini halilimwi. Hata hivyo tatizo kubwa katika eneo hili ni mbung'o wengi. Yapo pia maeneo makubwa wilayani Kongwa na Kondoa yenye mbung'o wengi, na yana rutuba ambayo inafaa kwa upanuzi wa kilimo. Aidha, mbali na maeneo hayo, yapo pia maeneo matupu yenye mvua kidogo karibu wilaya zote ambayo yanafaa kwa kilimo cha mazao yanayostamili ukame.

### 5.1.3 Uzalishaji wa Mazao:

Uzalishaji wa mazao ni shughuli inayofanyika katika wilaya zote kulingana na aina ya mazao. Hata hivyo, kilimo cha mazao karibu yote kinafanyika zaidi katika maeneo yenye rutuba na mvua za kutosha hususan katika wilayani za Mpwapwa, Kongwa, Kondoa na sehemu za magharibi ya wilaya ya Dodoma vijijini. Hata hivyo,

mazao yanayostahimili ukame kama vile mtama, uwele hulimwa katika maeneo yote mkoani. Wilaya ya Dodoma vijijini ndiyo inayoongoza kwa kilimo cha mazao yanayostahimili ukame.

Mazao mengine yanayolimwa mkoani Dodoma ni pamoja na mahindi, mpunga, maharage, mbegu za mafuta - kama vile karanga, ufuta, nyonyo n.k. Kilimo cha viazi vitamu, vitunguu, nyanya pamoja na mboga mboga matunda pia hulimwa.

### 5.1.4 Mazao ya Chakula:

(i) **Mahindi**:

Kwa ujumla, zao la mahindi hulimwa katika maeneo yote mkoani, lakini hustawi zaidi katika maeneo ya kusini na mashariki ya wilaya ya Kongwa, hasa maeneo ya Mkoka, wilaya ya Mpwapwa, mashariki ya wilaya ya Kondoa Tarafa ya Bereko na Magharibi ya Wilaya ya Dodoma vijijini. Maeneo yote haya yana rutuba, mvua za kutosha na udongo mzuri. Licha ya hali ya hewa kutokuwa nzuri, uzalishaji wa mahindi umeendelea kuongezeka tokea miaka ya 1980. Inasemekana kwamba; juhudi za kupanua na kukuza zao la mahindi kupitia shirika la Sasakawa Global 200" zimechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la uzalishaji wa mahindi mkoani Dodoma. Matokeo ya mradi ni ongezeko la uzalishaji kutoka magunia matatu hadi manne kwa ekari mwaka 1980, hadi kufikia magunia 20 - 30 kwa ekari. Jedwali LXVIII linaonyesha kuwa katika misimu mitatu mfululizo mkoa uliweza kuzalisha ziada ya mahindi ya wastani wa tani 59,000 kwa mwaka.

**JEDWALI LXVIII: UZALISHAJI WA MAHINDI MKOANI DODOMA 1990/1991 - 1994/1995**

| Zao | | 1990/91 | 1991/92 | 1992/93 | 1993/94 | 1994/95 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | Hekta | 40,183 | 42,505 | 62,994 | 50,634 | 88,883 |
| | Tani | 33,845 | 42,795 | 60,445 | 45,695 | 71,992 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Kilimo) Dodoma

Ukiacha miaka ya ukame, mkoa wa Dodoma unazalisha ziada ya mahindi kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, uzalishaji wa mahindi kwa mwaka mkoani Dodoma hauwezi kulinganishwa na uzalishaji wa mahindi katika mikoa maarufu kama vile Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Iringa na Morogoro. Katika kipindi cha ukame, mkoa wa Dodoma hupata mahindi kutoka mikoa ya jirani. Jedwali LXIX linajaribu kulinganisha uzalishaji wa mahindi kati ya mkoa wa Dodoma na mikoa iliyobobea.

**JEDWALI LXIX: UZALISHAJI WA MAHINDI MKOANI DODOMA UKILINGANISHWA NA MIKOA ILIYOBOBEA, NA ASILIMIA ZA UCHANGIAJI KITAIFA 1991/1992**

| Mikoa | Eneo linalolimwa(He) | Wastani (Tani) | Wastani Tani/Hekta | Asilimia Kitaifa |
|---|---|---|---|---|
| **Dodoma** | 34,860 | 21,200 | 0.61 | 0.9 |
| Iringa | 309,130 | 464,920 | 1.50 | 21.0 |
| Mbeya | 197,150 | 287,680 | 1.46 | 13.0 |
| Ruvuma | 122,180 | 230,780 | 1.89 | 10.0 |
| Rukwa | 121,540 | 217,170 | 1.79 | 10.0 |
| Mikoa mingine | | 1,255,781 | | 45.1 |
| Jumla ya Uzalishaji | | 2,260,361 | | |

Chanzo: Wizara ya Kilimo na Ushirika
(Takwimu 1996/87 - 1992/1993)

## ii) Mtama na Uwele:

Mtama na uwele ni mazao yanayostahimili ukame ambayo hulimwa kila mahali mkoani Dodoma, na ni chakula kikuu kwa watu walio wengi vijijini. Mazao haya hustawi vizuri

katika uwanda wa chini na hasa maeneo yenye mvua zisizoaminika, hali ambayo ndiyo inayotawala sehemu kubwa ya mkoa. Ulezi hulimwa katika wilaya ya Kondoa pekee kwa ajili ya utayarishaji pombe za kienyeji na ziada huuzwa ndani na nje ya mkoa.

Aidha mkoa wa Dodoma ni maarufu kwa uzalishaji wa mazao ya mtama na uwele. Kati ya tani 10,456 zilizozalishwa msimu 1991/92 na tani 14,744 msimu 1992/93 nchini kote, mkoa wa Dodoma ulichangia asilimia 75. Takwimu za 1991/92 zinaonyesha pia kuwa mkoa ulichangia asilimia 41.4 ya uwele uliyozalishwa nchini kote, kama jedwali LXXX linavyoonyesha.

**JEDWALI LXXX: UZALISHAJI WA MTAMA NA UWELE MKOA WA DODOMA IKILINGANISHWA NA BAADHI YA MIKOA - 1991/1992**

| Mkoa | MSIMU WA KILIMO WA 1991/1992 | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Mtama | Asilimia | Uwele | Asilimia |
| Dodoma | 124,350 | 21.2 | 108,750 | 41.4 |
| Singida | 105,500 | 18.0 | 57,980 | 22.1 |
| Rukwa | 7,070 | 1.2 | 34,580 | 13.2 |
| Shinyanga | 87,410 | 14.9 | 15,980 | 6.1 |
| Mara | 34,160 | 5.8 | 11,710 | 4.5 |
| Mingine | 228,394 | 38.9 | 68,060 | 25.9 |
| Kitaifa | 587,130 | 100 | 262,780 | 100 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo na Ushirika

Jedwali LXXXI linabaini kwamba wilaya za Kondoa, Mpwapwa na Kongwa zinazalisha kwa wingi zao la mahindi. Asilimia 68 ya mahindi yote yaliyozalishwa katika msimu wa kilimo wa mwaka 1992/93 mkoani yalitoka wilaya za Kondoa, na Mpwapwa. Kwa


upande mwingine wilaya ya Dodoma vijijini, katika msimu huo huo ilizalisha asilimia 47 ya mtama wote uliozalishwa mkoani Dodoma.

**JEDWALI LXXXI: UZALISHAJI WA MAZAO MAKUU YA CHAKULA MKOANI, KIWILAYA, 1993/94**


| Wilaya | Mahindi | | Uwele | | Mtama | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hekta | Tani | Hekta | Tani | Hekta | Tani |
| Kondoa | 22047 | 14041 | 47350 | 32652 | 9458 | 5907 |
| Mpwapwa | 15025 | 8340 | 9037 | 4512 | 38342 | 10001 |
| Dodoma (M) | 6084 | 3864 | 18250 | 21900 | 8250 | 2600 |
| Dodoma (V) | 7044 | 6649 | 50568 | 50568 | 51350 | 16802 |
| Jumla | 60200 | 32900 | 128824 | 109638 | 84748 | 35800 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Kilimo) Dodoma


**Kielelezo 20: Uzalishaji wa mahindi, Mkoa wa Dodoma, Kiwilaya, 1993/94**




**Kielelezo 21: Uzalishaji wa uwele, Mkoa wa Dodoma, Kiwilaya, 1993/94**



**Kielelezo 22: Uzalishaji wa mtama, Mkoa wa Dodoma, Kiwilaya, 1993/94**




iii) **Mpunga:**

Mpunga hulimwa katika mashamba madogodogo mengi yaliyotawanyika na, ni zao linaloendelea kupata umaarufu mkoani Dodoma. Maeneo maarufu kwa kilimo cha mpunga yako wilaya ya Dodoma vijijini na hasa katika bonde la ufa. Mpunga unalimwa vile vile katika wilaya za Kondoa na Mpwapwa katika mashamba madogo madogo. Jedwali LXXXII linaonyesha kuwa uzalishaji wa mpunga mkoani uliongezeka kwa asilimia 115 yaani kutoka tani 1,306 msimu wa mwaka 1990/91 hadi tani 2,808 msimu wa mwaka 1994/95. Zao hili hulimwa na wakulima wadogo wadogo ambao lengo lao ni kupata

chakula cha kutosheleza kaya zao, na kuuza ziada inapopatikana .

**JEDWALI LXXXII: UZALISHAJI WA MAZAO MBALI MBALI MKOANI DODOMA, 1990/91 - 1994/95**

| **Mahindi** | **1990/91** | **1991/92** | **1992/93** | **1993/94** | **1994/95** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. Hekta zilizolimwa | 57800 | 34860 | 50200 | 50634 | 86142 |
| 2. Mavuno Tani | 54000 | 21200 | 32900 | 92547 | 163091 |
| 3. Wastani wa uzalishaji wa Hekta (Tani) | 0.93 | 0.61 | 0.66 | 1.82 | 1.89 |
| 4. Thamani Tshs. | 627104 | 1283850 | 1813650 | 1776410 | 480273 |
| **Uwele:** | | | | | |
| 1. Hekta zilizolimwa | 181200 | 144490 | 107600 | 67225 | 178399 |
| 2. Mavuno Tani | 121500 | 124350 | 35800 | 82837 | 267881 |
| 3. Wastani wa uzalishaji wa Hekta (Tani) | 0.67 | 0.86 | 0.33 | 1.23 | 1.50 |
| 4. Thamani Tshs. | 492200 | 508920 | 1979700 | 2485110 | 8036430 |
| **Mtama:** | | | | | |
| 1. Hekta zilizolimwa | 73597 | 132960 | 128824 | 113983 | 133597 |
| 2. Mavuno Tani | 66255 | 108750 | 109638 | 119197 | 138245 |
| 3. Wastani wa uzalishaji wa Hekta (Tani) | 0.90 | 0.82 | 0.85 | 0.95 | 1.03 |
| 4. Thamani Tshs. | 530040 | 831000 | 3289140 | 3575910 | 4144350 |
| **Mpunga:** | | | | | |
| 1. Hekta zilizolimwa | 667 | 1075 | 862 | 1330 | 1440 |
| 2. Mavuno Tani | 1306 | 1877 | 1506 | 3714 | 2808 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 3. Wastani wa uzalishaji wa Hekta (Tani) | 2.0 | 1.75 | 1.74 | 2.8 | 2.0 |
| 4. Thamani Tshs. | 33956 | 58538 | 47288 | 116620 | 88171 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Kilimo) - Dodoma

### 5.1.5 Mbegu za Mafuta:

(i) **Karanga:**

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, mkoa wa Dodoma ulikuwa miongoni mwa mikoa iliyokuwa inaongoza kwa uzalishaji wa mbegu za mafuta katika miaka ya 1950 na 1960. Hata hivyo kutokana na mabadiliko ya bei, umuhimu wa uzalishaji na mabadiliko ya hali ya hewa, uzalishaji umeendelea kushuka mwaka hadi mwaka. Wakat zao la karanga uzalishaji wake umeongezeka, (kwa mfano kutoka tani 8,040 msimu wa mwaka 1990/91 hadi tani 30,036 msimu wa mwaka 1994/95) uzalishaji wa mazao mengine uliendelea kushuka. Aidha wilaya za Kongwa na Mpwapwa zinaongoza katika uzalishaji wa karanga. Kwa mfano katika msimu wa 1992/93, kati ya tani 20,000 za karanga zilizozalishwa mkoani, asilimia 58.3 zilizalishwa katika wilaza za Mpwapwa na Kongwa.

(ii) **Ufuta:**

Zao la ufuta ambalo zamani lilikuwa ni zao muhimu mkoani katika miaka ya 1950, hivi sasa linalimwa katika vijiji vichache tu. Katika msimu wa kilimo wa miaka 1992/93, 1993/94, na 1994/95 mkoa uliuza tani 1,634, tani 1.412 na tani 1,149 za ufuta kama takwimu na miaka ilivyofuatana.

(iii) **Alizeti:**

Zao la alizeti linalimwa kwa wingi kwa ajili ya biashara na ni wakulima wachache sana wanaobakisha sehemu ya mavuno yao kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Hivi sasa, ipo idadi ya watu na vikundi vinavyojishughulisha na ukamuaji wa mafuta kutokana na karanga na alizeti. Jedwali LXXXIII linaonyesha kuwa uzalishaji wa alizeti katika miaka ya 1990/91 hadi 1995/96 ulidumaa. Soko kubwa la alizeti ni mikoa ya Morogoro na Dar es Salaam. Mapande ya mabaki ya alizeti zilizokamuliwa huuzwa ndani ya mkoa kwa ajili ya chakula cha mifugo.

(iv) **Nyonyo:**

Uzalishaji wa nyonyo nao pia unadidimia mkoani. Uzalishaji kwa mfano ulipungua kutoka tani 679 msimu wa kilimo wa 1990/91 hadi kufikia tani 112 msimu 1995/96.

**JEDWALI LXXXIII: UZALISHAJI WA MBEGU ZA MAFUTA MKOANI, MSIMU 1990/91 - 1995/96**

| MAZAO | MIAKA YA FEDHA | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1990/91 | 1991/92 | 1992/93 | 1993/94 | 1994/95 | 1995/96 |
| Karanga: | | | | | | |
| Hekta | 19144 | 24975 | 44900 | 49183 | 50613 | 59186 |
| Tani | 8040 | 9581 | 20048 | 23057 | 24014 | 30036 |
| Alizeti: | | | | | | |
| Hekta | 29053 | 5329 | 25522 | 23209 | 20758 | 19822 |
| Tani | 14991 | 2751 | 10915 | 7507 | 14706 | 10355 |
| Ufuta: | 279 | 737 | 2001 | 3891 | 3501 | 2671 |
| Hekta. | 117 | 310 | 800 | 1634 | 1412 | 1149 |
| Tani: | | | | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Nyonyo:<br>Hekta<br>tani | 1475<br>679 | 1258<br>551 | 1366<br>750 | 668<br>604 | 670<br>335 | 626<br>112 |


Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Kilimo Dodoma

**JEDWALI LXXXIV: UZALISHAJI WA MBEGU ZA MAFUTA MKOA WA DODOMA, KIWILAYA 1992/93.**


| Wilaya | Mazao | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Karanga | Asilimia | Alizeti | Asilimia | Nyonyo |
| Kondoa | 2,606 | 12.7 | 3,070 | 27.6 | - |
| Mpwapwa | 11,628 | 58.3 | 2,953 | 27.3 | - |
| Dodoma (M) | 1,604 | 7.7 | 89 | 0.8 | 70 |
| Dodoma (V) | 4,210 | 21.3 | 4,803 | 44.3 | 1534 |
| Jumla | 20,048 | 100 | 10,915 | 100 | 604 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Kilimo) Dodoma

**Kielelezo 23: Uzalishaji wa karanga, Mkoa wa Dodoma, Kiwilaya, 1992/93**



**Kielelezo 24: Uzalishaji wa alizeti, Mkoa wa Dodoma, Kiwilaya, 1992/93**




## 5.1.6 Mazao mengine

### (i) Aina ya Mikunde:

Maharage, mbaazi na kunde hulimwa na kutumiwa na wakulima wadogo karibu maeneo yote mkoani Dodoma. Katika miaka ya hivi karibuni, pamekuwepo na ongezeko la uzalishaji wa mazao haya hususan katika wilaya ya Kondoa.

### (ii) Mizabibu:

Katika miaka ya 1970 na 1980 zabibu lilikuwa ni zao muhimu la biashara mkoani Dodoma. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 1980/81 kwa mfano, inakadiriwa kuwa jumla ya hekta 820 zilikuwa zimelimwa na kupandwa zabibu, ambapo inakisiwa kwamba tani 2,556 za zabibu zilizozalishwa. Katika jitihada za kukuza zao la zabibu serikali kwa kushirikiana na serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lijulikanalo kama KUEBEL STIFFUNG walianzisha kituo cha utafiti wa zao la zabibu pale Makutopora kwenye miaka ya 1980. Mapema miaka ya 1970 kiwanda cha kusindika zabibu (DAWICO) kilianzisha uzalishaji wa mvinyo mjini Dodoma. Pamoja na juhudi zote hizo uzalishaji wa zao la zabibu mkoani limeendelea kudidimia hadi kufikia tani 640 katika msimu wa mwaka 1994/95.

### 5.1.7 Mboga na Matunda:

Kwa muda mrefu mkoa wa Dodoma umekuwa ukitegemea mikoa ya jirani kwa ajili ya upatikanaji wa mboga na matunda. Mahitaji ya viazi, ndizi, kabeji, karoti, spinachi na maembe ni makubwa sana mkoani Dodoma. Upo uwezekano wa kupanua kilimo cha mboga na matunda kwa kuanzisha vitalu vya miche ya mboga na matunda kwa kutumia maji ya visima na mabonde ya mito kwa kilimo kidogo cha umwagiliaji. Sekta ya watu binafsi na wakulima wadogo wadogo hawana budi kuhamasishwa ili waanzishe vitalu vya miche ya miti ya matunda. Vijiji, shule na taasisi hazina budi kusaidiwa katika kuanzisha vitalu vya miti ya matunda, mkoani kote.

### 5.1.8 Zana za Kilimo:

Upanuzi wa kilimo mkoani tokea miaka ya 1980 ndio uliosababisha ongezeko kubwa la mahitaji na upatikanaji wa zana na vipuri vya zana za kilimo mkoani. Mgawanyo wa zana za kilimo mkoani kwa misimu ya 1989/90 hadi 1994/95 unaonyesha kuwa matumizi ya majembe ya kukokotwa na wanyama yaliongezeka mara dufu. Mahitaji ya majembe ya mkono yaliongezeka kwa asilimia 26.2 na mahitaji ya magunia yaliongezeka kutoka magunia 106,167 hadi kufikia magunia 250,000 kwa kipindi hicho.

Hata hivyo, matumizi ya matrekta na majembe yake hutumika zaidi katika baadhi tu ya maeneo ya mkoa, ambako wako wakulima wakubwa hususan katika maeneo yanayozalisha sana mahindi kama vile Mpwapwa na Kongwa. Matumizi ya wanyama kwa ajili ya kulima na kupalilia bado ni duni sana katika mkoa huu pamoja na kuwa na idadi kubwa ya mifugo.

**JEDWALI LXXXV: MGAWANYO WA ZANA NA VIFAA VYA KILIMO MKOANI DODOMA 1989/90 - 1994/95**

| Zana/Vifaa | Misimu ya Kilimo | |
|---|---|---|
| | 1989/90 | 1994/95 |
| Jembe la kukokotwa na ng'ombe | 1081 | 2,300 |
| Mikokoteni ya ng'ombe | 395 | 170 |
| Jembe la mkono | 48,056 | 183,224 |
| Magunia | 106,167 | 250,000 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Kilimo) Dodoma

### 5.1.9 Mbegu Bora, Mbolea na Madawa:

Tatizo kubwa linalowakabili wakulima wadogo wadogo vijijini ni upatikanaji wa mbegu bora, pembejeo na zana za kilimo kwa wakati unaotakiwa. Kwa mfano katika msimu wa kilimo wa mwaka 1994/95, mkoa ulifanikiwa kupata tani 1,501 tu za mbegu bora ya mtama iitwayo "Tegemeo na Lulu", wakati mahitaji halisi yalikuwa tani 8,339 ya mbegu hizo. Upungufu huu ndio unaowafanya wakulima wadogo kuendelea kutumia mbegu duni za jadi, ambapo mavuno yake huwa duni. Upatikanaji wa mbolea na madawa ya mimea pia ni mdogo ikilinganishwa na mahitaji halisi.

Uondoaji wa ruzuku katika pembejeo na zana za kilimo zimesababisha wakulima wadogo kushindwa kumudu bei kubwa ya zana hizo. Jedwali LXXXVI linaonyesha uchache wa pembejeo zilizopelekwa kwa wakulima katika misimu kati ya 1991/92 hadi 1994/95.

**JEDWALI LXXXVI: UNUNUZI WA PEMBEJEO MKOANI DODOMA (1991/92 - 1994/95).**

| Pembejeo za Kilimo | MISIMU YA KILIMO | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 1991/92 | 1992/93 | 1993/94 | 1994/95 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. **MBEGU;** (Tani)<br>- Mtama (Tegemeo/Lulu)<br>- Mahindi (Mbegu bora)<br>- Alizeti<br>- Ufuta (Tegemeo) | <br>38<br>24.0<br>-<br>- | <br>36<br>41<br>-<br>- | <br>22.3<br>40.0<br>1.0<br>- | <br>1,501.0<br>267.0<br>319.0<br>- |
| 2. **MBOLEA** (Za Chumvi Chumvi | 337.88 | 238 | 373.55 | 620 |
| 3. **MADAWA** (ya aina mbali mbali) | 17,279.25 | 19,033 | 13,137 | 16,523.3 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Kilimo) Dodoma

### 5.1.10 Matatizo na Uwezekano wa kupanua shughuli za Kilimo:

Uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kiasi kikubwa ni kwa ajili ya matumizi ya kaya. Ni kilimo cha kutosheleza kiwango fulani cha mahitaji ya chakula tu. Shughuli za kilimo/mifugo pekee huhusisha asilimia 85 ya watu wote mkoani, na ni sekta inayochangia kiasi kikubwa cha pato la mkoa. Pamoja na umuhimu wa sekta hii, bado inakabiliwa na vikwazo kadhaa kama ifuatavyo:

- **Mvua ndogo na isiyoaminika**:

  Mkoa wa Dodoma unafahamika kwa kuwa na mvua ndogo na isiyoaminika, ambapo husababisha upungufu mkubwa wa maji katika maeneo mengi mkoani. Kutokana na hali ya hewa isiyoaminika, mvua ndogo na

isiyoaminika, inakuwa ni vigumu kustawisha mazao mbali mbali mkoani. Hata wale wakulima walioendelea hushindwa kupanua zaidi mashamba yao kwa hofu ya mvua ndogo na isiyoaminika.

- **Udongo wenye rutuba duni:**

  Maeneo mengi mkoani Dodoma yana udongo ambao umechoka, kutokana na kutumika ovyo kwa malisho ya wanyama wengi kupita kiasi, uchomaji moto na ukataji holela wa misitu. Matukio haya kwa pamoja yamepelekea ardhi kuwa na uwezo mdogo wa kuzalisha. Hata hivyo kwenye mabonde na miinuko yapo maeneo yenye ardhi yenye rutuba nzuri.

- **Teknolojia duni:**

  Wastani wa takriban asilimia 80 hadi 90 ya mazao yanayozalishwa mkoani yanatokana na jembe la mkono, na kwa sababu hiyo, wastani wa uzalishaji kwa mkulima ni ndogo. Yapo baadhi ya maeneo ambayo kutumia ng'ombe kulimia .

- **Upungufu wa Matumizi ya Pembejeo:**

  Juhudi za kuwasaidia wakulima ili waweze kutumia pepmbejeo za kisasa bado ni mdogo. Ni wakulima wachache tu wenye uwezo wa kutumia mbolea, madawa ya wadudu, na mbegu bora. Matumizi ya mbegu bora ni muhimu sana katika kuongeza mavuno.

  Pamoja na kwamba mvua iliyopo ni ndogo na haiaminiki, bado upo uwezekano wa kuzalisha mara mbili ya kiwango cha sasa cha mazao, iwapo mbegu bora zitatumika na wakulima wote.

- **Ukosefu wa Mikopo:**

  Wakulima walio wengi vijijini hawajui wapi vilipo vyombo vinavyoweza kutoa mikopo ambayo ingewasaidia kununulia pembejeo muhimu kwa ajili ya kupanua shughuli zao za kilimo.

- **Ushauri kwa Wakulima:**

Pamoja na juhudi za serikali na wahisani kuendelea kutoa msaada wa kutoa ushauri kwa wakulima nchini kote, bado juhudi hizo hazijazaa matunda kama ilivyotarajiwa. Aidha upungufu wa motisha kwa wataalamu wanaotoa huduma hii ni mdogo, hususan tatizo la usafiri ni kubwa na linachangia sana kwa wataalam kushindwa kuwafikia wakulima vijijini.

### 5.1.11 Baadhi ya Mikakati Itakayoongeza Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo:

(i) **Miradi midogo midogo ya umwagiliaji:**

Upanuzi wa uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa umwagiliaji wa mashamba makubwa mkoani Dodoma hauwezekani. Hata hivyo kilimo cha umwagiliaji katika mashamba madogo madogo cha kitalaam kinawezekana katika mabonde ya mito kwa kutumia maji ya visima na mabwawa hususan kwa kilimo cha mboga na matunda. Aina hii ya umwagiliaji itaongeza uzalishaji wa nyanya, vitunguu, spinachi na kabeji. Uzalishaji uliopo sasa ni ule wa jadi.

(ii) **Matumizi ya Maksai:**

Ili kupanua uzalishaji katika sekta ya kilimo mkoani Dodoma, kuna haja ya kuelekeza nguvu zaidi katika matumizi ya maksai badala ya kuendelea kutegemea jembe la mkono tu. Wakulima wanatakiwa

kuhamasishwa juu ya matumizi ya teknologia hii kwa kupatiwa mafunzo ya awali. Aidha mamlaka za serikali za mitaa hazina budi kubuni mikakati ya kuwahamasisha wananchi juu ya matumizi ya teknologia hii na kuisambaza vijijini kwa kuanzisha vituo vya mafunzo. Vituo ambavyo tayari vipo kama cha Kigwe, Mtanana na Bihawana vinahitaji kuimarishwa ili viendelee kutoa mafunzo kikamilifu. Ili kuhakikisha kwamba vituo hivi vinajiendesha vyenyewe bila kufa, wananchi hawana budi kuchangia gharama za uendeshaji.

(iii) **Uimarishaji wa Huduma za Ushauri kwa Wakulima:**

Uimarishaji wa huduma za ushauri kwa wakulima ni kichocheo dhahiri ambacho kitawafanya wakulima waweze kutumia mbinu mpya za kitaalamu za kilimo ambazo hatimaye zitaongeza uzalishaji wa mazao yanayostahimili ukame kama mtama, uwele, aina ya mikunde, mpunga na mbegu za mafuta.

(iv) **Matumizi ya Samadi:**

Mkoa wa Dodoma una utajiri mkubwa sana wa samadi. Sensa ya mifugo ya hivi karibuni inaonyesha kuwa mkoa una jumla ya ng'ombe 1,600,295 wenye uwezo wa kuzalisha samadi ya tani 1.6 kwa mwaka, ambapo asilimia 6 ya samadi hiyo inapatikana katika mazizi ya wafugaji. Matumizi ya samadi mashambani itaongeza kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa mazao mbali mbali mkoani Dodoma. Sawia na matumizi ya mikokoteni

inayokokotwa na wanyama itasaidia sana katika kusafirisha samadi toka kwenye mazizi hadi mashambani, na hatimaye kusafirishwa mazao kutoka mashambani hadi nyumbani/sokoni. Matumizi ya samadi ni kirutubisho kizuri cha udongo

## 5.2 Maendeleo ya Sekta ya Mifugo:

### 5.2.1 Utangulizi:

Mauzo yatokanayo na mazao ya mifugo ndiyo chanzo cha pili kikuu cha mapato kwa karibu kaya nyingi mkoani Dodoma. Umuhimu wa mifugo pia unatokana na mifugo kuwa chanzo kikuu cha protini kutokana na mazao ya maziwa na nyama. Mifugo vile vile ni alama ya utajiri kwa watu wa Dodoma. Mara nyingine hutumika katika kulipa au kugharamia madeni na hutumika katika mambo ya jadi na mila. Kati ya kaya 259,365 zilizohesabiwa mwaka 1993/94 mkoani, kaya 82,478 sawa na asilimia 31.8 zilikuwa zinajihusisha na shughuli za ufugaji (Sensa ya Wizara ya Kilimo).

Katika mwaka 1984, mkoa wa Dodoma ulikuwa na ng'ombe 1,000,184, mbuzi 539,648 na kondoo 169,279 na hivyo kuufanya mkoa huu kuwa watatu kwa kuwa na mifugo mingi. Tanzania. Mkoa wa kwanza ni Shinyanga, na wa pili ni Mwanza. Kwa mujibu wa Sensa ya Mifugo ya 1984, uwiano kati ya idadi ya mifugo na ile ya watu ilikuwa 1:1.2 mkoani Dodoma. Mkoa huu unao mifugo mingi kupita uwezo wake, hasa ikizingatiwa kuwa uwezo wa malisho yaliyopo hivi sasa ni mifugo 12 kwa kilomita moja ya mraba, ikilinganishwa na hali halisi ya ng'ombe 20 hadi 26

kwa kilomita moja ya mraba. Ni dhahiri kuwa idadi ya wanyama waliomo mkoani inazidi uwezo wa maeneo ya malisho yaliyopo (Dodoma Interim RIDEP, 1980).

**JEDWALI LXXXVII: IDADI YA WANYAMA NA MSAMBAO WAKE KIWILAYA SENSA YA MWAKA, 1984**


| Wilaya | Ng'ombe | Mbuzi | Kondoo | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kondoa | 251,405 | 196,455 | 47,265 | 495,125 |
| Mpwapwa/Kongwa | 214,712 | 107,045 | 33,704 | 355,461 |
| Dodoma (V) | 448,102 | 182,054 | 78,229 | 708,385 |
| Dodoma (M) | 85,965 | 54,094 | 10,081 | 150,140 |
| Jumla | 1,000,184 | 539,648 | 169,279 | 1,709,111 |

Chanzo: Sensa ya Wanyama, 1984

## 5.2.2 Idadi ya Mifugo na mgawanyo wake:

Jedwali LXXXVII na LXXXVIII yanadhihirisha kuwa katika kpindi kati ya mwaka wa Sensa ya Wanyama ya mwaka 1984 na sensa ya mfano ya kitaifa iliyofanyika mwaka 1993/94, idadi ya ng'ombe mkoani iliongezeka kutoka 1,000,184 hadi kufikia 1,600,295. Hili ni ongezeko la wastani wa asilimia 62.5 katika kipindi cha miaka kumi. Ni dhahiri kwamba maelekezo ya serikali ya kupunguza idadi ya mifugo haikutekelezwa ipasavyo. Kati ya ng'ombe 1,600,275 waliohesabiwa mwaka 1993/94 katika sensa ya mifugo ya kitaifa, ng'ombe 19,842, sawa na asilimia 11.2 walikuwa ni ng'ombe wa kisasa - kama jedwali LXXXVIII linavyoonyesha.

**Kielelezo 25: Idadi ya ng'ombe mkoa wa Dodoma, Sensa ya mwaka, 1984**




**JEDWALI LXXXVIII: MGAWANYO WA NG'OMBE KWA AINA, ASILIMIA NA NAFASI YA MKOA KITAIFA - 1993/1994**

| Mikoa | Aina ya Ng'ombe | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkoa | **wa Jadi** | **wa Maziwa** | **Wanyama** | **Jumla** | **Asilimia** | **Nafasi** |
| **Dodoma** | **1,580,433** | **13,907** | **5,935** | **1,600,275** | **11.7** | **3** |
| Arusha | 1,349,572 | 36,421 | 13,196 | 1,399,189 | 10.3 | 4 |
| K'njaro | 340,604 | 102,098 | 42,838 | 485,540 | 3.6 | 11 |
| Tanga | 1,068,129 | 12,486 | 6,844 | 1,087,459 | 8.0 | 6 |
| Morogoro | 326,274 | 358 | - | 326,632 | 2.4 | 14 |
| Pwani/DSM | 48,094 | 1,462 | 1,756 | 51,312 | 0.4 | 17 |
| Lindi | 1,245 | - | - | 1,245 | 0.009 | 19 |
| Mtwara | 55,934 | - | 2,146 | 58,080 | 0.4 | 15 |
| Ruvuma | 48,882 | 3,459 | - | 52,341 | 0.4 | 16 |
| Iringa | 442,918 | 3,422 | 3,409 | 449,749 | 3.3 | 12 |
| Mbeya | 896,928 | 10,077 | 4,064 | 911,069 | 6.7 | 7 |
| Singida | 1,382,055 | - | 278 | 1,382,333 | 10.2 | 5 |
| Tabora | 547,286 | - | - | 547,286 | 4.0 | 19 |
| Rukwa | 547,420 | 691 | - | 548,111 | 4.0 | 9 |
| Kigoma | 32,097 | - | - | 32,097 | 0.2 | 18 |
| Shinyanga | 1,866,027 | - | - | 1,866,027 | 13.7 | 1 |
| Kagera | 384,031 | 7,325 | 28,374 | 419730 | 3.1 | 13 |
| Mwanza | 1,651,456 | - | 697 | 1,652,153 | 12.1 | 2 |
| Mara | 746,247 | 719 | - | 746,966 | 5.5 | 8 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| TOTAL | 13,315,632 | 192,426 | 109,537 | 13,617,595 | 100 | |

Chanzo: Sensa ya Wizara 1993/1994

Kwa mujibu wa sensa ya wanyama ya mwaka 1984, mkoa ulikuwa na jumla ya mbuzi 539,648, ambapo wilaya ya Kondoa ilikuwa inaongoza na kufatiwa na wilaya ya Dodoma vijijini. Katika matokeo ya sensa ya kitaifa ya wanyama ya mwaka 1993/94 inakadiriwa kuwa mkoa wa Dodoma ulikuwa na mbuzi 945,611. Takwimu hivi zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 1984 na 1993/94, idadi ya mbuzi iliongezeka maradufu.

Mbali ya ang'ombe na mbuzi, mkoa pia una kondoo wengi. Idadi ya kondoo pia iliongezeka kutoka 169,279 mwaka 1984 hadi 274,561 mwaka 1993/94. Jedwali LXXXIX linaonyesha jumla ya idadi ya mbuzi na kondoo mkoani Dodoma ikilinganishwa na baadhi ya mikoa mingine nchini. Wanyama wengine wanaofugwa mkoani Dodoma ni nguruwe 22,773 na punda 55,448 (Sensa ya mwaka 1993/94).


Katika miaka ya hivi karibuni, ufugaji wa kuku umeanza kustawi katika kaya nyingi mkoani, hususan mijini. Ufugaji wa kuku wengi wa biashara unafanywa na watu binafsi, taasisi za dini na za umma.

**JEDWALI LXXXIX: JUMLA YA IDADI YA MBUZI NA KONDOO NA WASTANI KWA KAYA KATIKA BAADHI YA MIKOA - 1993/1994**

| Mikoa | Jumla ya Mbuzi | | Jumla ya Kondoo | | Wastani kwa Kaya | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Idadi** | **%** | **Idadi** | **%** | **Mbuzi** | **Kondoo** |
| **Dodoma** | **954,611** | **11.05** | **274,561** | **10.20** | **13.77** | **8.93** |
| Arusha | 1,238,432 | 14.33 | 469,232 | 17.23 | 12.00 | 5.94 |
| Shinyanga | 1,112,590 | 12.88 | 404,955 | 15.04 | 9.40 | 5.57 |
| Singida | 676,518 | 7.83 | 377,388 | 14.02 | 10.74 | 7.13 |
| Mwanza | 627,202 | 7.26 | 144,495 | 5.37 | 5.99 | 4.46 |
| Tanga | 606,361 | 7.02 | 176,827 | 6.57 | 9.45 | 4.90 |
| Mikoa mingine | - | - | - | - | - | - |
| Kitaifa | 8,641,221 | 100 | | 100 | 7.45 | 5.40 |

Chanzo: Sensa ya Wizara 1993/94 - Wizara ya Kilimo

**Kielelezo 27: Idadi ya Wanyama (Kondoo) Kiwilaya Mkoa wa Dodoma, Sensa ya Wanyama 1984**




## 5.2.3 Vikwazo vya Maendeleo ya Mifugo Mkoani:

(i) **Uzalishaji duni wa mazao ya Mifugo:**

Idadi kubwa ya ng'ombe wanaofugwa Dodoma ni wale wa kienyeji wenye asili ya Zebu na Ankole ambao wana uzito mdogo wa nyama na hutoa maziwa kidogo. Kwa wastani ng'ombe hawa hutoa lita 2 - 3 za maziwa wakati wa masika na wastani wa maziwa hupungua hadi kufikia lita 0.5 hadi 1.0 kwa siku katika kipindi cha kiangazi. Wastani wa umri wa madume yanayochinjwa ni kati ya miaka 6 hadi 8 ambapo wastani wa uzito wa dume likiwa

hai ni kati ya kilo 200 hadi 300 nyakati za masika na, kilo 150 hadi 250 nyakati za kiangazi. Mitamba huwa tayari kupandikizwa mimba katika umri wa miaka kati ya 5 hadi 6. Wastani wa vifo vya ndama na wale wakubwa ni kati ya asilimia 20 - 25 kwa ndama na asilimia 10 kwa ng'ombe wakubwa. Kwa kawaida mbuzi na kondoo wanaofugwa na wenyeji hawakamuliwi maziwa na huchungwa pamoja na ng'ombe. Kwa ujumla, mbuzi na kondooo wanashamiri mkoani pote na huwa wana wastani wa uzito wa kilo 15 hadi 18 wakiwa hai. Wastani wa vifo ni chini ya asilimia 5. Wakulima wa mkoa wa Dodoma bado hawajafaidika vya kutosha na mradi wa mbuzi wa maziwa wa Hombolo ambao mbuzi huuzwa kwa bei nzuri. Kwa ujumla, mkoa wa Dodoma unapata mazao duni yatokanayo na mifugo na hivyo kutomudu kurudisha gharama za kuwatunza wanyama hawa.

(ii) **Malisho duni na ukosefu wa mipango madhubuti wa mgawanyo wa ardhi**

Matatizo makubwa yanayoisibu sekta ya mifugo ni pamoja na

- Mifugo mingi na ukosefu wa mpango mzuri wa malisho

- Malisho pamoja na maji ni adimu hususan katika kipindi cha kiangazi.

- nyakati za kiangazi vyanzo vya maji na malisho huwa ni mbali na wafugaji takriban kilomita 2 hadi

7. Hali hii ni mbaya zaidi katika wilaya za Dodoma vijijini na Kondoa. Baadhi ya wafugaji wenye makundi makubwa ya mifugo hulazimika kuhamia mikoa mingine.

- Idadi ya wanyama kwa kila kilomita moja ya mraba, ni kubwa kutokana na kukosekana kwa mipango mahususi ya kulinda na kutunza malisho yaliyopo. Ni dhahiri kuwa kukosekana kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi ambao utawapa wakulima mamlaka ya kusimamia eneo hilo kumevunjwa moyo wa kutunza na kuimarisha malisho ya mifugo.

(ii) **Huduma za Mifugo:**

Huduma za mifugo ikiwa ni pamoja na vifaa vya kazi ni haba na duni sana katika wilaya zote tano za mkoa wa Dodoma. Kwa mfano mwaka 1994, kati ya majosho 117 yaliyokuwepo mkoani ni majosho 17 tu yalikuwa yanafanya kazi. Vituo vya afya vya mifugo vilivyokuwepo ama havifanyi kazi kwa kukosa madawa au havipewi uzito unaostahili. Baadhi ya majosho hayafanyi kazi, kwa kukosa madawa na maji. Majosho mengine yameharibika na yanahitaji ukarabati. Vipo vituo 40 vya afya vya wanyama, ambavyo navyo viko katika hali mbaya na havina vifaa vya kazi. Mkoa ulikuwa na machinjio 57 ambayo nayo yanahitaji ukarabati mkubwa.

Mbali na matatizo yaliyoelezwa, mkoa unakabiliwa na magonjwa mengi ya mifugo, yale ya kawaida ni pamoja na kupe na ndigana

**JEDWALI XM: MSAMBAO WA MAJOSHO KIWILAYA, 1994**

| Wilaya | M A J O S H O | | | Vituo vya Afya - Mifugo | Masoko, Minada | Machinjio |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Yanayofanya kazi | Yalisiyofanya kazi | Jumla | | | |
| Dodoma (M) | 3 | 7 | 10 | 2 | 4 | 6 |
| Dodoma (V) | 2 | 35 | 37 | 15 | 26 | 21 |
| Kondoa | 3 | 35 | 38 | 12 | 17 | 17 |
| Mpwapwa / Kongwa | 1 | 31 | 32 | 11 | 11 | 13 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMLA | 9 | 108 | 117 | 40 | 58 | 57 |

Chanzo: Tume ya Mipango

(iv) **Ukosefu wa Fedha:**

Sekta ya mifugo inakabiliwa na matatizo ya fedha kwa sababu tokea halmashauri za wilaya na miji zirejeshwe tena mwaka 1980 hazijawahi kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa madawa ya mifugo wala vifaa muhimu. Uwekezaji wa watu binafsi katika sekta hii hata wafugaji wenyewe umekuwa mdogo. Pamoja na matatizo hayo, bado upo umuhimu mkubwa wa kuhamasisha watu kuwekeza zaidi katika sekta hii ili kuchochea uzalishaji zaidi wa mazao yatokanayo na mifugo. Maeneo yanayohitaji kuwekezwa mitaji ni pamoja na:

- Kuimarisha malisho
- Upatikanaji wa maji kwa ajili ya wanyama
- Udhibiti wa mbung'o
- Kuimarisha na kuongeza kliniki na vituo vya afya vya wanyama
- Uimarishaji majosho
- Kuboresha ufugaji mifugo na kutafuta masoko ya bidhaa za mifugo.

(v) **Ubora wa Mifugo:**

Wastani wa asilimia 95 ya ng'ombe wote waliopo mkoani ni ng'ombe wa kienyeji, ambao wanamudu mazingira magumu na rasilimali duni za mfugaji zilizoko mkoani. Hata hivyo, ubora wa mifugo inayofugwa na idadi kubwa ya wafugaji ni ya chini sana. Hali hii inapelekea uzalishaji mdogo wa maziwa na nyama hata kama malisho bora yatatumikaa.

**5.2.4 Maeneo muhimu yakushughulikiwa:**

Ufugaji mifugo ni shughuli kubwa ya kiuchumi mkoani. Baadhi ya maeneo yanayoweza kushughulikiwa kwa shabaha ya kuboresha ni pamoja na: kubadili mfumo wa ufugaji kuwa wa kibiashara, kuimarisha masoko, njia na huduma za masoko. Hii ingeweza kabisa ikaongeza pato la mkoa, na hivyo kuinua hali ya mapato na maisha ya wafugaji. Baadhi ya hatua zinazoweza kuchukuliwa kwa pamoja ni:

- Serikali za mitaa kuhakikisha kuwa madawa ya mifugo na vifaa muhimu vinapatikana katika vituo vya mifugo na kliniki zake. Pia, huduma za mifugo kama vile, majosho, vituo vya afya ya mifugo, kliniki, vibanio na machinjio, vikarabatiwa na kuwekewa vifaa. Hii itakuwa ndiyo njia pekee ya kudhibiti magonjwa ya mifugo na kuwaonyesha wafugaji matumizi ya kodi ya mifugo yao inavyowasaidia.

- Uanzishaji wa malisho na usimamizi mzuri. Utekelezaji wake uwe ni pamoja na kuyaainisha maeneo mazuri yanayofaa kwa malisho, kuzuia mmomonyoko wa udongo, na kuanzisha utaratibu wa kuyatumia malisho kwa mzunguko katika maeneo hayo. Hata hivyo katika vijiji ambavyo uwezo wa malisho ni mdogo kuliko idadi ya mifugo iliyopo, wafugaji wahamasishwe ili waiuze mifugo ya ziada hasa ile isiyo na faida, madume yasiyo ya lazima, ng'ombe waliodumaa n.k. Hatua kama hiyo itaacha ng'ombe wachache wenye faida kwao.
- Kuboresha masoko ya kuuzia bidhaa zitokanazo na mifugo na, pia vyombo vya kutoa mikopo nafuu kwa wafugaji.

- Wataalam wa huduma ya ugani hawana budi kuwaelimisha wafugaji njia nzuri za kuchagua ng'ombe bora ili waweze kuzalisha mbegu bora. Aidha ongezeko la uzalishaji wa mazao bora ya mifugo linaenda sambasamba na uchaguzi mzuri wa mbegu bora za mifugo hiyo.

- Watu binafsi mashirika mbali mbali, serikali za vijiji au vijiji vyenyewe vihamasishwe na kusaidiwa kuanzisha vituo vya ng'ombe wa maziwa na nyama.

- Vituo vya madume bora vinatakiwa vianzishwe katika vijijini vyote mkoani na vile vya zamani kama Mwitikila, Mkoyo, Sera na Mtamana vinatakiwa kufufuliwa na kufanya kazi.

- Utafiti unatakiwa ufanyike kujua mahusiano yaliyopo kati ya kilimo na mifugo katika vijiji kwa lengo la kuelewa mahusiano ya kiuchumi, kijamii na mazingira yaliyopo.

## 5.3 Maendeleo ya Sekta ya Maliasili:

### 5.3.1 Utangulizi:

Misitu na mapori ya mkoa wa Dodoma yameathiriwa kwa kiwango kikubwa kutokana na uvunaji na ufyekaji misitu kwa kiasi kikubwa, kilimo cha kuhama hama, uchomaji moto mapori, uchungaji wa mifugo mingi kuliko uwezo wa malisho, na upasuaji wa mbao, kuni na mkaa. Kwa sababu hizo ubora wa ardhi umeathirika sana na kuna upungufu mkubwa wa kuni na miti ya kujengea. Kutokana na hali hiyo wanawake walioko vijijini hivi sasa hulazimika kusafiri masafa marefu kwenda kutafuta kuni kwa ajili ya kupikia. Katika baadhi ya vijiji, wakazi wanalazimika kuchimba visiki vya miti na kutumia mizizi ya miti kwa ajili ya kupikia. Sehemu zingine, wanavijiji wameamua kutumia samadi kwa ajili ya kupikia. Kadri miaka inavyokwenda, ndivyo mahitaji ya mazao ya misitu yanavyoongezeka, kiasi kwamba hata maeneo ya misitu ambayo pia ni vyanzo vya maji yameathirika vibaya. Zipo sababu za kutosha kwa uongozi wa mkoa kulipa kipaombele swala la kupambana na uharibifu wa mazingira.

Mkoa wa Dodoma unakadiriwa kuwa na kilomita za mraba 14,700 za misitu na uoto wa asili, ikiwa ni pamoja na miinuko ya Irangi. Kati ya eneo lote hilo kilomita 942 za mraba sawa na asilimia 6.7 ni misitu ya hifadhi. Kwa ujumla ipo misitu 13 ya hifadhi mkoani Dodoma.

### 5.3.2 Misitu:

Mkoani Dodoma unakadiriwa kuwa kilomita 14,700 za mraba za misitu sawa na asilimia 36 ya eneo lote la mkoa. Mkoa una misitu 17 ya hifadhi ya serikali yenye eneo la kilomita 1,228.95 za mraba, kati ya hiyo misitu 13 inahudumiwa na serikali kuu. Misitu hiyo kiwilaya ni kama ifuatavyo:

(i) **Wilaya ya Kondoa:**

Ipo misitu ya hifadhi mitano chini ya mamlaka ya serikali kuu, na ina eneo la kilomita 324.73 za mraba. Misitu hiyo ni Salanka, Kome, Chemichemi, Berabera, na Songa. Misitu ya hifadhi ya serikali ya Kome na Chemichemi hairuhusiwi kuvuna, ila iliyosalia inahitaji kibali maalum cha kuvuna. Hifadhi kubwa kuliko zote ni Songa yenye kilomita 187.75 za mraba, ukifuatiwa na msitu wa Salanka wenye kilomita 83.36 za mraba. Msitu mdogo kuliko yote ni ule wa Chemichemi ambao una kilomita 0.16 za mraba na huu ndio chanzo cha chemchem ya maji moto mjini Kondoa.

Mbali ya hayo, upo msitu wa hifadhi wa Isabe wenye kilomita 42.49 za mraba unaomilikiwa na halmashauri ya wilaya ya Kondoa. Kwa ujumla eneo lote la misitu ya hifadhi chini ya usimamizi wa halmashauri ya wilaya ni kilomita za mraba 367.22.

(ii) **Wilaya ya Mpwapwa/Kongwa:**

Ipo misitu sita ya hifadhi inayomilikiwa na serikali kuu. Majina yake na ukubwa wa maeneo hayo katika kilomita za mraba ni kama ifuatavyo:

Njoge (11.52), Mafomero (32.37), Mangalisa (49.30), Wotta (18.72), Ibogo (3.27), na Mlali (62.16). Misitu ya Mafomero, Mangalisa na Wotta ni hifadhi zilizofungwa, na haziruhusiwi kuvunwa mazao ya miti na, ni vyanzo vizuri vya maji. Kwa ujumla, hifadhi za misitu iliyopo Mpwapwa na Kongwa ina eneo lenye kilomita 177.34 za mraba.

(iii) **Wilaya ya Dodoma Vijijini:**

Wilaya hii ina hifadhi nne za misitu ya serikali. Hifadhi ya Chenene ina kilomita 226.26 za mraba na ndiyo hifadhi pekee inayomilikiwa na serikali kuu, na ilizosalia ni mali ya halmashauri ya wilaya - kama vile Chiyai, (433.3), Goima (6.96), na Sasajila (11.45). Kwa ujumla, hifadhi ya misitu katika wilayani Dodoma vijijini ina kilomita 678.33 za mraba.

(iv) **Wilaya ya Dodoma Mjini:**

Wilaya ya Dodoma mjini ina misitu miwili ya hifadhi, yaani Vikonje na Kigongwe. Msitu wa hifadhi ya Vikonje ni mali ya halmashauri ya Manispaa na, una eneo la kilomita 1.98 za mraba. Msitu wa hifadhi wa Chigongwe wenye

kilomita 4.08 za mraba ni mali ya serikali kuu. Kwa ujumla, wilaya ya Dodoma mjini ina kilomita 6.06 za mraba za hifadhi za misitu.

(v) **Misitu inayoombewa Hifadhi:**

Ipo misitu mitatu inayoombewa hifadhi mkoani Dodoma. Misitu hiyo ni pamoja na ukanda wa juu wa Irangi wilayani Kondoa, wenye kilomita 178.36 za mraba, safu za Kiborian, zilizo katika wilaya ya Mpwapwa zenye kilomita 549.36 za mraba, na eneo la Chenene lenye kilomita 298.36 za mraba katika wilaya ya Dodoma vijijini. Kwa hiyo, jumla ya kilomita 1,026.42 za mraba ndizo zinazombewa kuwa misitu ya hifadhi ya serikali.

### 5.3.3 Upanuzi Misitu na Hifadhi ya Udongo:

Matatizo makubwa ya mmomonyoko wa udongo umeanza siku nyingi takriban kabla ya Tanzania kupata Uhuru mwaka 1961. Katika miaka ya 1940 na 1950 hatua kadhaa zilichukuliwa za kudhibiti mmomonyoko wa ardhi zikiwa ni pamoja na kutolewa amri ya kupunguza idadi ya mifugo, amri ya kulima makinga maji, kilimo cha matuta, na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua, na mpangilio mzuri wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho. Aidha amri ya kupanda miti kwa wingi ikiwa ni pamoja na kupanda mikatani - aina ya "Agave Sisalana" ilitekelezwa kikamilifu, kuzunguka mashamba pamoja na maeneo mengine yafaayo kwa kilimo ili yasiathirike zaidi.

Mradi wa Hifadhi Ardhi Dodoma (HADO) ulianzishwa mwaka 1973 na serikali kwa ushirikiano na shirika la misaada la serikali ya Sweden (SIDA). Kuanza kwa mradi huu kuliashiria dhamira ya wazi ya serikali ya kudhibiti tatizo la mmomonyoko wa udongo na uharibifu wa mazingira - mkoani Dodoma, hususan wilaya ya Kondoa ambapo uharibifu wa ardhi ni mkubwa.

Mpaka sasa mradi wa HADO unatekelezwa katika wilaya zote mkoani, kwa kuwahusisha wale wote wanaohusika katika shughuli mbali mbali, kama vile uoteshaji wa miche ya miti katika vitalu, ulindaji wa misitu iliyopandwa na uoto wa asili, upunguzaji mifugo, uimarishaji maeneo yaliyoathiriwa kwa kusisitiza upandaji wa miti ya mbao na kuni. Matunda ya kazi hiyo ngumu yameanza kupatikana hivi sasa, kwani maeneo yaliyoathirika zamani, leo yameanza kuwa na miti ya ujenzi na kuni. Kazi hiyo imefanyika kwa ushirikiano wa watu binafsi, wanavijiji, taasisi za umma n.k. kama jedwali LMI, XMII na XMIII yanavyoonyesha.

**JEDWALI XMI: UPANDAJI MITI NA UMILIKAJI - 1992**

| Wilaya | Vijiji | Shule | Serikali | Watu Binafsi |
|---|---|---|---|---|
| Kondoa | 5000 | 42324 | 297565 | 80890 |
| Dodoma (M) | - | 25095 | 434134 | - |
| Dodoma (V) | 33484 | 56940 | 363310 | 68440 |
| Mpwapwa | 4349 | 49549 | 407551 | 43090 |
| JUMLA | 42833 | 173908 | 1502560 | 192420 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Maliasili) Dodoma

**JEDWALI XMII: UPANDAJI MITI NA UMILIKAJI 1993**

| Wilaya | Vijiji | Shule | Serikali | Watu Binafsi |
|---|---|---|---|---|
| Kondoa | 6000 | 32141 | 207734 | 69440 |
| Dodoma (M) | 1649 | 12325 | 363310 | 5680 |
| Dodoma (V) | 7204 | 45828 | 285110 | 18500 |
| Mpwapwa | 80000 | 33000 | 50000 | 118000 |
| JUMLA | 94853 | 124294 | 902844 | 210620 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Maliasili) Dodoma

**JEDWALI L XMIII: UPANDAJI MITI NA UMILIKAJI 1994**

| Wilaya | Vijiji | Shule | Serikali | Watu Binafsi |
|---|---|---|---|---|
| Kondoa | 15424 | 18868 | 278999 | 57553 |
| Dodoma (M) | 3799 | 9275 | 269000 | 8670 |
| Dodoma (V) | 1700 | 47105 | 297565 | 31830 |
| Mpwapwa | - | 32460 | 465586 | 82790 |
| JUMLA | 20923 | 107708 | 1311150 | 180,843 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Maliasili) Dodoma

## 5.3.4 Kilimo na Hifadhi Misitu

Katika jitihada za kupunguza uwezekano wa kuenea kwa jangwa uongozi wa mkoa umefanya majaribio katika baadhi ya vijiji na shule za msingi zilizo chini ya mpango wa HADO, namna ya kuoanisha shughuli za kilimo na upandaji miti.

Matokeo ya majaribio hayo ni kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Thawi | Hekta | 1.0 |
| - | Kondoa | " | 2.0 |
| - | Kalamba | " | 5.0 |
| - | Bolisa | " | 0.27 |
| - | Waida | " | 1.0 |
| - | Kingale | " | 1.6 |

Katika miaka ya hivi karibuni, uoanishaji wa shughuli za kilimo na upandaji miti umeongezeka kwa kiasi kikubwa katika wilaya zote, wilaya ya Mpwapwa ikiongoza.

## 5.4 Ufugaji Nyuki:

### 5.4.1 Utangulizi:

Utafiti uliofanywa na timu ya wataalam kutoka Canada mwaka 1975 unaonyesha kwamba pamoja na mkoa wa Dodoma kuwa na hali mbaya ya hewa, mkoa una rasilimali kubwa sana kuendeleza ufugaji wa nyuki, kwani ipo miti na vichaka vya kutosha vyenye maua yanyofaa nyuki kwa ajili ya utengenezaji wa asali. (Dodoma RIDEP 1975)

Sehemu kubwa ya watu wa Dodoma hasa wa kabila la Wasandawe na Watatoga, ni wafugaji wa nyuki na warina asali wa siku nyingi katika maisha yao. Kwa hali hiyo, ufugaji wa nyuki ni mojawapo ya shughuli muhimu ya kiuchumi kwa baadhi ya vijiji. Inakadiriwa kuwa mauzo ya asali na nta yanachangia wastani wa asilimia 20 ya mapato ya kaya zinazojishughulisha na kazi hii kwa mwaka. Katika wilaya ya Kondoa pekee, mauzo ya asali na nta

huchangia wastani wa asilimia 30 ya mapato ya kaya zinazojihusisha na kazi hii kwa mwaka.

Tarafa zinazoongoza kwa uzalishaji wa mazao ya nyuki ni Kwamtoro, Farkwa, Mondo na Kituo katika wilaya ya Kondoa. Tarafa zingine ni Chilonwa, Mwitikira, Mundemu na Itiso katika wilaya ya Dodoma vijijini. Makadirio ya hivi karibuni (1996) yanaonyesha kwamba ipo mizinga zaidi ya 4,000, kati ya hiyo, mizinga 3,200 ni ya kienyeji. Kati ya idadi hiyo ya mizinga ya kienyeji, asilimia 60 inapatikana wilaya ya Kondoa.

### 5.4.2 Mazao ya Nyuki:

Upatikanaji wa takwimu sahihi na za kujitosheleza za mazao ya nyuki ni ngumu karibu katika wilaya zote. Takwimu chache zilizopo hazielezei kwa uhakika kuhusu kiasi halisi cha asali na nta kilichozalishwa kwa mwaka. Hata hivyo, kwa takwimu zilizokusanywa na kuonyeshwa katika jedwali XMIV zinadhihirisha kwamba kiwango cha mazao ya nyuki yaliyouzwa kati ya mwaka 1987 hadi 1992 aidha kiliongezeka kidogo au kilibakia pale pale. Hali hiyo huenda inatokana na njia na taratibu duni za urinaji, utayarishaji na uhifadhi wa asali na nta, ambao unasababishwa na matumizi ya vifaa duni.

**JEDWALI XMIV: MAZAO YA NYUKI YALIYOUZWA MKOANI KWA MIAKA ILIYOCHAGULIWA**

| Miaka | Nta (Tani) | Asali (Tani) |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1987 | 87,325 | 260,975 |
| 1989 | 59,732 | 158,196 |
| 1991 | 55,600 | 147,180 |
| 1993 | 73,400 | 219,412 |
| 1994 | 90,096 | 132,350 |

Chanzo: Takwimu za Shirika la RCU

### 5.4.3 Matarajio ya Mafanikio ya Sekta ya Nyuki:

Kama ilivyoelezwa awali, wastani wa milimita 550 za mvua kwa mwaka haifai kwa ufugaji wa nyuki. Hata hivyo mazingira yaliyopo mkoani Dodoma yanaruhusu upanuzi na uimarishaji wa shughuli za ufugaji nyuki. Uchunguzi wa awali wa maji viumbe na mimea uliofanyika Dodoma katika miaka ya 1974 (Chatlagi Mathew na N. Vishan, 1997) unaonyesha kuwa zaidi ya nusu ya eneo la mkoa lina aina fulani ya mimea na miti ambayo ndiyo inayofaa kwa shughuli za ufugaji wa nyuki wa biashara. Baadhi ya makabila kama vile Wasandawe, Waburunge na Watatoga wanao uzoefu wa hali ya juu kuhusiana na ufugaji wa nyuki kwa kipindi kirefu. Pamoja na yote hayo, hivi sasa biashara ya uuzaji wa asali na nta ina faida kubwa na ni chanzo kizuri cha mapato kwa kaya nyingi vijijini zinazojishughulisha na ufugaji huu, hususan katika wilaya za Kondoa na Dodoma Vijijini. Maendeleo ya sekta ya nyuki itategemea kutekelezwa kwa hatua zifuatazo:

(i) Uimarishaji wa huduma ya kitaalam (ugani) kwa wafugaji nyuki ili wapate utaalam unaohitajika.

(ii) Kuhamasisha watu binafsi na hasa wenye uwezo na nia ili waweze kuanzisha karakana za kutengeneza mizinga ya kisasa ya nyuki

(iii) Kuoanisha shughuli za ufugaji nyuki na zile za upandaji na uhifadhi misitu.

(iv) Utoaji wa fedha za mikopo kwa wanavijiji wanaojishughulisha na ufugaji wa nyuki.

(v) Kuanzishwa kwa masoko ya kuuzia mazao ya nyuki na vifaa vya kusindika mazao yake.

## 5.5 Uvuvi:

Kutokana na kutokuwepo kwa mito mikubwa na maziwa makubwa shughuli za uvuvi sio za muhimu sana kiuchumi mkoani Dodoma. Ongezeko la mavuno na mauzo ya samaki ndani ya mkoa katika miaka ya karibuni yametokana na mabwawa yaliyochimbwa, kama vile -Hombolo, Mtera, Nondwa, Kisaki na Dabalo. Hapo zamani shughuli hizi za uvuvi zilikuwa zikifanyika kwenye mabwawa na mito midogo, kama vile ziwa Haubi kwa ajili ya kitoweo tu. Baada ya kuchimbwa kwa mabwawa ya Mtera na Hombolo, baadhi ya watu wamejitokeza katika kuendeleza biashara ndogo ndogo ya samaki. Mauzo ya samaki kati ya miaka ya 1992 na 1994 yanaonyesha kuwa kiuchumi shughuli ya uvuvi bado ni ndogo mkoani Dodoma.

**JEDWALI XMV: UZITO NA THAMANI YA SAMAKI WALIOVULIWA NA KUUZWA MKOANI KATI YA 1992 NA 1994**

| Mwaka | Uzito Tani | Thamani Tshs.'000 |
|---|---|---|
| 1992 | 5306.3 | 585760.6 |
| 1993 | 4023.6 | 356069.5 |
| 1994 | 4664.9 | 470914.05 |
| JUMLA | 13994.8 | 1412744.2 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Maliasili) Dodoma

## 5.6 Rasilimali ya Madini:

Kwa ujumla mkoa haukujaliwa sana kuwa na rasIlimali ya madini, ingawa hivi karibuni, wataalam wa fani ya madini (jiolojia) wamegundua ishara za kuwepo dhahabu katika maeneo ya vilima vya Nzuguni, mashariki ya mji wa Dodoma, na pia, eneo la Mafurungi (Simanguru). Uvunaji chumvi upo katika maeneo ya bonde la Bahi na katika kijiji cha Mahomanyika katika wilaya ya Dodoma vijijini. Vile vile yapo machimbo ya chokaa katika maeneo ya Kigwe, Iringa-Mvumi, Keegea, Hombolo, Mahomanyika na Mlowa Bwawani katika wilaya ya Dodoma vijijini. Katika eneo la Nyankali kipo kiwanda cha kusaga kokoto ngumu kwa ajili ya shughuli mbali mbali za ujenzi. Mchanga unavunwa kando kando ya mito iliyopo katika manispaa ya Dodoma. Yapo aina nyingine ya madini ya vito mkoani kama vile "Chrysoprase" inayochimbwa maeneo ya Haneti, Itiso; madini aina ya "Scapolite," "Rhodolite" na "Opal" yanayochimbwa katika wilaya ya Mpwapwa.

## 5.7 Wanyama Pori:

Mkoa wa Dodoma una mbuga ya hifadhi ya wanyama pori iitwayo "Swagaswaga". Mbuga hii iko kilomita 24 magharibi ya mji wa Kondoa na ina kilomita 710 za mraba. Yapo pia maeneo mawili yaliyozuiliwa kuwindwa na serikali nayo ni; Rudi, mbuga hii ipo katika wilaya ya Mpwapwa na ina kilomita 1,364.5 za mraba, na Kongwa ambayo inajumuisha shamba la ng'ombe la Kongwa, lenye eneo la kilomita 1,500 za mraba wilayani Kongwa. Katika mbuga na maeneo yanayolindwa wapo wanyama pori wengi kama vile Tembo, Kudu, Nyemela, Nyati, Nguruwe pori, Ngiri,

Pundamilia, Simba, Swala, Chui, Fisi, Digidigi, na aina mbali mbali za ndege ikiwa ni pamoja na Mbuni.

## 5.8 Maendeleo ya Sekta ya Viwanda:

Juhudi ya serikali ya kutoa vivutio mbali mbali kwa wawekezaji katika sekta ya viwanda ilitekelezwa mwaka 1980, lakini hata hivyo, mafanikio ni madogo sana. Viwanda vilivyoaanzishwa kati ya mwaka 1975 na 1995 ni kama ifuatavyo:

- Kiwanda cha bidhaa za Kokoto - Nyankali
- Kiwanda cha Matofali na Malumalu cha Zuzu
- Kiwanda cha Magodoro
- Kiwanda cha Unga - Kipepeo
- Kiwanda cha Mvinyo - Dodoma
- Kiwanda cha Mvinyo - Bihawana

Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) limeendelea kuhamasisha na kusimamia uanzishaji wa viwanda vidogo mijini na vijijini. Katika jitihada hizo, SIDO inatarajia kuanzisha viwanda vidogo vya kutengeneza bidhaa mbali mbali katika maeneo ya Mlali, Mvumi, Hombolo na Bereko. Baadhi ya fani zitakazoendelezwa ni pamoja na ushonaji, useremala, ufundi vyuma na ufundi bati.

# SURA YA SITA

## 6.0 MASUALA MENGINE YA MAENDELEO:

### 6.1: Mpango wa Kuhamisha Makao Makuu ya Serikali:

Katika mwaka 1972 serikali ilitoa msimamo kuhusu dhamira yake ya kuhamisha makao makuu yake kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma. Kwa sababu hiyo, Mamlaka ya Ustawishaji makao makuu Dodoma (CDA) ikaundwa kwa sheria ya Bunge ya mwaka 1973, ili kuyatekeleza majukumu hayo. Shabaha ya kuanzishwa kwa mamlaka haya ilikuwa ni kuhakikisha dhamira ya kuhamia Dodoma inakamilika.

Baada ya serikali kugundua kuwa utekelezaji wa mpango huo ulikuwa unakwenda kwa kasi ndogo sana, mwaka 1989 ilipitishwa sheria ya upendeleo maalum kwa wale ambao wangewekeza katika mji mkuu Dodoma (Special Investment Area Act No. 7). Aidha shabaha ya sheria hiyo ilikuwa ni kuwahamasisha wafanya biashara mbali mbali, watu binafsi na mashirika ya umma ili waanzishe au wahamishie Dodoma shughuli zao za kibiashara. Sheria hiyo ya upendeleo ililenga katika maeneo muhimu yafuatayo:

(i) Sheria iliainisha vifaa vya ujenzi ambavyo kama vikiuziwa Dodoma vitasamehewa kodi ya mauzo na kodi ya ushuru. Shirika la CASCO lilianzishwa chini ya CDA ili kushughulikia mauzo hayo.

(ii) Sheria iliainisha shughuli za biashara na aina ya viwanda ambavyo vingesamehewa kodi ya mapato katika miaka mitano ya kwanza, na baada ya hapo kulipa nusu ya kodi hiyo kwa miaka 20 inayofuatia.

(iii) Sheria iliainisha viwanda ambavyo vingesamehewa nusu ya umeme na maji

(iv) Sheria iliruhusu mikopo kwa wale watakaowekeza Dodoma

Katika kutekeleza sheria hiyo, wawekezaji ambao walipenda kufaidika na sheria ya uwekezaji Dodoma walilazimika kujiandikisha katika shirika la Ustawishaji Makao Makuu (CDA).

Mpango wa kuhamiaji mji mkuu Dodoma ulipangwa kutekelezwa kwa muda wa miaka kumi lakini hadi mwaka 1996 mpango huu ulitimiza miaka 20. Aidha kwa mujibu wa ripoti ya utekelezaji ya CDA, kazi kubwa za kimsingi zimekwisha tekelezwa. Hata hivyo kutokana na uhaba wa fedha serikalini, uhamishaji wa makao makuu kwenda Dodoma bado haujatekelezwa. Kwa upande mwingine, kushindikana kuhamishwa makao makuu kwenda Dodoma kumewathiri kwa kiwango kikubwa wawekezaji ambao tayari walikwishawekeza vitega uchumi vyao. Kwa mfano majumba mengi yamebaki bila shughuli yoyote, mapato yatokanayo na shughuli za kibiashara bado ni duni, na baadhi ya wawekezaji wameuhama mji na kutoroka baada ya kushindwa kulipa madeni ya Benki, na hivyo vitega uchumi vyao kutwaliwa na Benki zinazohusika.

## 6.2 Vikundi vya Kiuchumi:

### (a) Vikundi vya akina Mama:

Kwa mujibu wa ripoti ya sensa ya mwaka 1988, wastani wa asilimia 52 ya watu wote wa mkoa ni wanawake. Sehemu kubwa ya idadi ya wanawake hawa, wanategemea kilimo, miradi midogo midogo kama usukaji na ushonaji, uendeshaji wa mashine n.k.

Wanawake ndilo kundi linaloshiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali lakini kutokana na mila na desturi za watu wa Dodoma, wanawake wananyimwa haki ya kimsingi ya kumiliki na kufaidi matunda ya miradi mbali mbali wanayoanzisha.

Pamoja na maonevu hayo, wanawake wa Dodoma wameweza kujiunga katika vikundi mbali mbali vya kiuchumi ili kuboresha maisha yao ya kila siku. Hadi kufikia mwaka 1995 jumla ya vikundi 260 vilikuwa vimeanzishwa mkoani Dodoma. Kati ya vikundi 260 vilivyopo vikundi 32 vimepata msaada moja kwa moja kutoka katika mfuko wa maendeleo ya wanawake, ulioanzishwa mwaka 1994/95 na serikali. Vikundi vilivyobakia 228 vya kiuchumi hujishughulisha na uzalishaji wa bidhaa kama vile ushonaji, usukaji, utengenezaji pombe za kienyeji, bustani na mama ntilie. Jedwali XMVI linaonyesha msambao wa vikundi vya akina mama kiwilaya. Aidha, asilimia 89 ya vikundi 260 viko mijini.

**JEDWALI XMVI: VIKUNDI VYA KIUCHUMI VYA AKINA MAMA KIWILAYA - 1995**

| Shughuli | Dodoma Mjini | Dodoma Vijijini | KONDOA | MPWAPWA | KONGWA | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Umoja wa vikundi vya akina mama | 8 | 6 | 6 | 6 | 6 | 32 |
| 2. Vikundi vya kazi mbali vya akina mama | 114 | 48 | 27 | 32 | 7 | 228 |
| Jumla | 122 | 54 | 33 | 38 | 13 | 260 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Maendeleo ya Jamii) Dodoma

## 6.3 Vyama vya Ushirika:

Hadi mwaka 1996, kulikuwepo na vyama vya ushirika 164 ambavyo vilikuwa na shughuli mbali mbali za kiuchumi kama Jedwali XMVII linavyoonyesha kiwilaya.

**JEDWALI XMVII: VYAMA VYA USHIRIKA VILIVYOPO MKOANI DODOMA, KIWILAYA, 1995**

| Aina ya Ushirika | Wilaya | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | Dodoma Vijijini | Dodoma Mjini | Mpwapwa /Kongwa | Kondoa | |
| • Vyama vya Msingi vya uzalishaji | 2 | 5 | 23 | - | 30 |
| • Maduka rejareja | - | 17 | - | - | 17 |
| • Kukopa na kulipa | 2 | 23 | 12 | 5 | 42 |
| .• Nyumba | - | 57 | - | - | 57 |
| •Ng'ombe wa maziwa | - | 1 | - | 8 | 9 |
| • Shughuli zingine | - | 5 | 3 | 1 | 9 |
| Jumla | 4 | 108 | 38 | 14 | 164 |

Chanzo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Ushirika) Dodoma

## 6.4 Wahisani/Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi Dodoma

Mkoa wa Dodoma unao wahisani na mashirika ya nje yasiyo ya kiserikali machache sana. Wahisani na mashirika haya hutoa misaada ya kiufundi na kifedha katika kutekeleza miradi mbali mbali hususan vijijini. Wahisani hawa hutekeleza miradi hii kwa kushirikiana na serikali kuu, serikali za mitaa na vijiji. Jedwali XMVIII linaonyesha orodha ya wahisani na mashirika yanayofanya kazi mkoani Dodoma, maeneo husika, na shughuli zao.

**JEDWALI XMVIII: ORODHA YA WAHISANI WALIOPO MKOANI, MAENEO NA SHUGHULI WANAZOZIFANYA**

| Jina la Mhisani au Shirika | Eneo la Kazi | Shughuli za Miradi |
|---|---|---|
| i) Water Aid Tanzania- Shirika la Kiingereza | - Wilaya zote 5 Mkoani | - Miradi ya maji vijijini<br>- Kuboresha afya za wanavijiji |
| ii) AFRICARE - Shirila la Kimarekani | - Dodoma mjini hasa Mkonze, Iyumbu Hombolo na Mkonya<br>- Kongwa Tarafa ya Mlali | - Kuboresha teknolojia ya upatikanaji maji vijijini, kwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua<br>- Kuboresha afya ya mama na watoto |
| iii) World Vision International<br>Umoja wa jumuiya ya Kikristo | - Wilaya zote tano | - Usambazaji maji<br>- Elimu ya msingi ya afya<br>- Misitu na uzalishaji wa mazao<br>- Ukarabati majengo ya shule<br>- Maafa |
| iv) Japanese Overseas Cooperation Volunteers (JOVC) shirika lililo chini ya JICA | - Dodoma Mjini | - Vitalu vya miche ya miti, maua<br>- Utengenezaji wa mazingira ya mji |
| v) Inades Information- Umoja wa nchi 11 za Africa | - Wilaya zote 5 | - Mafunzo kwa wanavijiji namna ya kuondokana na umaskini |

| | | | |
|---|---|---|---|
| vi) | SNV - Shirika la serikali ya Uholanzi | - Wilaya ya Kondoa | - Mpango wa uwiano wa wilaya ya Kondoa (KIRDEP) |
| vii) | LVIA - Shirika la Italy | - Kongwa | - Maji<br>- Usafi wa mazingira<br>- Kilimo |
| viii) | DONET | - Wilaya zote 5 | - Hifadhi ya mazingira |
| ix) | MIGESADO | - Wilaya zote 5 | - Nishati ya samadi (Bio-gas plants) |
| x) | HABITAT FOR HUMANITY | - Wilaya zote 5 | - Ujenzi wa nyumba bora na nafuu |
| xi) | CMRS | - Wilaya zote 5 | - Maji, mazingira |
| xii) | ICROSS | - Mpwapwa and Dodoma (V) | - Afya |

Chanzo:: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa - Dodoma.

# SURA YA SABA

## 7.0 MAENEO YANAYOFAA KWA UWEKEZAJI MKOA WA DODOMA

Shughuli za kilimo kwa kiwango kikubwa mkoani zinaendeshwa na wakulima wadogo wadogo. Uzalishaji wa mazao katika sekta ya kilimo mkoani ni mdogo sana, ikiliganishwa na hatua iliyofikiwa na wakulima wa mikoa ya Nyanda za juu za kusini. Hata hivyo, yapo maeneo yenye rutuba nzuri katika wilaya za Kongwa, Mpwapwa, na Kondoa, ambako kilimo cha mashamba makubwa makubwa kinawezekana.

Mabonde yenye maji maji ya Bahi yana udongo nzito wa ufinyanzi au udongo wa mbugani, ambao hauna chumvi chumvi na unafaa sana kwa kilimo cha mashamba makubwa makubwa ya mpunga. Ili kuwavutia wawekezaji katika miradi ya kilimo, mkoa umeamua kuimarisha huduma ya ushauri kwa wakulima, na mafunzo kwa shabaha ya kuwavutia wakulima wenye uwezo ili walime mashamba makubwa. Maeneo ambayo yanatiliwa mkazo na mkoa katika kilimo ili wawekezaji waweze kujitokeza ni pamoja na:

(i) **Kilimo cha mashamba makubwa ya Mahindi:**

Yapo maeneo kadha katika wilaya za Mpwapwa, Kongwa na Kondoa ambao yana rutuba na mvua za kutosha kwa ajili ya kilimo cha mahindi. Maeneo hayo yangeweza kulimwa mashamba makubwa makubwa ya

mahindi. Mkoa wa Dodoma kuwepo karibu na mkoa wa Dar es Salaam kuna uhakika wa soko la mahindi.

(ii) **Zao la Zabibu:**

Dodoma ni mkoa pekee Tanzania unaolima zabibu kwa wingi. Kwa sababu hiyo, upo uwezekano wa kulima mashamba makubwa na ujenzi wa viwanda vya kutengeneza mvinyo.

(iii) **Mbegu za Mafuta:**

Wawekezaji wanakaribishwa kuanzisha mashamba makubwa ya karanga na kufufua mashamba ya karanga yaliyoanzishwa na Wakoloni mara baada ya kwisha kwa vita vya pili vya Dunia. Mbegu za mafuta kama vile karanga, ufuta, nyonyo, zinastawi vizuri mkoani, na upo uwezekano wa kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa ya mazao hayo.

(iv) **Viwanda vya kusindika Nyanya:**

Dodoma ni maarufu sana kwa uzalishaji wa nyanya nyingi, hali ambayo inapelekea uwezekano wa kuanzisha viwanda vya kusindika nyanya.

## 7.2 Uzalishaji Mifugo:

Kwa ujumla Dodoma ni mkoa maarufu kwa utajiri wa mifugo. Kwa sababu hiyo, ufugaji wa mifugo ni mojawapo ya shughuli

kubwa ya kiuchumi. Zaidi ya asilimia 90 ya ng’ombe wote mkoani ni wa aina ya Zebu. Ng'ombe hawa wana pembe fupi, wana uzito mdogo wa takriban kilo 25 akiwa mzima, wana uzalishaji mdogo wa maziwa - lita 1 hadi 2 za maziwa kwa kutwa, na wana uwezo wa kuhimili magonjwa na mazingira magumu ya ukame. Hata hivyo kikwazo kikubwa katika jitihada mbali mbali za kuboresha mifugo ya jadi ni mila, desturi na mtazamo tofuti wa wenye ng'ombe wenyewe. Wafugaji wengi hufuga mifugo mingi kwa ajili ya ufahari na kwa ajili ya shughuli nyingine za kijamii. Iwapo wafugaji watafuata mtazamo mpya wa kuboresha mifugo yao ya jadi, pato lao linaweza kuongezeka mara dufu. Maeneo yafuatayo yanafaa kwa uwekezaji ndani ya sekta hii ya mifugo:

(i) **Mashamba ya Mifugo:**

Ipo haja ya kufanya utafiti wa maeneo ambayo yanfaa uanzishaji wa mashamba makubwa hususan katika wilaya za Kongwa, Mpwapwa na Kondoa.

(ii) **Ngozi**:

Zao la ngozi ni bidhaa muhimu kwani hutupatia fedha za kigeni na pia ni malighafi kwa ajili ya viwanda vinavyotengeneza bidhaa za ngozi na viatu. Baada ya kufilisika kwa kiwanda tanzu cha ngozi, hakuna soko la uhakika la kununua ngozi mkoani Dodoma. Kutokana na hali hiyo mkoa unakaribisha watu kuja kuwekeza katika sekta hii ya ununuzi na utengenezaji wa mazao yatokanayo na ngozi.

(iii) **Vituo vya kuzalisha Mitamba:**

Uwekezaji katika vituo vya kuzalisha mitamba unakaribishwa ili kuboresha aina ya mitamba na madume. Kwa hivi sasa shughuli ipo chini ya mikono ya serikali. Kutokana na tatizo la fedha vituo hivi havifanyi kazi kikamilifu.

## 7.3 Ufugaji wa Nyuki:

(i) **Shughuli za ufugaji Nyuki:**

Mkoa una uwezo mkubwa wa kupanua shughuli za ufugaji nyuki, kwa vile ipo mimea mingi inayofaa kwa ufugaji huu. Kinachohitajika ni kubadili teknolojia ya ufugaji kwa kutumia mizinga ya kisasa badala ya ile ya jadi. Pori lilipo mkoani lenye kila sifa ya kuendeleza ufugaji wa nyuki lina eneo la hekta 154,222. Watu binafsi hususan vijana ambao hawana kazi vijijini wanaweza kuanzisha miradi ya ufugaji wa nyuki.

## 7.4 Elimu:

Kijiografia mkoa wa Dodoma unafikika kirahisi kutoka sehemu yoyote ya nchi yetu na kwa hiyo hiki ni kivutio cha kutosha kwa wawekezaji katika sekta ya elimu. Sera za serikali kuhusu elimu zinaruhusu watu binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), madhehebu ya dini, kuanzisha na kuendesha shule za msingi, na za sekondari. Kwa sababu hiyo, mtu/watu binafsi na mashirika mbali

mbali wanakaribishwa kuwekeza katika sehemu zifuatazo za elimu:-

- Shule za msingi zinazofundisha Kiingereza
- Shule za Sekondari za Ufundi
- Vyuo cya Ufundi

## 7.5 Viwanda:

Mkoa una kiwango duni sana cha maendeleo ya viwanda. Upo uwezekano kuwa wawekezaji wengi hawajui maeneo ya uwekezaji ambayo mji wa Dodoma inaizidi miji mingine. Mamlaka ya ustawishaji makao makuu, Dodoma umekwishakamilisha ujenzi wa miundo mbinu mbali mbali kwa ajili ya uanzishaji wa viwanda mbali mbali. Kutokana na hali hiyo watu binafsi wanakaribishwa kuja kufanya utafiti wa aina gani ya viwanda vinavyofaa kuanzishwa Dodoma.

# KIAMBATISHO "A"

## MKOA WA DODOMA - KWA UFUPI

1:0 **Mahali ulipo:**

Mkoa wa Dodoma uko katikati ya nchi na uko kati ya nyuzi za Latitudo $4^{o}$ na 7o30' Kusini mwa Ikweta na nyuzi za Longitudi $35^{o}$ hadi 37'' Mashariki mwa Meridiani Kuu ya Griniwichi.

1:1 **Mipaka:**

| | | |
|---|---|---|
| Kaskazini | = | Mkoa wa Arusha |
| Mashariki | = | Mkoa wa Morogoro na Tanga |
| Kusini | = | Mkoa wa Iringa |
| Magharibi | = | Mkoa wa Singida |

1:2 **Eneo:**

| | | |
|---|---|---|
| Nchi kavu | = | Kilomita 41,311 za mraba |
| Eneo la Maji | = | Kilomita 41,311 za mraba |
| Jumla | = | Kilomita 41,311 za mraba |

Eneo la Dodoma ni asilimia 5 ya eneo la Tanzania

1:3 **Idadi ya Watu:**

| | | |
|---|---|---|
| 1978 | = | 972,005 |
| 1988 | = | 1,235,277 |
| 1996 | = | 1,493,512 (Maoteo) |

2000 = 1,642,036 (Maoteo)

- Wastani wa ongezeko la idadi ya watu = 2.4
- Idadi ya watu kwa kilomita ya mraba ni 30
- Wastani wa watu katika kaya moja ni watu 6.5

1:4 **Hali ya Hewa:**

(i) **Mvua:**

- Hali kama ya Savanna, na jangwa
- Mvua ni kati ya milimita 400 hadi 900 kwa mwaka
- Mvua inaanza katikati ya Desemba na inaishia mwanzoni mwa Aprili mwaka unaofuata
- Kipindi kirefu cha ukae kuanzia Aprili hadi mwanzoni mwa Desemba

(ii) **J o t o:**

- Kiwango cha juu sentigredi $26^0$
- Kiwango cha chini sentigredi $21^0$

(iii) **Mwinuko:**

- Wastani wa mita 1040 juu ya usawa wa bahari

## 1.5 **Utawala:**

- Wilaya = 5
- Tarafa = 26
- Kata = 136
- Vijiji = 453

## HUDUMA ZA MSINGI, KIWILAYA, 1995

| Huduma | Kondoa | Dodoma Mjini | Dodoma Vijijini | Mpwapwa |
|---|---|---|---|---|
| • Shule za msingi | 172 | 59 | 135 | 141 |
| • Shule za Sekondari | | | | |
| - Serikali | 4 | 4 | 1 | 4 |
| - Binafsi | 1 | 6 | 1 | 1 |
| • Vyuo vya Waalim | 1 | - | - | 1 |
| • Vyuo vya Maendeleo | 1 | - | - | 1 |
| • Vyuo vya Ufundi | - | 2 | - | - |
| • Hospitali | | | | |
| - Serikali | 1 | 2 | - | 1 |
| - Binafsi | - | 3 | 1 | - |
| • Vituo vya Afya | | | | |
| - Serikali | 4 | 3 | 6 | 4 |
| - Binafsi | - | - | - | - |
| • Zahanati | | | | |
| - Serikali | 39 | 3 | 52 | 39 |
| - Binafsi | 11 | 21 | 4 | 10 |
| • Kliniki za kuzunguka | 16 | 8 | 21 | 9 |
| • Huduma za kuzunguka | 106 | 42 | 64 | 55 |
| • Vyuo vya Afya | 1 | - | - | 1 |
| • Idadi ya miradi ya maji | 92 | 36 | 107 | 77 |
| • Miradi ya maji mizima | 76 | 27 | 73 | 63 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| • Asilimia ya watu wapatao maji | 78.9 | 76.7 | 53.4 | 75.2 |

# KIAMBATISHO "B"

## WILAYA YA DODOMA MJINI

1.0 **Mahali Ilipo:**

- wilaya ya Dodoma mjini iko katikati ya mkoa. Inazungukwa pande zote na Dodoma Vijijini. Ipo katikati ya latitudo $3^{o}5'$ na $7^{o}$ kusini mwa Ikweta longitudo $32^{o}$ na $35^{o}$ mashariki mwa Meridiani Kuu ya Griniwichi.

1.2 **Eneo na Idadi ya Wakazi:**

- Eneo lake ni kilomita 2,050 za mraba
- Idadi ya watu 1988 ilikuwa 250,000
- Wastani wa ongezeko la watu ni 2.4% kwa mwaka
- Idadi ya watu mwaka 1996 ni 245,006
- Idadi ya watu mwaka 2000 ni 269,388 (maoteo)
- Watu katika kilomita ya mraba ni 33.5

1.3 **Hali ya Hewa:**

- Ni wilaya kavu muda mwingi
- Wastani wa mvua ni milimita 580
- Wastani wa joto ni sentigredi $15.2^{o}$

1.4 **Utawala:**
- Tarafa 4

- Kata 30 (18 za mji na 12 za vijijini)
- Vijiji 42

**Ramani ya Dodoma Mjini**

## 2.0 Shughuli za Kiuchumi:

- Mazao:- mpunga na uwele, zabibu, mboga mboga na mpunga katika maeneo ya Swaswa.
- Mifugo:- ng'ombe.
- Biashara ndogo ndogo pia zipo.

## 2.1 Miundo mbinu ya Kiuchumi:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| - | Barabara Kuu | - | kilomita | 127 |
| - | Barabara za Kimkoa | - | kilomita | 44 |
| - | Barabara za Kiwilaya | | | 353 |
| | | **Jumla kilomita** | | 524 |

## 3.0 Huduma za Kijamii:

(a) Maji

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Jumla ya miradi ya maji | = | 36 |
| - | Jumla ya miradi inayofaya kazi | = | 27 |
| - | Asilimia ya wanaopata maji | = | 76.7 |

(b) **Elimu**

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Shule za msingi | = | 59 |
| - | Shule za sekondari | = | 10 (4 za serikali, 6 za binafsi) |

(c) **Afya:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| - | Hospitali | = | 3 (serikali 2, binafsi 1) |
| - | Vituo vya afya | = | 3 |
| - | Zahanati | = | 24 (serikali 3, binafsi 21) |
| - | Kliniki | = | 8 |

## KIAMBATISHO "C"

## WILAYA YA KONDOA

1.0 **Mahali Ilipo:**

- Wilaya ipo kaskazini mwa mkoa na ipo kati ya latitudo $4^{o}12'$ kusini mwa Ikweta na longitudo $35^{o}6'$ mashariki mwa Meridiani Kuu ya Griniwichi.

1.2 **Eneo na Idadi ya Wakazi:**

- Wilaya ina kilomita = 13,209 za mraba
- Idadi ya wakazi = 340,267
- Wastani wa ongezeko = 2.1% kwa mwaka
- Idadi ya wakazi 1996 = 452,292
- Watu kwa kilomita ya mraba 25.8

1.3 **Hali ya Hewa:**

- Hali ya ukame ukame
- Wastani wa mvua ni milimita 500-800
- Wastani wa joto ni sentigredi $21^{o}$

1.4 **Utawala:**

| | |
|---|---|
| - Tarafa | 8 |
| - Kata | 32 |
| - Vijiji | 153 |

2.0 Shughuli za Kiuchumi

- Asilimia 70 ya eneo linafaa kwa kilimo

- Mazao makuu ni mahindi, ulezi, uwele na alizeti
- Ng'ombe 237,552 (1984)
- Mbuzi 180,000
- Kondoo 40,388
- Punda 10,400

2.1 **Miundo mbinu ya Kiuchumi:**

- Barabara Kuu = 115
- Barabara za Kimkoa = 244
- Barabara za Kiwilaya = 568
- Barabara za Vijijini = 349

3.0 **Huduma za Kijamii:**

(a) **Afya:**

- Hospitali za serikali = 1
- Vituo vya Afya = 4
- Zahanati 50 (serikali 39, Binafsi 11)
- Vyuo vya afya 1

(b) **Elimu:**

- Shule za msingi = 172
- Shule za Sekondari = 5
- Vyuo vya Ualimu = 1

(c) **Maji:**

- Idadi ya miradi ya maji = 92

- Miradi inayofanya kazi = 76
- Asilimia ya wanaopata maji = 78.9

## KIAMBATISHO "D"

## WILAYA YA DODOMA VIJIJINI

### 1.0 Mahali Ilipo

Dodoma Vijijini iko katikati ya mkoa. Wilaya iko kati ya longitudo $4^o$ na $8^o$ kusini ya Ikweta na latitudo $34^o$ na $38^o$ mashariki mwa Meridiani Kuu ya Griniwichi.

Wilaya inapakana na Manyoni Mkoa wa Singida upande wa kaskazini na kaskazini magharibi, wilaya ya Mpwapwa upande wa mashariki, wilaya ya Iringa upande wa kusini na kusini magharibi.

### 1.2 Eneo na Idadi ya Wakazi:

- Wilaya inalo eneo la kilomita 14,004 za mraba
- Idadi ya watu 352,898 (1988)
- Wastani wa ongezeko la watu = 2.4% kwa mwaka
- Idadi ya wakazi kwa kilomita moja ya mraba ni 33.5

### 1.3 Hali ya Hewa:

- Hali ya kijangwa jangwa
- Mvua yenye wastani wa milimita 500 hadi 700 kwa mwaka kwa muda wa siku 56
- Mvua ni ndogo na haziaminiki
- Wastani wa joto ni sentigredi $22.6^o$

**Ramani ya Wilaya ya Dodoma Vijijini:**

## 1.4 **Utawala:**

| | | |
|---|---|---|
| - | Tarafa | 8 |
| - | Kata | 48 |
| - | Vijiji | 131 |

## 2.0 **Shughuli za Kiuchumi:**

- Shughuli za kilimo na ufugaji ndiyo shughuli kuu za kiuchumi

- Kilimo cha mseto kinatawala, huzalisha mtama, uwele, mahindi, mpunga, karanga, mizabibu, mbegu za mafuta, nyonyo, na alizeti

- Wanyama wanaofugwa ni pamoja na ng'ombe, kondoo, mbuzi

- Kwa Sensa ya 1984, wilaya ilikuwa na:

| | | | |
|---|---|---|---|
| • | Ng'ombe | = | 482,000 |
| • | Mbuzi | = | 180,000 |
| • | Kondoo | = | 125,000 |
| • | Punda | = | 22,000 |
| • | Nguruwe | = | 400 |

## 2.1 **Miundo mbinu ya Kiuchumi:**

- Reli ya kati inapita katika wilaya ya Dodoma Vijijini
- Barabara Kuu kilomita = 191

- Barabara za Kimkoa kilomita = 150
- Barabara za Kiwilaya kilomita = 216
- Barabara za Vijijini kilomita = 558

## 3.0 Huduma za Kijamii:

### (a) Maji:

- Idadi ya miradi ya maji = 107
- Miradi inayofanya kazi = 73
- Asilimia ya wakazi wapatao maji = 53.4%

### (b) Elimu:

- Shule za msingi = 135
- Shule za Sekondari = 2

### (c) Afya:

- Hospitali za serikali = 0
- Hospitali binafsi = 1
- Vituo vya Afya = 6
- Zahanati = 56 (serikali 52, binafsi 4)
- Vyuo vya afya 1

## KIAMBATISHO "E"

## WILAYA YA MPWAPWA:

### 1.0 Mahali Ilipo

- Mpwapwa iko magharibi mwa mkoa

- Mpwapwa inapakana na Dodoma Vijijini kwa upande wa magharibi, Kiteto na Kondoa kwa upande wa kaskazini, Kilosa kwa upande wa mashariki, na kwa upande wa kusini wilaya ya Iringa.

- Mpwapwa ipo kati ya latitudo $5^o$ - $7^o$ kusini mwa Ikweta, na longitudo $36^o$ - $37^o$ kusini ya Meridiani Kuu ya Griniwichi.

### 1.1 Eneo na Idadi ya Wakazi:

- Mpwapwa inalo eneo la kilomita 11.52 za mraba, eneo ambalo ni sawa na asilimia 27.9 ya eneo la Mkoa wa Dodoma.

**Idadi ya Wakazi**

- Kwa sensa ya 1988 Mpwapwa ilikuwa na wakazi 339,498
- Wastani wa ongezeko ni 2.6% kwa mwaka
- Watu mwaka 1996 ni 410,453
- Watu mwaka 2000 ni 451,270

- Idadi ya watu katika kilomita moja ya mraba ni 29

**Ramani ya Wilaya ya Mpwapwa:**

## 1.2 Hali ya Hewa:

- Mpwapwa iko mita 1040 juu ya usawa wa bahari
- Wastani wa joto wa sentigredi $24^o$
- Wastani wa mvua wa milimita 700 kwa mwaka, hasa kati ya Desemba hadi Aprili.

## 1.3 Utawala:

| | | |
|---|---|---|
| - Tarafa | = | 6 |
| - Kata | = | 26 |
| - Vijiji | = | 128 |

## 2.0 Shughuli za Kiuchumi:

- Shughuli kubwa ni kilimo na ufugaji

- Asilimia 90 ya watu wanaishi vijijini

- Asilimia 70 ya eneo linafaa kwa kilimo

- Mazao makuu ni mahindi, uwele, alizeti na viazi mviringo

- Kwa sensa ya wanyama ya 1984 Mpwapwa ilikuwa na jumla ya mifugo 353,242 kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| • Ng'ombe | = | 221,902 |
| • Mbuzi | = | 88,491 |
| • Kondoo | = | 33,121 |
| • Punda | = | 4,292 |
| • Nguruwe | = | 4,986 |

## 2.1 Miundo mbinu ya Kiuchumi:

- Barabara Kuu = kilomita 123
- Barabara za Kimkoa = kilomita 233
- Barabara za Kiwilya = kilomita 110
- Barabara za Vijijini = kilomita 847
- Reli ya kati inapita katikati ya wilaya ya Mpwapwa kituo kikubwa ni Gulwe

3.0 **Huduma za Kijamii:**

(a) **Afya:**

- Hospitali za serikali - 1
- Vituo vya afya - 4
- Zahanati = 49 (serikali 39, binafsi 10)
- Kliniki za garini - 9
- Huduma za mbali - 55

(b) **Elimu:**

- Shule za msingi - 141
- Shule za sekondari = 5 (serikali 4, binafsi 1)
- Vyuo vya Ualimu - 1
- Vyuo vya maendeleo - 1

(c) **Maji:**

- Idadi ya miradi ya maji - 77
- Inayofanyakazi - 63
- Asilimia ya watu wanaopata maji- 75.2

## KIAMBATISHO "F"

# 1.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU TANZANIA

## 1.1 MAHALI ILIPO:

Latitudo $1^0$-$12^0$ Kusini, Longitudo $29^0$-$41^0$ Mashariki

## 1.2 MIPAKA YA NCHI:

| | |
|---|---|
| Kaskazini: | Kenya na Uganda |
| Magharibi: | Burundi, Rwanda na Zaire |
| Kusini: | Zambia, Malawi na Mozambique |
| Mashariki: | Bahari ya Hindi |

## 1.3 UKUBWA/ENEO:

| | |
|---|---|
| Nchi kavu: | 881,289 $km^2$ |
| Maji (bara): | 61,495 $km^2$ |
| Jumla: | 942,784 $Km^2$ |

## 1.4 UKUBWA WA ENEO LA KILA MKOA TANZANIA BARA ($Km^2$):

**TANZANIA 942,784**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Arusha | 84,567 | Morogoro | 70,799 |
| Pwani | 32,407 | Mwanza | 35,248 |
| **Dodoma** | **41,311** | Lindi | 66,046 |
| Iringa | 58,936 | D'Salaam | 1,393 |
| Kigoma | 45,066 | Rukwa | 75,240 |
| Kagera | 39,627 | Ruvuma | 66,477 |
| Kilimanjaro | 13,309 | Shinyanga | 50,781 |
| Mara | 30,150 | Singida | 49,341 |
| Mbeya | 62,420 | Tabora | 76,151 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mtwara | 16,707 | Tanga | 26,808 |

## 1.5 IDADI YA WATU:

**HESABU YA IDADI YA WATU NA WASTANI WA UMRI WA KUISHI NCHINI TANZANIA KATIKA KILA MKOA 1967, 1978, 1988, 1996**

| MKOA | IDADI YA WATU | | | | UMRI WA KUISHI (WASTANI) 1988 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1967 (No.) | 1978 (No.) | 1988 ('000) | 1996** ('000) | Me Miaka | Ke Miaka |
| **Dodoma** | **709,380** | **972,005** | **1,234.9** | **1,472.5** | **45** | **47** |
| Arusha | 610,474 | 926,223 | 1,348.4 | 1,784.0 | 57 | 58 |
| Kilimanjaro | 652,722 | 902,437 | 1,106.0 | 1,703.5 | 57 | 62 |
| Tanga | 771,060 | 1,037,767 | 1,307.3 | 1,521.8 | 48 | 51 |
| Morogoro | 682,700 | 939,264 | 1,254.0 | 1,519.4 | 45 | 48 |
| Pwani | 428,041 | 516,586 | 636.5 | 740.9 | 46 | 51 |
| Dar es Salaam | 356,286 | 843,090 | 1,357.6 | 1,945.7 | 50 | 50 |
| Lindi | 419,853 | 527,624 | 645.0 | 744.8 | 46 | 48 |
| Mtwara | 621,293 | 771,818 | 887.4 | 976.7 | 44 | 48 |
| Ruvuma | 395,447 | 561,575 | 781.4 | 1,001.3 | 48 | 50 |
| Iringa | 689,905 | 925,044 | 1,206.0 | 1,472.9 | 44 | 47 |
| Mbeya | 753,765 | 1,079,864 | 1,472.7 | 1,857.0 | **45** | 48 |
| Singida | 457,938 | 613,949 | 789.9 | 949.4 | 54 | 55 |
| Tabora | 502,068 | 817,907 | 1,033.8 | 1,232.6 | 53 | 54 |
| Rukwa | 276,091 | 451,897 | 693.3 | 954.7 | 44 | 47 |
| Kigoma | 473,443 | 648,941 | 857.8 | 1,047.6 | 47 | 49 |
| Shinyanga | 899,468 | 1,323,535 | 1,768.6 | 2,194.83 | 48 | 51 |
| Kagera | 658,712 | 1,009,767 | 1,358.8 | 1,659.5 | 44 | 45 |
| Mwanza | 1,055,883 | 1,443,379 | 1,874.4 | 2,270.9 | 48 | 50 |
| Mara | 544,125 | 723,827 | 968.6 | 1,202.0 | 46 | 48 |
| Tanzania Bara | 11,958,654 | 17,036,499 | 22,582.4 | 28,252.2 | 49 | 51 |
| Zanzibar Kaskazini | 56,360 | 77,017 | 97.1 | 119.0 | 46 | 52 |
| Zanzibar Kusini | 39,087 | 51,749 | 70.2 | 91.8 | 46 | 48 |
| Zanzibar Mjini | 95,047 | 142,041 | 208.4 | 290.4 | 45 | 50 |
| Pemba Kaskazini | 72,015 | 106,290 | 137.4 | 172.6 | 46 | 47 |
| Pemba Kusini | 92,306 | 99,014 | 127.7 | 160.4 | 45 | 50 |
| Zanzibar | 354,815 | 476,111 | 640.7 | 834.2 | 45 | 49 |
| Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 12,313,469 | 17,512,610 | 23,223.1 | 29,086.4 | 49 | 51 |

Chanzo: Idara ya Takwimu

**MAELEZO: Idadi ya Watu 1996 ni makadirio kutokana na mwenendo wa ukuaji wa Idadi ya hesabu ya watu tangu sensa ya mwaka 1978 hadi 1988.

## 1.6 MATUMIZI YA ARDHI (HA):

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mashamba Madogo | - | 4.1 | - | 5% |
| Mashamba Makubwa | - | 1.1 | - | 1% |
| Malisho | - | 35.0 | - | 39% |
| Misitu na Miti | - | 44.0 | - | 50% |
| Ardhi nyingine | - | 4.4 | - | 5% |
| **Jumla** | **-** | **88.6** | **-** | **100%** |

## 1.7 ARDHI KILIMO NA MIFUGO:

Ardhi ya kufaa (Ha.) 3,634,000

## 1.8 MAZIWA:

| | | |
|---|---|---|
| Victoria | - | 34,850 $km^2$ |
| Tanganyika | - | 13,350 $km^2$ |
| Nyasa | - | 5,600 $km^2$ |
| Rukwa | - | 2,850 $km^2$ |
| Eyasi | - | 1,050 $km^2$ |
| Natron | - | 900 $km^2$ |
| Manyara | - | 320 $km^2$ |

## 1.9 MILIMA: (Mita za urefu kutoka usawa wa Bahari)

| | | |
|---|---|---|
| Kilimanjaro: | - | 5,895 |
| Meru: | - | 4,566 |

## 1.10 HALI YA HEWA:

### (a) MVUA:

Kuna misimu miwili ya mvua katika Tanzania:

(i) Vuli: Mvua za vuli hunyesha katika miezi ya Oktoba, Novemba na Desemba

(ii) Masika Mvua za masika hunyesha katika miezi ya Machi, Aprili na Mei.

Mtawanyiko wa mvua ni mzuri katika mwaka mzima ingawa zipo tofauti kati ya sehemu mbalimbali

Mvua nyingi hunyesha hasa katika miezi ya Machi na Mei

### (b) HALI YA JOTO:

Wastani wa juu wa joto (Nyuzijoto)

| | **Januari**. | **Aprili** | **Julai** | **Oktoba** |
|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 31.6 | 30.1 | 28.6 | 31.3 |
| Arusha | 28.9 | 25.3 | 21.1 | 27.3 |
| Dodoma | 31.4 | 28.4 | 26.0 | 30.2 |

Wastani wa chini wa joto (Nyuzijoto)

| | **Januari**. | **Aprili** | **Julai** | **Oktoba** |
|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 23.3 | 22.9 | 18.3 | 31.3 |
| Arusha | 12.2 | 16.9 | 12.6 | 27.3 |
| Dodoma | 19.2 | 13.5 | 16.2 | 30.2 |

## 1.11 PATO LA TAIFA (1996)

| | | |
|---|---|---|
| Kwa bei za mwaka unaohusika (Shilingi milioni) | - | 3,317,634 |
| Kwa bei za mwaka 1992 (Shilingi milioni) | - | 1,354,038 |

## 1.12 WASTANI WA PATO LA MTU BINAFSI (1996)

| | | |
|---|---|---|
| Kwa bei za mwaka unaohusika (Tsh.) | - | 117,230.9 |
| Kwa bei za mwaka 1992 (Tsh.) | - | 47,845.9 |

# 2.0 HUDUMA ZA JAMII

## 2.1 AFYA:

Idadi ya Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati

| MWAKA | HOSPITALi | VITUO VYA AFYA | ZAHANATI |
|---|---|---|---|
| 1960 | 98 | 22 | 975 |
| 1980 | 149 | 239 | 2,600 |
| 1990 | 173 | 276 | 3,014 |

## 2.2 ELIMU:

Ulinganisho wa kiwango cha kuandikisha wanafunzi katika mashule kati ya nchi za Afrika Mashariki 1995.

| NCHI | IDADI | |
|---|---|---|
| | SHULE ZA MSINGI | SHULE ZA SEKONDARI |

| | | |
|---|---|---|
| KENYA | 94 | 28 |
| UGANDA | 76 | 20 |
| TANZANIA | 67 | 13 |

## 2.3 MAJI:

Hali ya usambazaji wa huduma ya maji safi mijini na vijijini Tanzania Bara 1994

| JUMLA YA WATU (000) | IDADI YA WATU MJINI (000) | WANAOPATA MAJI (000) | % | IDADI YA WATU VIJIJINI (000) | WANAOPATA MAJI (000) | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 27,061.7 | 5,363.4 | 3,668.6 | 68.5 | 21,698.3 | 10,046.3 | 46.3 |

Chanzo: Wizara ya Maji, Madini na Nishati, 1994

## 3.0 HIFADHI ZA TAIFA:

| JINA LA HIFADHI | MAHALI ILIPO NA MAELEZO MUHIMU |
|---|---|
| **HIFADHI YA TAIFA YA SERENGETI** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ipo karibu na mpaka wa Mkoa wa Arusha na Mara, mwendo wa kilometa 32 kutoka mjini Arusha.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Hifadhi ina eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 14,763. Ni hifadhi iliyokubwa zaidi na ya zamani Tanzania iliyoanzishwa baada ya kuanzishwa na wakoloni wa Kiingereza mwaka 1951.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Kongoni kiasi cha 1.7 milioni, Simba 3,000, Anuwai 35 za wanyama pori na 500 za ndege wakiwemo Nyati, Duma, Chui n.k. |

| | |
|---|---|
| **HIFADHI YA TAIFA YA LAKE MANYARA** | **MAHALI ILIPO:**<br>Ipo kiasi cha kilometa 125 kusini magharibi mwa mji wa Arusha.<br><br>**UKUBWA:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Lake Manyara ina ukubwa wa kilo meta za mraba 320. Kati ya hizo kilometa 230 za mraba ni eneo la Ziwa Manyara.<br><br>**VIVUTIO:**<br>Bonde la Ufa kwa upande wa magharibi na Ziwa kubwa (Manyara) kwa upande wa chini. Misitu yenye mito na chemchemi asili. Simba wenye kukwea mitini, aina mbalimbali za hayawani na anuwai 360 za ndege wakiwemo Tembo, Viboko, Chui, Nyani n.k. |
| **HIFADHI YA TAIFA YA TARANGIRE** | **MAHLI ILIPO:**<br>Kusini mwa mji wa Arusha kando kando ya barabara kuu iendayo Dodoma. Hifadhi imeanzishwa mwaka 1970.<br><br>**UKUBWA:**<br>Hifadhi vya Taifa ya Tarangire ina eneo la kilometa za mraba 2,600.<br><br>**VIVUTIO:**<br>Chatu wenye kukwea mitini, Pundamilia, Kongoni, Tembo, Nyati, Swala, Choroa n.k. |
| **HIFADHI YA TAIFA YA ARUSHA (MONELLA)** | **MAHALI ILIPO:**<br>Hifadhi ipo katikati ya ulipo mlima Meru na Kilimanjaro. Mwanzoni ilijulikana kama hifadhi ya Taifa ya Ngudoto hadi mwaka 1967. Ilipewa hadhi ya kuwa hifadhi ya Taifa Mwaka 1960.<br><br>**UKUBWA:**<br>Ukubwa wa eneo la hifadhi hii ni kilometa za mraba 140.<br><br>**VIVUTIO:**<br>"Ngudoto Crater", Ziwa Momela, mlima Meru, na misitu ya asili ya Momela. Anuwai mbalimbali za wanyama pori na ndege wakiwemo Tembo, Viboko, Nyani, Funo/Mindi na aina mbalimbali za ndege. |

| | |
|---|---|
| **HIFADHI YA TAIFA YA KILIMANJARO** | **MAHALI ILIPO**:<br>Hifadhi ya Kilimanjaro ipo katika mlima wa Kilimanjaro ambao ndio chimbuko la jina lake. Hifadhi hii imeanzishwa mwaka 1973.<br><br>**UKUBWA**:<br>Mipaka yake inajumuisha misitu ya asili iliyopo maeneo yote ya chini na pembezoni/karibu na mlima. Ukubwa wa eneo la hifadhi ni kilometa za mraba 760.<br><br>**VIVUTIO**:<br>Mlima Kilimanjaro na vilele vyake vitatu: Shira (3,962 meta), Mawenzi (5,149 meta) na Kibo (5,895 meta) juu ya usawa wa bahari. Zipo pia anuwai mbalimbali za wanyama pori na ndege. |
| **HIFADHI YA TAIFA YA MIKUMI** | **MAHALI ILIPO**:<br>Hifadhi hii ipo kiasi cha kilometa 216 kando kando mwa barabara kuu itokayo Dar es Salaam kwenda Zambia eneo la Mikumi Mkoa wa Morogoro/Iringa. Imeanzishwa mwaka 1964.<br><br>**UKUBWA**:<br>Hifadhi ya Taifa ya Mikumi hupakana na hifadhi kubwa ya wanyama kuliko zote katika Afrika ya Selous. Ni ya tatu kati ya hifadhi za Taifa kubwa ikipitwa tu na hifadhi za Serengeti na Ruaha. Ina eneo la kilometa a mraba 3,230.<br><br>**VIVUTIO**:<br>Tambarare zinazozunguka mto Mkata. Utajiri mkubwa wa Flora na Fauna aina aina. Namna mbalimbali za wanyama pori wakiwemo Tembo, Pundamilia, Nyati, Twiga, Viboko, Simba, Swalapala n.k. |

| | |
|---|---|
| **HIFADHI YA TAIFA YA UDZUNGWA** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Hifadhi hii ipo kusini mwa hifadhi ya Taifa ya Mikumi kando kando mwa barabara kuu ya Mikumi-Ifakara. Ilianzishwa mwaka 1992.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Udzungwa ambayo asili ya jina lake linatokana na milima maarufu ya Udzungwa ina eneo la kilometa za mraba 1990.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Namna mbalimba na kipekee za Fauna na Flora zilizopelekea ipewe hadhi ya kuwa hifadhi ya Taifa. Milima ya Udzungwa ambayo ni chanzo asili cha mito na chemchemi za maji, ukiwepo mto maarufu wa kilombero wenye kumwagilia shamba la hekta nyingi za kilimo cha miwa la kilombero. Vivutio vingine ni wanyama pori: Simba, Nyati, Twiga n.k. |
| **HIFADHI YA TAFIA YA RUAHA** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Jina Ruaha hutokana na neno la kihehe **"Luvaha"** kumaanisha mto. Hifadhi hii ipo kilometa 130 magharibi mwa mji wa Iringa.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Hifadhi ina ukubwa wa kilometa za mraba 12,950. Ni ya pili kwa ukubwa nchini na imeanzishwa mwaka 1964.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Mto wa Ruaha ni mojawapo yakivutio kikubwa. Mamia ya namna mbalimbali za Flora. Wanyama aina aina wakiwemo Mamba, Viboko, Tembo n.k. |

| | |
|---|---|
| **HIFADHI YA TAIFA YA KATAVI** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Katavi ipo wilayani Mpanda Mkoa wa Rukwa. Ilianzishwa mwaka 1974.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Katavi iliyopo kiasi cha umbali wa kilometa 40 kusini mashariki mwa mji wa Mpanda ina ukubwa wa kilometa za mraba 2253.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Ziwa Chala na Chada pamoja na Chemchemi na mito ambayo maji yake hutiririka kwenye Ziwa Rukwa ni vivutio vya kipekee kwa watalii katika/ kwenye hifadhi hii. Wanyama mbalimbali wakiwemo Pundamilia, Mbelele, Pofu, Chui, Nyati, Simba, Tembo, Paa/Palakala, Kulungu n.k. |
| **HIFADHI YA TAIFA YA MAHALE** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Ikiwa umbali wa kiasi cha kilometa 120 kusini mwa mji wa Kigoma na kandokando ya ufukwe wa Ziwa Tanganyika, hifadhi ya Taifa ya Mahale ni kivutio kingine maarufu katika urithi wa maliasili za Tanzania.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Mahale ina ukubwa wa karibu kilometa za mraba 410 na ilichapishwa kwenye gazeti la serikali mwaka 1948.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Idadi kubwa ya Sokwe ni mojawapo ya kivutio cha kusisimua katika hifadhi hii. Ipo pia idadi nzuri ya Nyani wa namna mbalimbali wakiwemo aina ya nyani wekundu wajulikanao kwa lugha ya kiingereza kama “Red Colobus Monkey”. |

| | |
|---|---|
| **HIFADHI YA TAIFA YA RUBONDO** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Hifadhi hii ipo kati ya mojawapo ya vifungu visiwa (Archiplelagos) vilivyopo katika Ziwa Victoria.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Ina ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 460 na imeanzishwa mwaka 1977.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Sokwe na namna mbalimbali za wanyama pori wakiwemo Viboko, Twiga na Tembo. Kutokuwepo kwa Simba wala watu na Chui ni hakikisho tosha kuivinjari hifadhi kwa usalama na pia kufanya shughuli za uvuvi wa boti kwa msaada wa "wadeni" au mlinzi hifadhini. |
| **HIFADHI YA TAFIA YA NGORONGORO** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Ngorongoro ipo magharibi mwa mji wa Arusha umbali wa kiasi cha kilometa 230.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Hifadhi hii ina ukubwa wa kilometa za mraba 8,320.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Kongoni, Simba, Nyati, Chui, aina mbalimbali za ndege, Twiga, Tembo n.k. Inakadiriwa kwamba wapo Sokwe 700 katika hifadhi ya Taifa ya Mahale na anuwai 15 za Nyani ambazo makaazi yao ya asili ni sawa na yale ya Sokwe. |
| **HIFADHI YA TAIFA YA GOMBE** | **<u>MAHALI ILIPO</u>:**<br>Hifadhi ya Taifa ya Gombe ipo kilometa 16 kusini ya mji wa kigoma magharibi mwa Tanzania. Ni mwanya mwembamba wa eneo la milima linalopakana kwa upande wa magharibi na bonde la Ufa na Ziwa Tanganyika kwa upande wa mashariki.<br><br>**<u>UKUBWA</u>:**<br>Ina ukubwa wa kiasi cha kilometa za mraba 52 na ilianzishwa mwaka 1968.<br><br>**<u>VIVUTIO</u>:**<br>Misitu ya kujani kibichi cha kudumu na mamalia wa hali ya juu wakiwemo Sokwe na anuwai mbalimbali za Nyani - wakiwemo Mbega (Red Colobus), Nyani (Baboons), Nyani wekundu/Bluu na Ngedere. |